# SIRAJI IMULIKAYO

Na

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian

Masihi Mau'udi na Imam Mahdi

*Siraji Imulikayo*

Tafsiri ya Kiswahili ya *Siraje Munir* (Kiurdu)
Swahili translation of *Siraaj-e-Muneer* (Urdu)

Mwandishi:
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian

Mfasiri:
Sheikh Yusuf Athumani Kambaulaya

Chapa ya Kwanza (Kiurdu): Qadian 1897
Tafsiri ya Kiswahili: Tanzania, Kenya 2019

© Islam International Publications Ltd.

Kwa Maelezo Zaidi:
Tanzania:
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed, S.L.P. 376, Dar es Salaam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744

Kenya:
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi, Kenya
Simu: +254222111031

Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salaam, Tanzania / Nairobi, Kenya

Cover design by: Usman Nasir Choudhary

ISBN: 978-1-84880-559-0
10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

# MAELEZO YA MWENEZI

Siraji Imulikayo — Siraje Munir — ni kitabu alichokiandika Seyidna Ahmad[as], Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, mnamo Mei 1897. Ndani ya kitabu hiki ametaja bishara zake 37 kubwa ambazo yeye alifunuliwa na Mwenyezi Mungu, alizochapisha miaka kadha mapema kabla hazijatimia. Hususan ameeleza kinaganaga bishara kuwahushu Atham na Lekhram.


Katika sehemu ya mwisho, amezitoa barua zile pia alizoandikiana na Hadhrat Khwaja Ghulam Farid wa Chachrhan. Hadhrat Khwaja amedhihirisha katika barua zake ikhlasi na upendo wake mwingi kwa Seyidna Ahmad[as].

Kitabu hiki toka Kiurdu amekifasiri Sheikh Yusuf Athumani Kambaulaya. Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani alipitia tafsiri na kisha Sheikh Adnan Hashimi naye akaidurusu tafsiri hii. Kabla ya kupelekwa mtamboni niliilinganisha na matini ya Kiurdu kwa uangalifu. Sheikh Ansar Hussain akapanga herufi zake kwa kompyuta. Syed Tanwir

Mujtaba naye akaishughulikia fometi yake. Mwenyezi Mugnu awape malipo bora wote walioitia sehemu yao katika kazi hii njema. Mwenyezi Mungu Awanufaishe sana wote watakaopata bahati nzuri ya kuisoma.

Jamil. R. Rafiq
Wakilut Tasnif
Tahrike Jadid
Rabwah, Pakistan 25 Machi 2018

Jalada la chapa ya mara ya kwanza


مطبوعہ ضیاء الاسلام

سراج منیر ۱۳۱۴

مشتمل بر نشانہائے ربِّ قدیر

قادیان دارالامن والامان
مئی سنہ ۱۸۹۷ء

Jalada la chapa ya kwanza

Imepigwa chapa
katika Dhiaul
Islam

# Siraji Imulikayo

## Imejumuisha Ishara za Mola Mweza

Qadian,
Darul Amni Wal Amaan
Mei 1897

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ نَحۡمَدُہٗ وَنُصَلِّیۡ عَلٰی رَسُوۡلِہِ الۡکَرِیۡمِ[1]

جَآءَ الۡحَقُّ وَزَھَقَ الۡبَاطِلُ اِنَّ الۡبَاطِلَ کَانَ زَھُوۡقًا[2]

بنگر اے قوم نشانہائے خداوند قدیر
چشم بکشاکہ برچشم نشانے است کبیر

رو بدو آرکہ گر او بپذیرد رُو تافت
ورنہ این روئے سیہ ہست بتراز خنزیر

چون بتابی سرخود زاں ملک ارض و سما
گربگیر د ز غضب پس چہ پنہ ہست و ظہیر

قمر و شمس و زمین و فلک و آتش و آب
ہمہ در قبضۂ آں یار عزیز اند اسیر

قدسیان جملہ بلرزند ازان ہیبت پاک
انبیا را دل و جان خون و الم دامنگیر

جنت و دوزخ سو زندہ ازوے لرزند
توچہ چیزی چہ ترا مرتبہ اے کِرم حقیر

چند این جنگ و جدل ہا بخدا خواہی کرد
توبہ کن توبہ مگر درگذر و از تقصیر

من اگر در نظر یار مقامے دارم
پس چہ نقصان ز نکوہیدن تو وازتکفیر

لعنت آن است کہ از سوئے خدا می بارد
لعنت بدگہران است یکے ہرزہ نفیر

اے برادر رہ دین است رہ بس دشوار
خاک شو خاک مگر باز کنندش اکسیر

تو ہلاکی اگر از کبر بتابی سرخویش
من از و آمدم وباتو بگویم چو نذیر

آن خدائے کہ از و خلق و جہان بیخبر اند
برمن او جلوہ نمودست گراہلی بپذیر

---

[1] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu. Tunamhimidia Yeye na tunamsalia Mtume wake Mtukufu.

[2] Ukweli umefika na uwongo umetoweka, hakika uwongo ndio wenye kutoweka

Tafsiri:

Ewe kaumu ziangalie ishara za Mungu Mweza. Fumbua macho, kwani ipo ishara kubwa sana mbele ya macho yako.

Geukia upande Wake, kama Akikubali, uso utang'aa, waila uso huu mweusi u mbovu kuliko hata nguruwe.

Mbona unampa kisogo Mfalme wa mbingu na ardhi! Kama ghadhabu Yake ikikukamata, ni nani, basi, awezaye kukupa pa kimbilio au msaada?

Mwezi na jua, ardhi na mbingu, moto na maji, vyote hivyo ni mahabusu ndani ya utawala wa Mpendwa Huyo Mwenye heshima.

Malaika wote wanatetemeka kwa haiba yake. Nafsi na mioyo ya manabii inayo majonzi, nao wamezingirwa na hofu.

Pepo na pia Jahanamu iunguzayo zinatetemeka kwa kumhofia. Ewe kidudu dufu, u kitu gani, unalo daraja gani!

Mpaka lini utaendelea kupigana vita hii na Mungu? Tubu, tubu ili Akusamehe makosa

yako.

Kama mimi, ninalo daraja fulani machoni mwa Mpendwa, basi wewe kunilaumu na kunikufurisha unaweza kunihasiri nini?

Laana ndiyo ile iteremkayo toka kwa Mungu; laana ya watu waovu ndiyo tu kelele za ovyo zisizo na maana.

Ewe ndugu! Njia ya dini ni njia ngumu sana, jinyenyekeze, kuwa vumbi, ili Akufanye uwe tiba ya magonjwa yote.

Kama utakengeuka kwa kiburi, utaangamia. Mimi nimetoka Kwake, nami nakufahamisha nikiwa kama mwonyaji.

Yule Mungu Ambaye mahuluku na ulimwengu haunayo habari Yake, Amejidhihirisha kwangu. Kama u mwenye akili, basi nikubali mimi.

Amma ba'du, iwe wazi kuwa wakati huu nitaelezea ishara moja kubwa ya Mwenyezi Mungu. Wabarikiwe wale watakaoisoma kwa makini na kisha kufaidika nayo. Kumbukeni kabisa kuwa Mungu Hampi mwongo heshima ile wanayopewa manabii wake watukufu na wateule. Mla nyamafu, mwongo ana

haki gani kuwa mbingu idhihirishe ishara kwa ajili yake na ardhi ionyeshe maajabu kinyume na kawaida kwa ajili yake? Basi, Enyi wazee na wenye busara wa kaumu! fikirieni juu ya matukio kwa utulivu. Je matukio haya yanatokana na waongo au wakweli? Je yupo yeyote aliyesikia kuwa kwa ajili ya mwongo ishara zimedhihiri huko mbinguni? Je yupo mtu aliyeona kuwa mwongo amewashinda wakweli katika maajabu yake? Je mtu yeyote anakumbuka kuwa mwongo na mzushi alipewa muhula wa miaka ishirini na mitano tangu kuanzia siku ya kuzua kama nilivyojaliwa mimi. Mwongo anasagwa kama kunguni na anatoweshwa kama kiputo. Kama waongo na wazushi wangepewa muda mrefu kiasi hicho na ishara za wakweli zingedhihirishwa kwa ajili yao, basi machafuko yangeenea duniani na ulimwengu ungeharibika. Basi, wakati muonapo kuwa kelele zimepigwa sana dhidi ya mdai fulani na dunia imeelekea kumpinga, na vimbunga vingi vimevuma na tufani nyingi zikaja lakini hakuanguka, basi mara moja jihadharini na shikeni ucha Mungu isije mkahisabiwa kuwa wenye kupigana na Mungu.

Mkweli kamwe hatahilikishwa kwa mikono yenu, na mkweli hataangamizwa kwa njama zenu. Msiyarefushe maneno kwa bahati mbaya. Kadri

mtakavyofanya ukali huu, utawarudieni tu, na kadri mtakavyomtakia fedheha, hiyo itawageukieni. Enyi wenye bahati mbaya! je mnayo imani juu ya Mungu pia au hapana? Kwa nini Mungu Aitangulize miradi yenu juu ya miradi Yake, na silsila hii Aliyonuia kuiimarisha tangu zamani kwa nini Aiangamize kwa ajili yenu? Ni nani miongoni mwenu atakayebomoa nyumba yake kwa kuambiwa na majununi fulani na kuikata bustani yake, na kuwaua watoto wake kukaba roho zao? Basi, Enyi majahili na mlionyimwa hekima za Mungu, yawezekanaje kuwa kwa kukubali dua zenu za kipumbavu, Mungu Aangamize bustani yake na nyumba yake, na mlelewa wake. Zindukeni na tegeni masikio kwamba mbingu yanenaje! Na zitambueni nyakati za ardhi na misimu yake mkapate heri, na ili msikatwe kama mti uliokauka na siku za maisha yenu ziwe nyingi. Acheni shutuma za upuuzi na jiepusheni na kukosoa pasipo haki na jikingeni na mawazo ya kifasiki. Msinirushie tuhuma za uongo kuwa mimi nimedai unabii kwa uhakika. Je, hamkusoma kuwa *Muhaddath* pia huwa mtume? Je, hamkumbuki ile kira'at[3] ya [4]وَلَا مُحَدَّثٍ. Basi shutuma hii ni ya kiupuuzi namna gani kuwa nimedai

[3] Somo jingine la aya. Mfasiri.

[4] Hakuna Muhaddath.

kuwa mtume? Enyi majahili, elezeni kuwa yule anayetumwa ataitwa Mursal au Rasul kwa Kiarabu au ataitwa jina jingine? Lakini kumbukeni kuwa katika ufunuo wa Mungu muradi wake mahali hapa sio maana ya asili inayohusiana na mtume aletaye sheria, bali yule anayetumwa, yeye huwa ni Mursal. Ni kweli kuwa ule ufunuo ambao Mungu Ameniteremshia, ndani yake kunihusu mimi maneno Nabii, Mursal na Rasul yamo kwa wingi. Hivyo, maneno haya hayatumiki kwa maana halisi.[5] وَلِكُلٍّ اَنْ يَّصْطَلِحَ. Basi hii ni istilahi ya Mungu ambayo sawa nayo Ametumia maneno kama haya.

Sisi tunakubali na kukiri kuwa kutokana na maana halisi ya neno *Nubuwwat* hakuna baada ya Mtume[saw] nabii mpya wala wa zamani anayeweza kuja. Kurani Tukufu inazuia kuja kwa Manabii kama hao, lakini kwa maana ya kimajazi, Mungu Ana hiari ya kumtaja mwenye kufunuliwa kwa neno Nabii au Mursal. Je hamkusoma zile Hadithi mlimoandikwa رَسُوْلُ رَسُوْلِ اللهِ[6]. Mpaka sasa Waarabu wanamwita aliyetumwa na mtu kuwa Rasul7. Sasa kwa nini iwe haramu kwa Mungu kutumia neno Mursal kwa maana ya kimajazi pia.

---

[5] Na kila mtu ana haki ya kuunda istilahi.

[6] Mjumbe wa Mtume wa Mungu.

[7] Mtume au mjumbe.

Je, hamkumbuki فَقَالُوۡۤا اِنَّاۤ اِلَيۡكُمۡ مُّرۡسَلُوۡنَ[8] katika Kurani Tukufu. Angalieni kwa uadilifu, je huu ndio msingi wa kukufurisha? Kama mkiulizwa mbele ya Mungu, niambieni mnayo dalili gani juu ya kunikufurisha. Nasema mara kwa mara kuwa maneno haya Rasul na Mursal na Nabii yamo kutoka kwa Mwenyeji Mungu katika ufunuo kunihusu mimi bila shaka, lakini hayachukuliwi katika maana yake ya asili. Na kwa vile hayo hayachukuliwi katika maana ya asili, vivyo hivyo huku kumtaja Nabii kulikokuja ndani ya Hadithi kwa ajili ya Masihi Mau'udi, pia hakuchukuliwi katika maana yake ya asili. Hii ndiyo elimu Aliyonipa Mungu. Mwenye kutaka kuelewa, na aelewe. Haya ndiyo yaliyofunuliwa kwangu kwamba milango ya unabii halisi, baada ya Khatamun Nabiyyin[saw] imefungwa kabisa, sasa kutokana na maana ya kweli hakuna Nabii mpya anayeweza kuja wala Nabii wa zamani. Lakini wapinzani wetu wadhalimu wanafikiria kuwa milango ya "Khatme Nubuwwat" haikufungwa kikamilifu. Bali kwao kwa ajili ya kurejea Nabii Mwisraeli Masihi dirisha moja bado liko wazi. Basi wakati ambapo baada ya Kurani pia nabii halisi mkweli atakuja, na silsila ya ufunuo

---

[8] Nao walisema: Kwa hakika sisi tumetumwa kwenu. Sura Yaa Siin, 36: 15.

wa unabii itaanza, hapo semeni vipi na kwa namna gani itakuwa Khatme Nubuwwat. Je, wahyi wa Nabii utaitwa wahyi wa unabii au kitu kingine? Je, hii ni itikadi yenu kuwa Masihi wenu wa kubuni atakuja pasipokuwa na bahati ya kupata wahyi kabisa? Tubuni, na muogopeni Mungu na msiruke mipaka. Kama mioyo haikugeuka kuwa migumu, basi kwa nini mnajasiri kumkufurisha bila sababu mtu ambaye anamfahamu Mtume[saw] kuwa Khaatamul Ambiyya kwa maana halisi, na anaikubali Kurani kuwa Khatamul Kutub, anawaamini mitume wote, na ni mwenye kuelekea kibla, na anaielewa halali ya Sheria kuwa ni halali na haramu kuwa haramu.

Enyi wazushi! Mimi sijamvunjia heshima Nabii yeyote. Mimi sikusema dhidi ya itikadi yoyote iliyo sahihi. Lakini kama nyinyi wenyewe hamwelewi, nifanyeje mimi? Ninyi wenyewe mnakubali kuwa shahidi wa kawaida anaweza kumzidi Nabii mkubwa katika kuwa shahidi. Na hii ni kweli kuwa mimi sioni fadhili ya Mungu iliyo juu yangu kuwa kidogo kuliko Masihi, lakini huu si ukafiri, bali ni kumshukuru Mungu kwa neema yake. Ninyi hamjui siri za Mungu, ndiyo maana mwaifikiria kuwa kufuru.

Mtamsemaje aliyesema هُوَ اَفۡضَلُ مِنۡ بَعۡضِ الۡاَنۡبِيَاءِ[9]. Kama mimi machoni mwenu ni kafiri, basi ni kafiri kama mwana wa Mariamu alivyokuwa kafiri machoni mwa waandishi wa Wayahudi. Ninayo mambo mengi ya fadhili za Mungu kuliko hayo, lakini ninyi hamwezi kuyavumilia. Kumbukeni vizuri kuwa si rahisi kuniita kafiri. Ninyi mmebeba mzigo mzito kichwani, nanyi mtaulizwa kuhusu maneno hayo yote!!

Enyi watu wenye bahati mbaya! Mmeangukia wapi? Yalikuwa matendo gani mabaya yaliyofichika ambayo yaliwasibuni. Kama mngekuwa na wema hata chembe, Mungu Hangewapoteza. Bado upo muda kidogo, na thawabu nyingi mmekwisha poteza, jizuieni. Je, mtapigana na Mungu mfano wa yule mpumbavu asiyejiondoa mbele ya mwenye nguvu mpaka anasagwa kwa kupigwa na kukanyagwa, na hatimaye akiisha vunjiwa mifupa anaanguka ardhini mithili ya mfu. Wayahudi walipata nini kutokana na vita, na ninyi mtapata nini? هٰذَا وَبَعۡدَ الۡمَوۡتِ نَحۡنُ نُخَاصِمُ[10]. Masufii pia walikiri mengi juu ya ukamilifu wa kibinadamu kuwa mtu hufikia mpaka wapi, leo wao pia wamelala. Enyi wenye akili! Nitambueni mimi kwa kazi zangu. Kama zile kazi na ishara hazidhihiriki

---

[9] Yu ni mbora kuliko baadhi ya manabii.

[10] Ni hii tu, na baada ya kifo tutashindana.

kwangu zinazotakiwa kudhihirika kwa waliopata kusaidiwa na Mungu basi ninyi msinikubali. Lakini kama zinadhihirika, basi msijitumbukize katika shimo la maangamio huku mkijua. Acheni dhana mbaya, jizuieni kufikiria vibaya, kwani kwa sababu ya kumvunjia heshima mtakatifu mmoja, mbingu inakuwa nyekundu[11], nanyi hamwoni. Na damu inatiririka kutoka ndani ya macho ya malaika, nanyi hamuioni. Mungu Yupo ndani ya jalali yake, na sehemu zote zatetemeka. Iko wapi akili ile iwezayo kuelewa. Yako wapi macho yale yazitambuayo nyakati. Hukumu moja ikaandikwa mbinguni, je, ninyi mnaikasirikia? Je, mtamwuliza Mola Mwenye heshima kwa nini Umefanya hiyo? Ewe mtu usiyejua! Jizuie, kwani haitakufaa kusimama mbele ya radi.

Ziangatieni dhuluma zenu na yafikirieni maringo yenu kwamba kwanza Mungu Alionyesha ishara na Akampa Atham mauti ya aina mbili. Mosi, yeye alilaumiwa kwa hatia ya kuficha ukweli na kuongopa,

[11] Tanbihi: Mashuhuda yanayotolea na mbingu na ardhi kwa ajili ya kudhihiri Imam mmoja siyo maana yake kuwa Mahdi fulani wa kumwaga damu au Masihi mwanavita atadhihiri. Maneno yote haya ni mawazo ya kutofahamu; bali mimi nimetumwa ili kuwatia haya wakanao, na kuingiza imani ndani ya mioyo kwa miujiza. Mwandishi

lakini hakuweza kujiondolea lawama kwa njia yoyote, si kwa kushtaki wala kwa kula kiapo na wala kwa ithibati nyingine yoyote ile. Ya pili, sawa na ahadi ya Mungu baada ya kung'ang'ania kuficha ukweli akafa haraka. Sasa elezeni kwamba kwa kusadikisha utabiri huu mmepatwa na matatizo gani? Je, Atham hakuendelea kuogopa? Je, hatimaye hakufa? Je, ndani ya utabiri halikuwemo sharti la wazi wazi kwamba kwa kurejea kwenye ukweli kifo kitaahirishwa? Kisha, je miongoni mwenu yupo yeyote anayeweza kula kiapo kuwa kutokana na mambo yanayolingana na akili lawama hii haikuthibitika juu ya Atham kuwa yeye kwa kauli na matendo na kwa udhuru wa kipuuzi alithibitisha kwamba yeye baada ya utabiri lazima alikuwa anaogopa. Na hakuweza kuthibitisha kwamba kwa nini hofu hiyo aliyoikiri mwenyewe inasibishwe, kwa udhuru usio na dalili, kwa nyoka aliyefundishwa n.k., ilhali, kwa kuimarisha dalili hii katika mioyo, njia zote mbili za kula kiapo na kushtaki zilikuwa wazi kwa ajili yake. Sasa elezeni, je, alikula kiapo? Je, alishtaki? Je, alitoa uthibitisho wowote mwingine wa tuhuma zake? Semeni chochote kwa midomo! Toboeni kwamba yeye baada ya kukiri hofu yake na kwa kutumia tu tuhuma na uzushi akaelezea nyoka n.k kuwa msingi wa hofu

yake, akatoa dalili zipi kwa kuthibitisha udhuru huo aliozusha mwenyewe! Enyi wenye chuki, wenye bahati mbaya! Je, ninyi hamtakufa abadani? Je, haitakuja siku ile mtakaposimamishwa mbele ya Mola wa walimwengu? Kama yangekuwa mashtaka yoyote ya kidunia ya aina hiyo na ninyi mngefanywa kuwa wazee wa baraza au waamuzi, bila shaka mngemuona mwongo mtu kama huyo ambaye hakuweza kama Atham kutoa hoja yoyote ya kujitetea, na kwa kuogopa mahakama ya kibinadamu mngeandikisha maelezo ya kweli. Lakini sasa mnafahamu kuwa Mungu yuko mbali nanyi na Hasikii chochote na siku ya hukumu bado iko mbali sana!!!

Semeni kweli, je Atham amekufa akiwa hana lawana? Na hakwenda na lawama yoyote dhidi yake kutoka kwetu? Semeni kwa kuapa, niambieni je, hamkusoma ndani ya matangazo yangu kuwa Atham baada ya kung'ang'ania kuficha haki atakufa haraka? Ndivyo ilivyotokea, na akafa ndani ya miezi saba kuanzia tangazo letu la mwisho lililokuwa kama kukamilisha hoja. Sasa huu ni ukosefu wa imani kiasi gani kwamba watu wenye tabia chafu wa kaumu hii wakawaunga Wakristo mikono na wakaipinga sauti ya kimbingu na wakasadikisha sauti ya kishetani. Lakini hii imekuwa vizuri kuwa

wakatimiza Hadithi ya Mtume wa Mungu s.a.w. Wenye bahati mbaya Mwislamu mpya Sa'dullah na Muhammad Ali Wa'idh mpaka sasa wanalilia kuwa bishara haikutimia. Enyi kundi la mashetani, mpaka lini mtauficha ukweli? Je, kwa juhudi zenu ukweli utaangamia? Piganeni na Mungu kadri mwezavyo kupigana, kisha muone kuwa ushindi ni wa nani, kwani hukumu hutegemea mwisho. Ewe kaumu isiyo na haya! Atham aliogopa kunikabili lakini nyinyi hamkuogopa. Yeye alisagwa na laana lakini hakujitokeza. Yeye aliahidiwa zawadi ya rupia elfu nne. Hakupata ujasiri wa kuja kwetu hata hatua moja mpaka akaingia kaburini. Akachelea kufungua mashtaka pia. Na Wakristo walipomsisitizia, kakataa. Je, mpaka sasa haijathibitika kuwa yeye alijua kuwa mapambano yake ni kinyume cha ukweli, na moyo ukajaa hofu. Hata hivyo, kwa sababu ya kuficha ukweli, Mungu Hakumuacha na sawa na ahadi ya Mungu akafa sawa na matakwa ya ufunuo, na akawafedhehesha Masheikh na Wakristo. Yeye kwa umri hakunizidi sana isipokuwa miaka michache. Ni khulka mbaya ya Sa'dullah Mwislamu mpya kuwa anamwita yeye kuwa mzee mkongwe. Myahudi huyu anataka kwa vyovyote vile bishara ifichike. Hivyo, Enyi wapinzani! kwa kukosa haya kataeni kadri

mnavyotaka, lakini uhakika umebainika na wenye akili wameishafahamu kuwa bishara imetimia, si kwa jiha moja bali imetimia kwa jiha nne.[12]

Atham alipewa faida ya kurejea kwake na hofu ile iliyodhihirika kwake, kama ilivyokuwa sharti katika ufunuo, na ilikuwa ni sehemu moja ya bishara. Na kurejea huko kulipatikana ndani yake mara tu alipoisikia bishara, kwani yeye alikuwa ameritadi Islam na alikuwa na dukuduku siku zote kuhusiana na uungu wa Yesu na alikuwa akitoa maelezo mbalimbali. Na tangu awali alikuwa na dhana njema juu yangu, kwani kwa kukaa katika wilaya hii alikuwa anaelewa vizuri habari zangu za mwanzoni. Haingewezekana kwake kunifikiria kuwa mwongo, ndiyo maana wakati wa kuambiwa bishara akageuka rangi na hali yake ikabadilika. Na niliposema kuwa wewe ndani ya kitabu chako umemwita Mtume[saw] kuwa dajali, hii ndiyo adhabu yake utakayopata,

[12] (1) Jiha moja ni hii kwamba sharti lililokuwa ndani ya ufunuo, kwa sababu ya kulitimiza kifo cha Atham kikaahirishwa. (2) Pili ni kwamba kwa sababu ya kuficha ushahidi Atham alikufa haraka kulingana na ufunuo (3) Tatu ni kwamba kutokana na hila za Wakristo na njama za Masheikh kwa pamoja, utabiri wa *Barahine Ahmadiyya*, uk. 241, ukatimia (4) Bishara ya Mtume[saw] iliyohusu ugomvi baina ya Waislamu na Wakristo nayo pia ikatimia kwa tukio hili. Mwandishi

akatishika na kupigwa na bumbuazi na akaweka mikono yake miwili juu ya masikio yake kana kwamba akawa anatubu wakati huo. Nafikiri watu sabini takriban walikuwa ndani ya mkutano huo wa Wakristo. Ilmuradi, si kwamba akarejea baada ya muda, bali papo hapo akaanza kurejea, na hadi mwisho wa muda, alipitisha siku zake mfano wa wendawazimu.

Sasa uovu mkubwa zaidi kuliko huu utakuwa ni nini kuwa licha ya matukio haya ya waziwazi inasemwa kuwa bishara haikutimia. لَعْنَةُ اللهِ عَلَى الْكَاذِبِيْنَ[13]. Neno la marejeo lililomo ndani ya sharti, lilikuwa tendo la moyo lililoanzia wakati huo huo. Lipo wapi neno la Islam wazi wazi ndani ya sharti? Je mshirikina mmoja wakati wa bishara nzito kama hiyo angeweza kusimama imara. Kila mmoja anatakiwa akumbuke kuwa bishara hii haikuanzia siku hiyo hiyo, bali ndani ya *Barahine Ahmadiyya* habari hii mapema ilitolewa miaka kumi na miwili hapo kabla na pamoja nayo ilikuwa habari ya bishara kuhusu Lekhram. Kama mkisoma ukurasa wa 239 na 240 na 241 wa *Barahine Ahmadiyya*, picha hii nzima itakuja mbale ya macho yenu. Ndani ya maandiko ya zamani na

[13] Laana ya Mungu iwe juu ya wasemao uwongo.

Hadithi za Mtume[saw] kuhusiana na Mahdi wa zama za mwisho ilikuwa imeandikwa kuwa mwanzoni yeye atatambuliwa kuwa mtu asiye dini na kafiri. Na watu watakuwa na bughudha kali sana naye, na watamlaumu na watamuita kwa jina la dajali, asiye na dini na mwongo, na hao wote watakuwa ni Masheikh. Na siku hiyo katika umati huu hatakuwa mtu mbaya zaidi juu ya ardhi kuliko hao masheikh. Basi, kwa muda fulani itaendelea kuwa hivyo, kisha Mungu Atamsaidia kwa ishara za kimbingu, na sauti itatokea kwa ajili yake kutoka mbinguni kuwa huyu ni خَلِيْفَةُ اللهِ الْمَهْدِيُّ[14]. Lakini je, mbingu itaongea kama aongeavyo binadamu? Hapana, bali muradi wake ni kuwa ishara za kuogofya zitadhihiri zitakazofanya nyoyo zitishike. Ndipo Mungu Ataielekeza mioyo kumpenda yeye. Na kukubaliwa kwake kutaenezwa ardhini, hata kwamba hawatakaa watu wanne mahali pamoja wasiomtaja kwa upendo na sifa njema. Hivyo, kurasa hizo za Barahin zinatoa picha ya matukio haya haya yaliyotajwa hapo juu. Kwanza aliniambia kuwa watu watakufikiria kuwa mpotevu, jahili na mtu mwenye mawazo ya kishetani, watakutesa na watasema maneno ya aina aina na watafanya dhihaka. Na tena Akasema kuwa Mimi nitakutosha kwa shari

---

[14] Khalifa wa Mungu aliye Mahdi.

ya wote wanaodhihaki. Na kisha Akasema: قُلْ عِنْدِيْ شَهَادَةٌ مِّنَ اللّٰهِ فَهَلْ اَنْتُمْ مُؤْمِنُوْنَ[15]. Kwa hiyo Ameashiria kuwa katika siku hizo ishara za kimbingu zitadhihiri. Kisha baada yake katika ukrasa wa 241, ameeleza ishara kuhusu Atham na hapo hapo Akatoa habari kwamba kuhusu ishara hii Wakristo na Waislamu wenye sifa za Kiyahudi wataleta ghasia, nao watafanya hila na Mungu naye pia Atafanya hila, na hila, za Mungu hushinda. Kisha baada yake Akanena kuwa baada ya hila hizo Mungu Atadhihirisha ukweli, na utakuwa ushindi mkubwa. Basi, Mungu Akalionyesha tukio la Lekhram kuwa ni ushindi mkubwa. Na haikuwa katika uwezo wa yeyote isipokuwa Mungu kutoa habari ya matokeo ya mapambano kama hayo na kutoa bishara ya ushindi.

Bishara ya pili inamhusu Lekhram ambaye kuhusiana naye kuna ishara ndani ya ufunuo huo huo wa *Barahine Ahmadiyya*. Na ndani ya Baharine Ahmadiyya, baada ya hila za Wakristo, imeandikwa ufunuo huu kuwa اَلْفِتْنَةُ هٰهُنَا فَاصْبِرْ كَمَا صَبَرَ اُولُوا الْعَزْمِ, yaani wao watakapofanya hila, kutatokea fitina kubwa, na nchini kelele zitapigwa kuihami batili, na mkweli atachukuliwa kuwa ni mwongo na watawafahamu waongo kuwa wakweli. Sasa, Enyi wenye macho!

[15] Tafsiri: Sema nina ushahidi kutoka kwa Mungu, je mtaamini.

Msiingie moto wa jahanamu kwa kutilifikisha ukweli kiasi hiki. Angalieni, adhama kiasi gani imo ndani ya bishara hii kuwa miaka kumi na miwili mapema ikaelezwa kwa uwazi kabisa. Na kuhusiana nayo kuna Hadithi ya Mtume[saw] pia iliyosimuliwa kuwa kutakuwa na ugomvi na Wakristo, ndipo sauti itatokea ardhini kuwa wafuasi wa Isa wako juu ya haki na sauti itatokea mbinguni kuwa wafuasi wa Muhammad wako juu ya haki. Sasa semeni kweli kuwa mpaka sasa sauti imekuja au hapana? Kama mtazidi katika shari, basi Yeye Atazidi kuionyesha kudra Yake. Je, yuko anayeweza kumchosha?

Sasa hapa tunaiandika bishara ya Lekhram kinaganaga pamoja na ibara asili za vitabu vile ambavyo ndani yake bishara hii ipo, na tunawaelekeza wasomaji wasome sehemu hizi kwa makini kwa kumcha Mwenyezi Mungu na kisha wafikirie kuwa je, hii ni kazi ya mwanadamu, au ni ya Yule Mungu Ambaye ni Mmiliki wa mbingu na ardhi na Mungu Mwenye nguvu zote. Zingatieni kuwa vitabu ambavyo ibara zake zinaandikwa hapa chini, ibara zote hizi zimeandikwa vivyo hivyo vilivyo. Hazina upungufu wala zaidi ya hata herufi moja, hata kwamba shairi lililoandikwa mwanzoni mwa bishara, linaloanzia na mshororo huu: عجب نور یست در جان محمدﷺ[16] chini ya mkono

[16] Imo nuru ya ajabu rohoni mwa Muhammad[saw].

uliochorwa kuonyesha bishara, huo nao pia umetiwa mahali hapo hapo ili wasomaji wa kijitabu hiki waelewe kikamilifu habari ile iliyofafanuliwa ya mauti ya Lekhram miaka minne kabla ya kufa kwake. Na licha ya hii vitabu hivyo vinaweza kupatikana katika kila mji na kwa miaka mingi vinachapishwa katika Panjab na India. Yeyote atakaye basi aone katika vitabu vya asili.

Hapa kuna jambo muhimu linalostahili kukumbukwa, ambalo ni kiini na kusudio hasa la kitabu chetu hiki, nalo ni hili kuwa bishara hii ilitolewa kwa kudhihirisha shabaha moja kubwa, yaani kuthibitisha jambo hili kwamba dini ya Aria ni batili kabisa na ma-Veda hayakutoka kwa Mwenyezi Mungu, na Seyidna wa Maulana Muhammad Mteule[saw] ni Mtume Mtakatifu wa Mwenyezi Mungu na ni Nabii mtukufu, na Islam ni dini ya kweli kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Na hayo ndiyo yaliyoandikwa mara kwa mara, na kwa kuitimiza shabaha hii dua ziliombwa. Hivyo, bishara hii haipaswi kufikiriwa kuwa ni bishara tu pekee, bali hii ni Hukumu moja ya Kimbingu, kutoka kwa Mwenyezi Mungu, baina ya Mabaniani na Waislamu. Tangu muda fulani, ukali ulikuwa umezidi ndani ya Mabaniani, hususan huyo Lekhram alionekana kana kwamba hakuwa

na itikadi kuwa Mungu pia yupo. Basi, Mungu Aliwaonyesha ishara ing'aayo. Inatakiwa kila mtu achukue somo kwa hiyo. Mtu anayefungua mdomo kuwafedhehesha Manabii watukufu wa Mungu, hawezi kamwe kuwa na mwisho mwema.

Lekhram kwa kifo chake amewapa Waariya fundisho la ibra. Inatakiwa waachane na kufanya shari alizoeneza Dayanand nchini, na waitendee Islam kwa upole na unyofu na upendo wa kweli na heshima. Tokea hapo wanayo hiari. Baadhi ya wapumbavu ambao wakijiita Waislamu walikuwa wameelekea kwenye Waariya, sasa huu ni wakati wao wa kutubu. Wanapaswa kuona kuwa Mungu wa Islam Yu Mshindi kiasi gani? Waaria, wakati wa kutoa bishara hii, waliarifiwa kwa njia ya matangazo yaliyochapishwa kuwa kama dini yenu ni ya kweli na Islam ni batili, basi alama yake ni hii tu kuwa mwokoeni wakili wenu Lekhram kwa athari ya bishara hii, na kadri itakavyowezekana mwombeeni, na kwa maombi muda pia ulikuwa mwingi, lakini watu hao hawakuweza kuibadilisha nia ya Mungu kumwadhibu vikali. Yapasa kufahamu kuwa kisu alichochomwa nacho Lekhram, ndicho kile kile alichoendelea kutumia kwa miaka mingi kwa kumvunjia heshima Seyidna wa Maulana Mtume[saw].

Hivyo ukali ule wa ulimi wake ukachukua sura ya kisu, kikaingia tumboni mwake. Kisu kisipotumukia mbinguni, hakiwezi kamwe kutumika ardhini. Watu huenda wakadhani kwamba Lekhram ameuawa sasa. Lakini mimi nilikuwa nimemfahamu kuwa ameuawa aliponijia malaika mmoja katika sura ya mmwagaji damu na akauliza, "Lekhram yuko wapi"? Basi, habari hii yote mtasoma ndani ya bishara hizo zinazoandikwa kama ifuatavyo.

**Kwanza**, (katika tangazo la tarehe 20 Februari 1886, kumhusu Lekhram, katika ukurasa 4 ipo bishara kiasi hiki tu) kuwa juu ya takdiri kuhusu Lekhram Peshawarii pengine mambo kadha yataandikwa ndani ya kijitabu hiki pamoja na wakati na tarehe. Kama bishara yoyote ya aina hii imsumbue mtu yeyote, basi itamjuzu kuwa kuanzia tarehe 1 Machi 1886 au kuanzia tarehe ile ambapo ndani ya gazeti lolote madhumuni haya kwa mara ya kwanza yachapishwe, aniarifu kwa maandishi yenye saini yake ndani ya wiki mbili barabara ili bishara hiyo ambayo kudhihiri kwake kunamtisha iwekwe kando na isiandikwe ndani ya kijitabu, na kwa kuifikira kuwa itasababisha kuudhi asijulishwe mtu yeyote hiyo wala yeyote asiarifiwe kuhusu wakati wake wa kudhihirika. Na baada ya hapo barua ya Pandit Lekhram ikafika kuwa

mimi ninaruhusu kuwa bishara itolewe kuhusiana na kifo changu lakini inatakiwa kuwekwa muda. Kisha baada ya hapo ufunuo ulioelezwa chini ulifunuliwa.

**Pili:** Ufunuo uliandikwa katika kijitabu *Karaamaatus Sadiqiin*, kilichochapishwa mwezi Safar 1311 Hijria:

وَعَدَنِيْ رَبِّيْ وَاسْتَجَابَ دُعَائِيْ فِيْ رَجُلٍ مُفْسِدٍ عَدُوِّ اللّٰهِ وَرَسُوْلِهِ الْمُسَمّٰى لِيْكهرَام اَلْفِشَاوَرِيَّ وَ اَخْبَرَنِيْ اَنَّهٗ مِنَ الْهَالِكِيْنَ. اِنَّهٗ كَانَ يَسُبُّ نَبِيَّ اللّٰهِ وَيَتَكَلَّمُ فِيْ شَاْنِهٖ بِكَلِمَاتٍ خَبِيْثَةٍ. فَدَعَوْتُ عَلَيْهِ. فَبَشَّرَنِيْ رَبِّيْ بِمَوْتِهٖ فِيْ سِتَّةِ سَنَةٍ اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيَةً لِّلطَّالِبِيْنَ

Yaani, Mwenyezi Mungu Aliniahidi kuhusu adui mmoja wa Mungu na Mtume[saw] anayemtukana Mtume[saw], na anatumia lugha chafu dhidi yake, ambaye jina lake ni Lekhram, na Alisikia dua yangu. Na nilipoomba dua dhidi yake hapo Mungu Akanipa bishara kuwa huyo ataangamia ndani ya miaka sita. Hii ni ishara kwa  wale ambao wanatafuta dini ya kweli.

**Tatu:** Ufunuo huu uliandikwa ndani ya tangazo la 20 Februari 1893 ambao umetiwa ndani ya kitabu cha Ainae Kamaalaate Islam.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

عجب نوریست در جان محمدؐ عجب لعلیست در کان محمدؐ | ز ظلمت ہا دلے آنگہ شود صاف کہ گردد از محبانِ محمدؐ

عجب دارم دل آں ناکساں را کہ رو تابند از خوانِ محمدؐ | ندانم ہیچ نفسے در دو عالم کہ دارد شوکت و شانِ محمدؐ

خدازان سینہ بیزارست صدبار    کہ ہست از کینہ دارانِ محمدؐ
اگر خواہی نجات از مستی نفس    بیا در ذیل مستانِ محمدؐ
اگر خواہی دلیلے عاشقش باش    محمدؐ ہست برہانِ محمدؐ
بگیسوئے رسول اللہ کہ ہستم    نثار روئے تابانِ محمدؐ
بکار دین نترسم از جہانے    کہ دارم رنگ ایمانِ محمدؐ
فدا شد در رہش ہر ذرّۂ من    کہ دیدم حسن پنہانِ محمدؐ
بدیگر دلبرے کارے ندارم    کہ ہستم کشتۂ آنِ محمدؐ
دل زارم بہ پہلویم مجوئید    کہ بستیمش بدامانِ محمدؐ
تو جان ما منور کردی از عشق    فدایت جانم اے جانِ محمدؐ
چہ ہیبت ہا بدادند ایں جواں را    کہ ناید کس بمیدانِ محمدؐ
رہ مولیٰ کہ گم کردند مردم    بجو در آل و اعوانِ محمدؐ
کرامت گرچہ بے نام و نشان ☞

خدا خود سوزد آں کرم دنی را    کہ باشد از عدوّانِ محمدؐ
اگر خواہی کہ حق گوید ثنایت    بشو از دل ثنا خوانِ محمدؐ
سرے دارم فدائے خاک احمدؐ    دلم ہر وقت قربانِ محمدؐ
دریں رہ گر کشندم وربسوزند    نتابم رُو زِ ایوانِ محمدؐ
بسے سہل ست از دنیا بریدن    بیاد حسن و احسانِ محمدؐ
دگر استاد را نامے ندانم    کہ خواندم در دبستانِ محمدؐ
مرا آں گوشۂ چشمے بباید    نخواہم جز گلستانِ محمدؐ
من آن خوش مرغ ازمرغان قدسم    کہ دارد جا بہ بستان محمدؐ
دریغا گر دہم صد جان دریں راہ    نباشد نیز شایان محمدؐ
الا اے دشمن نادان و بے راہ    بترس از تیغِ بُرّانِ محمدؐ
الا اے منکر از شانِ محمدؐ    ہم از نور نمایان محمدؐ
بیا بنگر زِ غلمانِ محمد [17]

# Bishara Moja Kumhusu Lekhram Peshawarii

Ibainike kuwa katika tangazo la tarehe 20 Februari

---

[17] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

Mna nuru ya ajabu katika dhati ya Muhammad[saw], mna yakuti ya ajabu katika mgodi wa madini ya Muhammad[saw].

Moyo unatakasika na giza, unapoingia katika wapenzi wa Muhammad[saw].

Nashangaa kwa mioyo ya hao wajinga waikimbiao meza iliyoandikwa tayari ya Muhammad[saw].

Simjui mtu yeyote katika dunia na akhera, ambaye anayo heshima na adhama kama ya Muhammad[saw].

Mungu anakasirikia sana mtu anayemchukia

1886 ambalo lilitiwa ndani ya kitabu hiki, niliwaita

---

Muhammad[saw].

Mungu Mwenyewe Anamwunguza yule mdudu hakiri aliye miongoni mwa maadui wa Muhammad[saw].

Kama ukitaka kuokolewa katika upotevu wa nafsi, basi uwe miongoni mwa wapenzi wa Muhammad[saw].

Kama ukitaka kusifiwa na Mungu, basi uwe mwenye kumsifu Muhammad[saw] kwa moyo wote.

Kama unataka dalili ya ukweli wake, basi uwe mpenzi wake, kwani Muhammad[saw] mwenyewe ndiye dalili ya Muhammad[saw].

Kichwa changu kimejitolea vumbini pa miguu ya Ahmad[saw], na wakati wote moyo wangu unajitolea mhanga kwa Muhammad[saw].

Naapa kwa uzuri wa Mtume[saw] wa Mungu kwamba najitolea mhanga kwa uso ung'aao wa Muhammad[saw].

Kama nikiuawa katika njia hii au nikichomwa moto, hata hivyo sitaachana na kizingiti cha Muhammad[saw].

Kuihusu kazi ya dini siuogopi hata ulimwengu mzima, kwani ninayo rangi ya imani ya Muhammad[saw].

Ni rahisi sana kutengana na dunia kwa kukumbuka uzuri na hisani ya Muhammad[saw].

Katika njia yake kila chembe yangu yajitolea mhanga, kwani nimeshauona uzuri uliofichika wa Muhammad[saw].

Sitambui jina la mwalimu yeyote, maana nimehitimu katika chuo cha Muhammad[saw].

Indarman Muradabadi na Lekhram Peshawarii kwenye jambo hili kuwa wakitaka, baadhi ya bishara zichapishwe kuhusu takdiri yao. Basi, baada ya tangazo hili Indarman akahepa na baada ya muda mfupi akafariki. Lakini Lekhram kwa ujasiri mkubwa

---

Na sihusiki na mpendwa yeyote, kwani uzuri wa Muhammad[saw] umenipenya kabisa.

Nahitaji mtazamo wake wa upendo, sihitaji kitu isipokuwa bustani ya Muhammad[saw].

Msitafute moyo wangu uliojeruhiwa katika kifua change, kwani nimeuambatanisha kwa dhati ya Muhammad[saw].

Miongoni mwa nyuni watukufu, mimi ndiye nyuni mtukufu ninayekaa katika bustani ya Muhammad[saw].

Umenurisha roho yetu kwa upendo, uhai wangu utolewe mhanga kwako, Ee Muhammad[saw].

Hata kama katika njia hii nijitolee maisha yangu mara mia, haitalingana na shani ya Muhammad[saw].

Shujaa huyo amepewa haiba nyingi iliyoje hata kwamba hakuna yeyote anayojitokeza uwanjani mwa Muhammad[saw].

Ewe adui uliye mjinga na mpotofu! Jihadhari na upanga mkali wa Muhammad[saw].

Njia hii ya Mungu iliyosahauliwa na watu, uitafute katika ali na wasaidizi wa Muhammad[saw].

Jihadhari, Ee mtu ukanaye shani ya Muhammad[saw] na nuru iliyo dhahiri ya Muhammad[saw].

Ingawaje karama imeadimika kabisa, lakini njoo ukaione kwa watumishi wa Muhammad[saw].

akanitumia postikadi kuwa uchapishe tu juu yangu bishara yoyote utakayo, mimi natoa ruhusa. Hivyo, nilipoelekea kwa Mungu kumhusu yeye, basi kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mwenye shani ufunuo huu ukafunuliwa.

عِجْلٌ جَسَدٌ لَّهٗ خُوَارٌ ۔ لَهٗ نَصَبٌ وَّعَذَابٌ

Yaani, huyu ni ndama tu asiye na uhai ambaye kutoka ndani yake sauti ichukizayo inatoka, na kwa sababu ya utovu wake wa adabu na mdomo mchafu, ikabu na huzuni na adhabu ndiyo takdiri yake ambayo lazima ataipata. Na baadaye, leo tarehe 20 Februari 1893, siku ya Jumatatu, nilielekea kwa Mungu ili kujua muda wa adhabu hii, basi Mwenyezi Mungu Akanidhihirishia kuwa kuanzia tarehe ya leo, ambayo ni 20 Februari 1893, hadi muda wa miaka sita, mtu huyu atakumbwa na adhabu kali sana kwa sababu ya mdomo wake mchafu, yaani kwa utovu wa adabu kwa Mtume wa Mungu[saw]. Hivyo, sasa, mimi kwa kuichapisha bishara hii ninawadhihirishia Waislamu na Waaria na Wakristo wote na madhehebu mengine kwamba kama kuanzia tarehe ya leo ndani ya muda wa miaka sita adhabu[18] yoyote haitamteremkia mtu huyo, ambayo iwe zaidi

[18] Sasa Waariya wanapaswa wafanye maombi kwa pamoja kwamba adhabu hiyo imuepuke wakili wao.

ya shida za kawaida na ya kimuujiza na yenye heba ya Kiungu, basi fahamuni kuwa mimi sikutoka kwa Mwenyezi Mungu, wala mimi siongei kwa roho yake. Na kama mimi nikipatikana mwongo katika bishara hii, basi niko tayari kupokea adhabu yoyote, na niko radhi kwamba nikifungwa kamba shingoni mwangu nitundikwe juu ya msalaba wowote ule. Pamoja na ikirari yangu hii, ni wazi pia jambo hili kwamba mtu kuthibitika kuwa mwongo ndani ya bishara yake ni fedheha kubwa kuliko fedheha zote. Zaidi ya haya niandike nini?

Ibainike kuwa mtu huyo amemfanyia Mtume wa Mungu[saw] utovu wa adabu sana hata kwa kuufikiria tu mwili unatetemeka. Vitabu vyake vimejaa kejeli ya ajabu, shutuma na matusi. Ni Mwislamu gani avisomaye vitabu hivyo na moyo wake na ini lake lisipasuke vipande vipande. Pamoja na ujasiri na kebehi zake, mtu huyo ni jahili mtupu, hana habari yoyote ya lugha ya Kiarabu, bali hana hata uwezo wa kuandika lugha ya Kiurdu sanifu pia. Na bishara hii siyo ilitolewa hivi tu, bali mimi nilifanya maombi hasa kwa ajili ya shabaha hii hii, nami nilipata jawabu hili. Na bishara hii ni ishara kwa ajili ya Waislamu pia, laiti wangeuelewa uhakika na mioyo yao ingelainika. Sasa ninamalizia kwa jina la Mungu

Yule Yule Mwenye heshima na utukufu Ambaye kwa jina Lake nilianzia.

وَالْحَمْدُ لِلّٰهِ وَالصَّلٰوةُ وَالسَّلَامُ عَلٰى رَسُوْلِهٖ مُحَمَّدِ الْمُصْطَفٰى اَفْضَلِ الرُّسُلِ وَ
خَيْرِ الْوَرٰى سَيِّدِ كُلِّ مَا فِى الْاَرْضِ وَالسَّمَا ۔[19]

Ni mimi Mirza Ghulam Ahmad kutoka Qadian

Wilaya ya Gurdaspura (20 Februari 1893)

**Nne:** Jibu la shutuma lililoandikwa kwenye jalada la *Baraka za Dua* pamoja na taarifa iliyoandikwa kwenye tanbihi ya ukurasa wa 4 wa jalada

## Mfano wa dua iliyokubaliwa Gazeti Anise Hind, Meerut, na shutuma dhidi ya bishara yetu

Nimepokea toleo la gazeti hili la tarehe 25 Machi 1893, ambamo mna baadhi ya shutuma dhidi ya ile bishara yangu niliyoichapisha kumhusu Lekhram Peshawarii. Nimefahamu kuwa hata baadhi ya magazeti mengine pia yamesumbuliwa na neno hili la haki. Kwa hakika ni jambo la furaha kwangu kwamba kwa njia hii bishara hii inapata kujulikana na kuenea kwa mikono ya wapinzani wenyewe. Basi,

[19] Sifa zote njema ni za Mungu, na baraka na amani ziwe juu ya Mtume wake Muhammad[saw], mteule, mbora wa Mitume wote na mbora wa wanadamu wote , Bwana wetu na Bwana wa wote waliomo ardhini na mbinguni. Mfasiri

mimi kwa wakati huu, katika kuijibu shutuma hiyo, naona inatosha tu kuandika kuwa namna Alivyotaka Mwenyezi Mungu, ndivyo Alivyotenda; mimi simo humo. Naam, suala hili kwamba bishara kama hii haitakuwa na faida, na ndani yake shaka zitabaki, kuhusiana na shutuma hii nafahamu vema kuwa hiyo imeletwa kabla ya wakati wake. Mimi mwenyewe ninakiri jambo hili, na sasa ninakiri tena, kwamba ikiwa, kama wanavyofikiri wapinzani, hatimaye matokeo ya utabiri huo yakawa kwamba huyo akapata homa kidogo au maumivu kidogo au akashikwa na kipindupindu na halafu hali ya asili ya afya ikarejea, basi hiyo haitahesabiwa kuwa ni bishara, na bila shaka hiyo itakuwa ni hila na uadanganyifu. Kwani hakuna yeyote aliyeepukana na maradhi ya aina hii. Sisi sote wakati mwingine tunaumwa. Hivyo, kwa hali hii bila shaka nitakuwa mwenye kustahili kupewa adhabu ile niliyoitaja. Lakini kama bishara ikitimia kwa namna ambavyo ndani yake alama za adhabu ya Mwenyezi Mungu zionekane wazi wazi kabisa, basi hapo mtambue kuwa bishara hiyo imetoka kwa Mwenyezi Mungu.

Hakika yenyewe ni kwamba taadhima na heba ya dhati ya bishara haihitaji kuwekewa siku na nyakati. Kuhusu hiyo inatosha tu kuweka muda maalum wa

zama za kushuka adhabu. Halafu kama kwa hakika bishara idhihiri kwa matisho makubwa, basi yenyewe huivutia mioyo. Na mawazo yote haya na shutuma zote hizi zizalikazo nyoyoni kabla ya wakati wake, hutoweka kabisa kwa njia hii kwamba waadilifu wenye busara wanaachana na rai zao wakitahayari. Mbali na hayo, mimi nami nipo chini ya kanuni ya maumbile. Ikiwa kwa upande wangu msingi wa bishara ni huu tu kwamba mimi nimeitangaza bishara hii kwa njia ya kupayuka tu na kufikiria maradhi kadha kwa njia ya kubahatisha, basi yule mtu ambaye bishara hii inamhusu, yeye naye anaweza pia kufanya hivyo na kutoa bishara kunihusu mimi kwa kutegemea mabahatisho yayo hayo. Bali mimi niko radhi kwamba badala ya miaka sita ambayo ni muhula niliomwekea, yeye aandike miaka kumi kwa ajili yangu. Umri wa Lekhram kwa wakati huu, pengine kwa wingi kabisa ni miaka thelathini, naye ni mtu aliye kijana, kipande cha mtu, mwenye afya bora; na mimi umri wangu kwa wakati huu ni zaidi ya miaka hamsini, tena ni dhaifu na mwenye kusumbuliwa daima na magonjwa na ninaugua maradhi mbalimbali; lakini hata hivyo katika mashindano haya itajulikana yenyewe kwamba kauli ipi imetoka kwa mwanadamu na kauli ipi imetoka

kwa Mwenyezi Mungu.

Na kauli ya mpinzani kwamba hizi si zama za bishara za aina hii, ni sentensi ya kawaida tu ambayo watu wengi huitamka vinywani mwao. Nielewavyo mimi, hizi ndiyo zama za kukubali kweli zilizo imara na kamilifu ambazo pengine mfano wake haupatikani katika zama zilizopita. Naam, katika zama hizi udanganyifu na hila yoyote haiwezi kufichika; lakini hili ni jambo la furaha zaidi kwa wakweli kwani, yule mtu ajuaye kutofautisha baina ya udanganyifu na ukweli, huyo ndiye anayeuheshimu ukweli kwa moyo na kwa furaha huukimbilia kuukubali. Na kweli huwa na mvuto ule ambao wenyewe unajikubalisha. Ni dhahiri kwamba zama hizi zinaendelea kuyakubali mamia ya mambo mapya ambayo mababu wa watu hawakuyakubali. Kama zama hizi hazina kiu ya ukweli, kwa nini basi mapinduzi makubwa yameanza ndani yake? Bila shaka zama hizi ni rafiki wa kweli zilizo halisi, sio adui. Na kusema kwamba zama zina akili na wakati wa watu wasiojua mengi umeshapita, hii kwa maneno mengine ni sawa sawa na kuzikejeli zama hizi, kana kwamba zama hizi ni mbaya kiasi hiki kuwa baada ya kuukuta ukweli kuwa ni ukweli kwa hakika, hata hivyo haziukubali. Lakini mimi kamwe sitakubali kwamba ndivyo ilivyo, kwani mimi

naona kuwa wengi wanaonijia na kufaidika nami ni wale wale wenye elimu ya kisasa ambao baadhi yao wamefika hadi shahada ya B.A. na M.A. Na pia naona kwamba kundi hili la watu wenye elimu ya kisasa wanaendelea kupokea ukweli kwa shauku sana. Na si hiyo tu, bali kundi moja la Waislamu wapya, wenye wazazi wa Kizungu na Kiasia walioelimika waishio katika eneo la Madras wamejiunga katika Jumuiya yetu, nao wana yakini juu ya kweli zote.

Sasa nafikiri nimeshayaandika mambo yote yale yatoshayo kufahamu kwa mtu amchaye Mungu. Waaria wanayo hiari ya kuyafasiri madhumuni yangu haya wapendavyo. Siijali hata kidogo, kwa sababu nafahamu kwamba kwa wakati huu ni mamoja tu kuisifu bishara hii au kuilaumu. Ikiwa hii imetoka kwa Mwenyezi Mungu, nami nafahamu vizuri kwamba imetoka Kwake tu, basi lazima itatimia kwa ishara ya kutisha na itatetemesha mioyo. Na kama haikutoka Kwake, basi itadhihirika dhila yangu. Na kama wakati huo nitatoa udhuru mbovu, basi huo utasababisha dhila yangu maradufu. Yule Dhati asiye na mwanzo, Mtukufu na Mtakatifu, Ambaye Anayo madaraka yote mikononi Mwake, Hampi katu mwongo heshima. Si sawa kabisa kwamba mimi ninao uadui binafsi na Lekhram. Mimi binafsi sina

uadui na mtu yeyote yule; bali mtu huyu aliufanyia ukweli uadui na akamfehehesha yule Mkamilifu na Mtakatifu aliyekuwa chemchemi ya kweli zote. Ndiyo sababu Mwenyezi Mungu Akataka kudhihirisha duniani heshima ya mpendwa wake.

Na amani iwe juu ya yule aufuataye mwongozo.

## Habari nyingine kumhusu Lekhram Peshawarii.

(Iliyoandikwa katika maelezo ya pembeni kwenye ukurasa wa nje wa *Baraka za Dua*)

Leo, tarehe 2 April 1893, sambamba na tarehe 14 mwezi wa Ramadhani 1310 Hijiria, majira ya asubuhi, niliona nikiwa katika hali baina ya kulala na kuamka kwamba nimekaa ndani ya nyumba moja yenye wasaa, na marafiki wachache pia wapo pamoja nami, mara mtu mmoja aliye pande la mtu, mwenye sura ya kutisha, kana kwamba ameghadhibika vikali sana sana, akaja na kusimama mbele yangu. Nikainua macho na kumtazama, nikafahamu kuwa yeye ni mtu wa umbo na tabia ngeni, kana kwamba si mwanadamu bali ni miongoni mwa Malaika wakali wenye nguvu; na nyoyo zilitishika kwa hofu yake. Nilipomtazama tu akaniuliza, "Lekhramu yuko wapi"? Na akataja jina la mtu mwingine kuwa

yu wapi? Ndipo nikafahamu wakati huo kuwa huyo ameamrishwa kuwaadhibu Lekhramu na yule mtu mwingine, lakini sikumfahamu yule mtu wa pili ni nani. Naam, nakumbuka kwa yakini kabisa kuwa yule mtu wa pili alikuwa miongoni mwa wale watu wachache ambao kuwahusu hao nimekwisha tangaza. Na hiyo ilikuwa siku ya Jumapili, majira ya saa kumi za usiku. Basi, Alhamdulillahi kwa hayo.

## Mawazo ya Waariya kuhusu Lekhram baada ya kuuawa kwake

Katika gazeti la Akhbare Aam lililochapishwa Jumatano, tarehe 10 Machi 1897, imeandikwa kuniashiria mimi kuwa: "Bishara ya kufa kuhusu Mkristo mmoja bwana Kamishna Mdogo ilikuwa imetangazwa tangu muda wa mwaka mmoja, na ikaenezwa sana ndani ya magazeti, na kama — Mungu Apishe mbali — katika siku hizo bwana Kamishna Mdogo angepatwa na tukio hilo (yaani tukio la mauaji) ambalo ikambidi bwana Lekhram kupata upatilizi wake hapo hali ingekuwa tofauti." Sasa kila mmoja anaweza kuelewa kuwa maelezo ya bwana Mhariri yana maana gani. Anamaanisha iyo hiyo kwamba kama bwana Atham angeuawa, basi kama afikirivyo bwana Mhariri, serikali mara moja

ingeelekea kwa yule mtoaji wa bishara na upelelezi ungefanyika ambao sasa haupo. Huenda bwana Mhariri akawa na nia nzuri lakini ni masikitiko kwani fikara hii ndiyo ya juu juu tu na ufahamu huu ndio kinyume cha ukweli. Imefahamika hii pia kwa maneno ya Bwana Mhariri kuwa bishara inayomhusu Atham haikutimia. Lakini sisi kwa muhtasari tunakumbusha kuwa bishara ile ilitimia kwa uwazi sana. Bw. Atham tangu zamani alikuwa ananitembelea, yeye safari moja aliniomba akisisitiza kwa mdomo na kwa maandishi kwamba 'kama kuna bishara yoyote kunihusu mimi nayo itokee kuwa kweli, basi mimi nitajirekebisha kiasi fulani', basi Mungu Akadhihirisha bishara hii inayomhusu yeye kuwa katika kipindi cha miezi kumi na mitano ataanguka katika Jahanamu sharti asipoelekea kwenye haki katika kipindi hiki. Basi, kwa vile ndani ya bishara mlikuwa na sharti na Bw. Atham kwa hofu akazingatia sharti hilo, hivyo ikalazimu yeye afaidike na sharti lile, maana haiyumkiniki kuwa mtu atekeleze sharti la Mungu kisha asinufaike nalo. Hivyo basi, kwa athari ya sharti hilo, kifo chake kikaahirishwa kwa muda fulani. Kama ukisema inathibitikaje kuwa moyoni yeye akarejea kwenye Uislamu au hofu ya bishara ya Kiislamu ilimshinda,

basi jibu lake ni hili kuwa Mungu Akaniarifu kuwa Atham amefaidika na sharti, na Tumeahirisha kifo chake kwa muda fulani, hapo mimi nikamwita Bwana Atham kuwa aje kuapa kwa zawadi ya rupia elfu nne kwamba kama ndani kwa ndani hakujirejesha kwenye Uislamu au heba ya Kiislamu haikumtawala moyoni mwake, basi akija uwanjani ale kiapo. Au kama si kiapo, basi kwa kupeleka kesi mahakamani athibitishe sababu za hofu anayokiri. Lakini yeye hakula kiapo wala hakushtaki mahakamani. Hata hivyo, yeye alikiri kwa uwazi kuwa mimi ndani ya muda wa bishara nilikuwa naogopa, lakini si kwa heba ya Kiislamu, bali kwa nyoka aliyefundishwa na kwa mashambulio n.k. Na kwa kuwa yeye hakuweza kuificha hofu, ndiyo maana akatoa visingizio hivyo na hakutoa ithibati yoyote, na kwa sababu hii hii aliitwa aje kuapa ili kama yu mkweli ale kiapo, lakini hata juu ya ahadi ya kupewa rupia elfu nne yeye hakuapa, wala hakushtaki kuzithibitisha tuhuma zake mpaka akaingia kaburini. Ndani ya ufunuo wangu ilikuwemo hii pia kuwa Atham kama hatatoa ushahidi wa kweli na hatakula kiapo, hata hivyo baada ya kung'ang'nia atakufa haraka. Na ndivyo ilivyotokea, na Bw. Atham akafariki ndani ya miezi saba baada ya tangazo langu la mwisho. Na ajabu

zaidi ni hii kuwa miaka kumi na miwili kabla ya kutokea tukio hili habari zake zilikuwemo ndani ya *Barahine Ahmadiyya*, angalieni uk. 241 wa *Barahine Ahmadiyya*. Basi, kuhusu bishara hii wazi na ing'aayo kudhania kuwa haikutimia ni kinyume kabisa na uadilifu. Je, kulikuwa hamna sharti lolote ndani ya bishara hii juu ya Bwana Atham? Na kama lilikuwepo, je Bwana Atham kwa kauli zake na vitendo vyake hakuthibitisha kutimia kwa sharti hilo? Je, Bwana Atham hakuenda kaburini pamoja na lawama yangu hii kuwa yeye baada ya kukiri hofu, hakuthibtisha kuwa hofu ile ilitokana na nyoka aliyefundishwa na mashambulio, sio kwa sababu ya heba ya bishara ya Kiislamu? Yeye daima alikuwa anafanya mahojiano, lakini baada ya utabiri akanyamaa hadi akafariki katika hali ya kunyamaza tu.

Hivyo basi, bishara ilitimia kwa njia tatu. Ya kwanza, kulingana na sharti lake kwamba kwa kutekeleza sharti Atham akafaidishwa. Pili, kulingana na ile ahadi, iliyokuwa ahadi ya mauti baada ya kuficha. Tatu, kwa mujibu wa ufunuo huu wa *Barahine Ahmadiyya* uliotolewa miaka kumi na miwili kabla ya tukio hili. Sasa fikirieni kuwa kama bishara yoyote itakuwa wazi zaidi ya hii, itakuwa vipi? Kama mtu akiacha ukweli apige domo, sisi

hatuwezi kuuziba mdomo wake. Lakini maneno ya ufunuo yanayomhusu Atham ni wazi kiasi hiki kwamba mtafuta ukweli hana budi kuyamini. Na ufunuo wa *Barahine Ahmadiyya* — unaomhusu Atham ambao miaka kumi na miwili kabla ya bishara hii uliishaenezwa katika karibu uliwmengu wote wa Kiislamu — wale watakaoutafakari wataanguka katika sijida kwamba Mungu Yu Mjuzi wa ghaibu kiasi gani Ambaye Akaatoa habari za matukio na magomvi yote yajayo.

Kwa kuwa siku hizi watu wengi wa dunia hawana imani juu ya Dhati Aliyetukuka, ndiyo maana mawazo yao badala ya kuelekea kwenye dhana njema, yanaelekea kwenye dhana mbaya. Hili ni kosa kabisa kusema kuwa serikali ilifanya uzembe kuhusu kesi ya Lekhram, na katika kesi ya Atham, kama angeuawa, haingefanya ulegevu. Sisi tunasema kuwa bila shaka hii ni faradhi ya serikali kwamba iwatazame Waislamu na Mabaniani kuwa sawa kama macho mawili, isiwapendelee wowote, kama inavyofanya kwa hakika serikali hii yenye uadilifu. Lakini mimi nauliza kuwa je, kuna serikali yoyote inayoweza kupigana na Mungu? Bila shaka serikali ina wajibu wa kumkamata mtu yeyote mwovu, muuaji, na kumnyonga, na kumtanabahisha kwa

adhabu kali zaidi na zaidi ili wengine wapate somo, na amani idumu nchini. Kama Atham angeuawa, bila shaka angenyongwa yule ambaye angekuwa muuaji wa Atham. Vivyo hivyo itakapothibitika kuwa fulani ndiye muuaji wa Lekhram, naye atatiwa nguvuni. Basi vivyo hivyo yeye pia atapata adhabu ya kunyongwa. Serikali ina kosa gani kwa hili? Ina ulegevu gani? Waariya wanataka kumkamatisha muuaji gani na kwa ithibati ipi ambaye Serikali inasita kumkamata? Lakini Serikali haiwezi kuingilia kati bishara za Mungu. Kadri serikali itakavyozingatia jambo hili ndivyo itakavyozikuta bishara hizo kuwa ni za kimbingu, za kweli na safi. Kwa vyovyote serikali hii ni ya watu wa Kitbau na haimkatai Mungu Anayezijua siri zilizofichikana na Anaweza kutoa habari za zama zijazo kwa njia hii kana kwamba zama zile zipo sasa. Je ni muhali kwa Mungu kuelezea muda wa miaka sita na kubainisha siku ya pili baada ya idi na kuelezea sura ya kifo? Kama ni muhali kwa Mungu, basi binadamu anawezaje kutoa mwenyewe bishara pamoja na masharti hayo? Je, kutoa habari sahihi za aina hii muda mrefu mapema ndiyo kazi ya mwanadamu? Kama ndiyo kazi yake, basi leteni mfano wake wowote katika dunia. Serikali inapaswa kuona fahari kuwa ndani ya nchi hii na katika zama

za ufalme wake Mungu Anajenga mahusiano na baadhi ya watumishi wake, ambayo yameandikwa ndani ya vitabu kama visa na hadithi. Ni rehema hii juu ya nchi hii kuwa mbingu imeikaribia ardhi, mfano wake hakuna katika nchi zingine.

Hakuna budi kueleza hii pia kuwa barua kadha zimewasilia kutoka sehemu mbalimbali za Panjab, ambamo humo zimeelezwa harara na njama zisizofaa za baadhi ya Waaria. Barua hizo zipo kwangu, zimehifadhiwa, na baadhi ya Waariya wa eneo hili nimewaonyesha barua hizo. Basi, barua moja iliyotoka Gujranwala, ya mheshimiwa chifu mmoja imenifikia ambayo madhumuni yake ni haya: "Hapa kwa siku mbili kulikuwa na kikao cha maombolezo ya Lekhram, na kwa mwenye kumkamata muuaji imetangazwa zawadi ya rupia elfu moja, na rupia mia mbili kwa atoaye habari zake. Na habari za nje zimesikika kuwa kamati moja ya siri imeundwa kwa kukuua[20] na wanakamati wa kamati hii ni wenjeji wa miji ya karibu (kama vile Lahore, Amristar, Batala na hususan Gujranwala). Na imependekezwa kuwa baada ya kuchanga rupia elfu ishirini wamtume mtu mmoja mwenye shari, mwenye tamaa, kwa ajili ya

[20] Habari hii hii imeiandika pia kwa ufupi ndani ya gazeti la 'Pesa Akhbar'. Mwandishi.

kazi hii, ili aue atakapopata nafasi.[21] Basi, mchango wa rupia elfu mbili tayari umekwishapatikana, zilizobaki zitachukuliwa kutoka miji na vijiji vingine". Kisha baada ya hapo mwandishi anaandika, "Ingawa wewe uko chini ya himaya ya Mhafidhi wa Kweli, hata hivyo ni lazima kutumia njia za dhihiri pia, nami naonelea katika wakati kama huu ni lazima kujiepusha pia na Waislamu wenye shari, maana wao ni wenye tamaa na tabia mbovu. Si ajabu kuwa wao baada ya kufanya bai'ati kidhahiri wajasiri kutenda kitendo hiki kwa kupewa tamaa na Waaria". Anaandika tena mwandishi, "Mimi nimepata kujua hii pia kuwa viongozi wa kundi la waliotoa shauri la kuua ni baadhi ya mawakili na baadhi ya maafisa wa serikali na baadhi ya Waariya matajiri na wakubwa wa mji huu wa Lahore. Kadri zilivyonifikia habari, nimezielezea, na Mungu Anajua zaidi". Na barua za

21 Ufunuo wa *Barahine Ahmadiyya* yaani يَا عِيْسٰى اِنِّيْ مُتَوَفِّيْكَ ulioenezwa miaka kumi na saba iliyopita, wakati huu maana yake imefahamika vizuri, yaani ufunuo huu ulikuwa ni kama kumfariji Hadhrat Isa[as] wakati huo ambapo Wayahudi walikuwa wanafanya juhudi ya kumsulubisha, na hapa badala ya Wayahudi, Wahindu ndio wanaofanya juhudi hizo, na maana ya ufunuo ni hii kuwa mimi nitakuepusha na vifo duni vya aina hii vilivolaaniwa. Tazameni kuwa tukio hili limeliwekaje jina la Isa kwangu. Mwandishi.

kuisadikisha zimefika kutoka Pind Dadan Khan na sehemu nyinginezo na maudhui yao ni karibu haya haya. Barua zote hizo zimehifadhiwa. Na harara ile ililyodhihirishwa na gazeti la baadhi ya Waariya, inadhihirisha kuwa wakati wa jazba ya aina hii, mawazo ya namna hii yanawezekana. Basi, ndani ya toleo maalum la gazeti '*Panjab Samachaar*' la Lahore imeandikwa mistari hii michache kunihusu mimi: "Bwana mmoja labda ndani ya kitabu chake Mau'udi Masihi alitoa bishara hii pia kuwa Pandit Lekhram ndani ya miaka sita, siku ya idi, atakufa katika hali ya kutia uchungu. Bishara hii ilikuwa inakaribia kutimia muda wake, maana aghalabu mwaka 1897 ulikuwa ni wa sita, na tarehe 5 Machi 1897 ilikuwa idi ya mwisho ya mwaka wa sita. Alikuwa akitangaza wazi wazi kwa njia ya maandishi na ulimi kuwa atamuua Pandit na zaidi ni kwamba Pandit katika muda huu na katika siku fulani atakufa katika hali ya uchungu mkali. Je, mpinzani huyu wa dini ya Kiaaria na mwandishi maalum wa vitabu vichache (yaani mimi) hana uhusiano wowote na njama hii? Mwandishi huyu wa gazeti hili na kadhalika wengine nao wamefahamu kutokana na bishara hii kuwa hii ilikuwa ni njama iliyotangazwa kama bishara, kama aandikavyo ndani ya ukurasa wa pili wa gazeti hilo

kuwa, "Mauaji haya ni matokeo ya njama madhubuti iliyofikriwa na kupangwa na watu wengi tangu muda mrefu." Sisi tunakubali na kukiri jambo hili kuwa ndani ya maelezo ya bishara hii iliandikwa mara kwa mara kwa kufahamishwa na Mungu kwamba itatimia kwa njia ya kutisha, na kwamba mauti ya Lekhram hayatasababishwa na ugonjwa wowote, bali Mungu Atamfanya yule atakayekuwa amepandwa na mori kumtawala yeye. Lakini siku ya idi iliyoandikwa ndani ya gazeti la '*Panjab Samachaar*' la 10 Machi 1897, kwa kutaja ufunuo ni kosa lake. Maneno ya ufunuo ni haya سَتَعْرِفُ يَوْمَ الْعِيْدِ وَالْعِيْدُ اَقْرَبُ , yaani utaitambua siku ya ishara hiyo ikiwa kama idi, na idi itakuwa karibu sana na siku ya ishara hiyo. Mungu Aliitoa habari hii kuwa siku ya idi itakuwa imeungana na siku ya kuuliwa kwake. Na ndivyo ilivyotokea. Idi ilikuwa siku ya Ijumaa, na Jumamosi iliyokuwa tarehe pili ya *Shawal* 1314 Hijria, Lekhram akauawa.

Basi, iliyomaanisha bishara yote ni kuwa hili litakuwa ni tukio moja la kutisha litakalotokea ndani ya muda wa miaka sita, na siku hiyo itakuwa imeungana na siku ya idi, yaani itakuwa tarehe pili ya Shawal.

Sasa fikirini je, hii ni kazi ya mwanadamu kuwa

tarehe ilitajwa, siku ilitajwa, sababu ya kifo ilielezwa, na ilielezwa kuwa tukio hili litatokea kwa sura ya kutisha. Picha yake ilielezwa ndani ya madhumuni ya Baraka za Dua. Je, hii inaweza kuwa kazi ya mla njama kwamba miaka sita mapema atoe habari pamoja na alama zilizo wazi kama hizo, na habari ile itimie. Torati inatoa ushahidi kuwa bishara ya nabii mwongo kamwe haitimii. Mungu Husimama kukabiliana naye ili dunia isiangamie, kama vile siku hizo hizo Lekhram pia kwa ujanja wa kidunia akatoa tangazo kunihusu mimi kuwa 'wewe utakufa hadi miaka mitatu'. Basi, kwa nini yeye hakuweza kupangiana na muuaji yeyote ili habari aliyotoa ingetimia!

Jambo jingine lapasa kuzingatia kuwa dhana hii mbaya kuwa labda mfuasi wake yeyote ndiye aliyemuua, ni mawazo ya kishetani. Kila mwenye busara anaweza kuelewa kuwa wafuasi huwa na uhusiano nyeti na mwongozi, na msingi wa itikadi huwa juu ya ucha Mungu na utakaso na wema. Watu wanaokuwa wafuasi wa mtu yeyote, hao huwa wafuasi kwa nia hii hii kwamba wanafahamu kuwa mtu huyu ni mja wa Mungu, hana udanganyifu wala ufisadi moyoni mwake. Basi kama yu mtu mwovu na mlaaniwa kiasi hiki kwamba mwenyewe anazua

bishara ya uongo kuhusiana na kifo cha mtu fulani na muda wake unapokaribia kutimia anamnyenyekea mfuasi wake fulani kuwa sasa nilindie heshima yangu na jitilie kamba shingoni na ukanifanye nionekane mkweli. Sasa nawauliza waadilifu kuwa baada ya kuiangalia mienendo hii ya mtu mchafu na mlaaniwa kama huyo na baada ya kusikia njama hii ya kishetani, je, mfuasi yeyote anaweza kuwa na imani naye? Je, hatamfikiria mwongozi huyo kuwa ni mwovu, mlaaniwa, fasiki na mwenye dhambi? Na je, yeye hatamwambia, "Ewe mwovu! mwenye kutuharibia imani yetu, je hiyo ilikuwa hakika ya asili ya bishara zako? Je, matakwa yako ni kuwa uongo uuseme wewe na kamba itiwe shingoni mwa mwingine na kwa njia hii bishara yako itimie?

Kadri manabii na wajumbe walivyoopita duniani au mitume na *muhaddathina* watakaokuwepo baadaye, mtu yeyote asingeliweza wala hataweza kuingia katika wafuasi wao ilhali anawafahamu kuwa wadanganyifu na wafanyao hila. Uhusiano baina ya uongozi na ufuasi ni nyeti sana. Kwa dhana mbaya kidogo sana tofauti hutokea ndani yake. Safari moja, niliona ndani ya Jamaat ya wafuasi wangu kuwa miongoni mwao baadhi yao wakawa na shaka kuhusiana nami kwa sababu tu kwamba

ndani ya sala wakati wa kukaa kwa *Attahiyyatu* sikuwa nimeinua mguu wangu wa kuume kutokana na udhuru wa maradhi ambayo hawakuyajua, kwa jambo hili tu watu wawili wakaanza kupiga domo na kuingia katika mashaka kuwa hii ni kinyume cha suna. Safari moja, mimi nilishika kikombe cha chai kwa mkono wa kushoto kwa sababu mfupa wa mkono wangu wa kulia ulikuwa umevunjika na ni dhaifu. Kwa sababu hii tu baadhi yao wakaatibu kuwa ni kinyume cha suna. Na daima hufanyika hivi kuwa baadhi ya wafuasi wapya wanaingia katika majaribio kwa mambo madogo madogo kwa sababu ya ukosefu wa kufahamu. Na huanza kuatibu hata mambo madogo madogo ya binafsi, kama vile walivyokuwa wakimsumbua nabii Musa pia vivi hivi. Kwani Islam ni dini ambayo wafuasi wake hupima kauli na matendo ya kila mtu kwa kipimo cha unyofu na ucha Mungu. Na kama wakiipata kuwa kinyume chake basi mara moja hujitenga naye.

Basi, inatakiwa kufikiri kuwa inawezekanaje kwamba watu wa aina hii waweze kuwa waaminifu kwa huyu mtu muovu ambaye kazi zake zote zimejaa udanganyifu na njama. Na yuataka kuwaamuru watu wamwage damu bila haki ili asifedheheke na bishara yake itimie. Hakuna mtu anayetaka kuipoteza imani

yake makusudi. Tena hata kama mfuasi yeyote ashiriki katika njama za aina hii, basi iweje jambo hili lifichikane kwa wafuasi wote. Na ni dhahiri kuwa ndani ya Jamaat yetu wapo waheshimiwa wakubwa wakubwa, wenye shahada za B.A., M.A., na ma-Afisa wa Tarafa, watoza ushuru, maafisa wasaidizi wa ziada serikalini, matajiri wakubwa wakubwa na kundi la maulamaa na wataalamu. Je hili lote ni kundi la wahuni na waovu? Sisi tunasema kwa kupaza sauti kuwa Jumuiya yetu ni ya watu wenye mienendo mizuri, wastaarabu na watawa. Yuko wapi mfuasi wetu mchafu mlaaniwa adaiye kuwa sisi tulimtuma kwa kumwua Lekhram? Sisi tunamchukulia kiongozi kama huyo pamoja na mfuasi wa aina hii kuwa mbaya zaidi kuliko mbwa. Na ni mwenye maisha machafu sana yule ambaye anazua bishara mwenyewe kisha kwa mkono wake na kwa udanganyifu na ulaghai wake anajaribu kuzitimizia na kuwaomba wengine wazitimize.

Hivyo, ni masikitiko kuwa katika gazeti la Panjab Samachaar toleo la 10 Machi, tuhuma ya njama tuliyosingiziwa ni kubatilisha namna gani ukweli! Mimi namwuliza mwenye gazeti kuwa kati yenu pia wametokea Ma-Autar wakubwa wakubwa kama vile Ram Chandar na Raja Krishna. Je, mnaweza

kuwadhania kwamba mmoja wao alitoa bishara kisha kwa ajili ya kulinda heshima zake akafanya hila kwamba akamuomba mfusai wake kwa kumbembeleza kuwa yeye aitimize bishara hiyo kwa juhudi zake na kulinda heshima yangu, na hata hivyo wafuasi hao wakawadhania kuwa watu wema? Naam, hii inawezekana kuwa majambazi wachache waunguane na jambazi mmoja mwovu  na wafanye kazi za aina hii kwa siri. Lakini katika Jumuiya hii ya wafuasi wangu inayoambatana na madai ya Mahdi Mau'udi na Masihi Mau'udi pia kwa nguvu sana, matendo haya maovu hayawezi kulingana. Kila mfuasi kwa kuliona dai hilo kubwa sana anataka kuuona mfano wa ucha Mungu wa hali ya juu kabisa. Sasa yawezekanaje kuwa dai liwe hili kuwa mimi ndiye Isa wa zama na atake kutimiza bishara za uongo hivi kuwa ajinyenyekeza mbele ya wafuasi wake kuwa nimekosea, nisitirini, nendeni mkafe na kwa vyovyote kutimiza bishara yangu. Je dhalili kama huyo anaweza kuwa mwongozi wa Jumuiya takatifu? Iko wapi dhamiri yenu takatifu, Enyi Waaria waungwana? Na iko wapi busara yenu ya asili, Enyi wenye busara wa Waaria! Sisi sheria yetu ni kuwa wahurumieni wanadamu wote. Kama mtu mmoja anamwona jirani yake Baniani kuwa nyumba

yake imepata moto, naye hainuki ili asaidie kuuzima moto, basi mimi ninasema kweli kabisa kuwa huyo hatokani nami. Kama mtu mmoja miongoni mwa wafuasi wangu anaona kuwa mtu fulani anataka kumwua Mkristo mmoja na yeye hafanyi juhudi ya kumsaidia asiuawe, basi mimi ninawaambia sawa kabisa kuwa huyo hayumo miongoni mwetu. Islam siyo mdhamini wa waovu wa kaumu hii. Baadhi yao huwaua watoto kwa tamaa za rupia moja tu. Matukio ya aina hii mara nyingi hufanywa kwa ajili ya tamaa za nafsi. Na hususan Jamaat yetu ambao wamekusanyika kwangu kujifunza wema na unyoofu, hao hawaji kwangu ili wajifunze kwangu kazi za ujambazi na kuiangamiza imani yao. Mimi nasema kwa kuapa na ninasema kweli kuwa mimi sina uadui na kaumu yoyote ile. Naam, kadri inavyowezekana ninataka kurekebisha itikadi zao. Na kama mtu akinitukana basi mashtaka yetu yako kwa Mungu na siyo kwa mahakama nyingine yoyote ile. Na pamoja na hayo yote ni jukumu letu kuwahurumia wanadamu. Sisi wakati huu tuitulize vipi na kwa maneno yepi mioyo ya Waaria kuwa hila za maovu siyo desturi yetu. Tunahuzunika kwa kifo cha mwanadamu mmoja, na tunafurahia pia kutimia bishara moja ya Mungu. Kwa nini twafurahi? Kwa wema wa mataifa tu. Laiti

wangefikiri na wangefahamu kuwa kutoa habari miaka mingi mapema waziwazi wa daraja la juu kabisa si kazi ya mwanadamu. Wakati huu hali ya moyo wetu ni wa ajabu. Kuna uchungu vilevile na raha pia. Uchungu ni kwa sababu kama Lekhram angejirudi hata kama sio sana bali kwa uchache angeachana na lugha chafu, hapo ninaapa kwa Mwenyezi Mungu kuwa ningemuombea dua, nami nilikuwa natumai kuwa yeye hata kama angekatwa vipande vipande pia, angehuika. Mungu Yule ninayemjua, hakuna jambo lisilowezekana kwake. Na furaha ni ya jambo hili kuwa bishara ilitimia kwa uwazi sana. Imetia mwanga tena kwenye bishara ya Atham pia. Laiti watu sasa wafikiri na wafahamu, na bughudha na chuki baina ya mataifa iondoke kwani maisha ya uadui na uhasama ni karibu na kifo.

Na kama bado shaka ya mwenye kushuku haiwezi kuondoka, na ananichukulia mimi kuwa mshiriki katika njama ya mauaji haya kama ilivyoelezwa na magazeti ya Kibaniani, basi mimi ninatoa ushauri mwema utakaotoa hukumu juu ya kisa chote hiki, nao ndio huu kuwa mtu wa aina hii ale kiapo mbele yangu kwa maneno haya: "Mimi kwa yakini ninajua kuwa mtu huyu alishiriki katika njama za mauaji, au mauaji yamefanywa kwa amri yake. Na kama hii

siyo sahihi, basi Ewe Mungu Mweza katika mwaka mmoja nishushie adhabu ile ambayo iwe ni adhabu ya kutisha, lakini isiwe kwa mkono wa mtu wala isiweze kufikiriwa kuwa imetokana na njama zozote za kibinadamu. Basi, kama mtu huyo katika kipindi cha mwaka mzima atasalimika kutokana na maombi yangu dhidi yake, hapo mimi nitakuwa mwenye hatia, nami nitastahiki ile adhabu anayostahili kupewa muuaji. Sasa kama yupo Mwaria yeyote mshupavu mwenye moyo wa kishujaa ambaye kwa njia hii aiondolee dunia shaka hizi basi na ashike njia hii. Njia hii ni rahisi na ni ya kuamua ukweli. Labda kwa njia hii Masheikh wapinzani wetu pia watafaidika. Nimeandika haya kwa moyo wa kweli, lakini ikukmbukwe kuwa mwenye kufanya majaribu haya aje mwenyewe Qadian na nauli yake itakuwa juu yangu. Maandishi ya pande zote mbili yatachapishwa. Mungu Asipomhilikisha kwa adhabu isiyokuwa kwa mikono ya binadamu, basi nitathibitika kuwa mwongo. Na dunia nzima iwe shahidi kuwa katika hali hii mimi nitastahili adhabu ile ile anayostahili kupewa mwenye hatia ya mauaji. Mimi siwezi kuondoka hapa kwenda sehemu nyingine, mshindani anatakiwa aje mwenyewe. Lakini mshindani anatakiwa awe mwenye moyo

wa kishujaa sana, barobaro na madhubuti. Tangu sasa itakuwa ni kukosa haya kuwa mtu anitilie shaka chafu za aina hii kwa ghaibu. Mimi nimekwisha weka njia ya maamuzi. Kama baadaye nikigeuka, basi laana ya Mungu iwe juu yangu, na kama mpinzani yeyote asipoachana na tuhuma na asipotafuta uhakika kwa njia hii ya kuamulia, basi laana iwe juu yake. Enyi watu wenye haraka, kama mdhanivyo, mimi sina uadui na kaumu yoyote. Ninayo huruma kwa wanadamu wote, na kiasi cha nguvu niliyonayo mwilini mwangu, nashughulikia kufanya huruma hiyo. Na kama ninavyohurumia kaumu zote ndivyo ninavyoishukuru serikali ya Uingereza na kuitakia heri kwa moyo wa kweli, na najitenga kabisa na ufisadi kwa moyo wote.

Kuna jambo moja linalotakiwa kukumbukwa kuwa bishara iliyotolewa kumhusu Pandit Lekhram, bishara hiyo ilielezwa miaka kumi na saba iliyopita, kama ulivyo ufunuo huu ndani ya uk 241 wa *Barahine Ahmadiyya:*

لَنْ تَرْضٰى عَنْكَ الْيَهُوْدُ وَلَا النَّصَارٰى ۔ وَخَرَقُوْا لَهٗ بَنِيْنَ وَبَنَاتٍ بِغَيْرِ عِلْمٍ ۔ قُلْ
هُوَ اللّٰهُ اَحَدٌ اَللّٰهُ الصَّمَدُ لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُوْلَدْ وَلَمْ يَكُنْ لَّهٗ كُفُوًا اَحَدٌ ۔ وَيَمْكُرُوْنَ وَ

يَمْكُرُ اللّٰهُ وَاللّٰهُ خَيْرُ الْمَاكِرِيْنَ ۔ اَلْفِتْنَةُ[22] هٰهُنَا فَاصْبِرْ كَمَا صَبَرَ اُولُوا الْعَزْمِ ۔ قُلْ

---

[22] Ndani ya *Barahine Ahmadiyya* zimetajwa fitina tatu. Mosi, fitina kubwa ya Mapadri wa Kikristo ambao kwa udanganyifu walileta vurumai duniani kote kuwa bishara kuhusu Atham imetokea kuwa uongo, na wakawaunganisha Masheikh wenye sifa za Kiyahudi na Waislamu wenye tabia yao pamoja nao. Tazameni uk. 241. Fitina ya pili yenye daraja la pili ni fitina ya Maulawii Muhammad Husain Batalawii, ambayo kuhusiana nayo imeandikwa katika ukurasa 510 wa Barahin:

وَاِذْ يَمْكُرُ بِكَ الَّذِيْ كَفَرَ اَوْقِدْ لِيْ يَا هَامَانُ لَعَلِّيْ اَطَّلِعُ اِلٰى اِلٰهِ مُوْسٰى ۔ وَاِنِّيْ لَاَظُنُّهٗ
مِنَ الْكَاذِبِيْنَ ۔ تَبَّتْ يَدَا اَبِيْ لَهَبٍ وَّ تَبَّ ۔ مَا كَانَ لَهٗ اَنْ يَّدْخُلَ فِيْهَا اِلَّا خَائِفًا ۔
وَمَا اَصَابَكَ فَمِنَ اللّٰهِ ۔ اَلْفِتْنَةُ هٰهُنَا فَاصْبِرْ كَمَا صَبَرَ اُولُوا الْعَزْمِ ۔ اَلَا اِنَّهَا فِتْنَةٌ
مِّنَ اللّٰهِ لِيُحِبَّ حُبًّا جَمًّا ۔ حُبًّا مِّنَ اللّٰهِ الْعَزِيْزِ الْاَكْرَمِ عَطَاءً غَيْرَ مَجْذُوْذٍ

Yaani, zikumbuke zama zile atakapokufanyia hila mkataaji mmoja, na atamwambia rafiki yake Hamana kwamba washa moto wa fitina, mimi nataka nimchungulie Mungu wa Musa, nami namdhani kuwa yu mwongo. Mikono yote miwili ya Abu Lahab imeangamia na yeye mwenyewe pia ameangamia, haikumpase kujiingilia kati habari za kukufurisha na kukadhibisha, isipokuwa kwa kuogopa. Angeyauliza mambo aliyokuwa hayaelewi. Na lolote litakalokufikia ni kutoka kwa Mungu. Hapa patakuwa na fitina moja, basi wewe wapaswa kufanya subira kama walivyosubiri Manabii wenye imara. Kumbuka kuwa majaribio hayo yatatoka kwa Mungu ili Akupende sana sana — upendo wa Mungu Ambaye ni Allah Mwenye nguvu Mwenye heshima, ni kipawa kisichokatizwa. Hivi sasa nimeelewa kuwa ndani ya ufunuo 'Hamana' muradi wake ni Nadhir Husain Muhaddith wa Delhi. Maana, Muhammad Husain alipeleka ombi kwake kabla ya wote, na akasema اَوْقِدْ لِيْ يَا هَامَانُ , maana yake ni hii kuwa weka msingi wa kukufurisha ili wengine wafuate. Kwayo inathibitika kuwa mwisho

wa Nadhir Husain umeangamia kama akifa bila kutubu. Na yumkini muradi wa Abu Lahab pia ni Nadhir Husain tu, na mwisho wa Muhammad Husain uwe sawa na aya hii

اٰمَنْتُ اَنَّهٗ لَآ اِلٰهَ اِلَّا الَّذِیْٓ اٰمَنَتْ بِهٖ بَنُوْٓا اِسْرَآءِیْلَ

[Yuunus, 10:91]

Kwani baadhi ya ruya zangu zinayatilia nguvu maelezo haya. Basi, kwa fadhili za Allah, si ajabu kuwa baada ya kushuhudia misaada ya kufululiza hatimaye apate kutubu, na Hamana ahilikike. Fitina ya tatu iliyoko kwenye daraja la tatu ni fitina ya kifo cha Lekhram. Yaani dhana mbaya za Waaria na juhudi zao za siri za kudhuru kama zilivyotajwa nia zao za kuniua ndani ya gazeti la *Pesa Akhbar*. Na ndani ya *Barahine Ahmadiyya*, ukurasa wa 557, kuhusu fitina hii pamoja na ishara inayoambatana nayo kuna ufunuo huu:

میں اپنی چمکار دکھلاؤں گا اپنی قدرت نمائی سے تجھ کو اٹھاؤں گا۔ دنیا میں ایک نذیر آیا پر دنیا نے اس کو قبول نہ کیا۔ لیکن خدا اسے قبول کرے گا اور بڑے زور آور حملوں سے اس کی سچائی ظاہر کر دے گا۔

اَلْفِتْنَةُ هٰهُنَا فَاصْبِرْ كَمَا صَبَرَ اُولُوا الْعَزْمِ۔ فَلَمَّا تَجَلّٰى رَبُّهٗ لِلْجَبَلِ جَعَلَهٗ دَكًّا

[Tafsiri: Mimi nitaonyesha mng'ao wangu, Nitakunyanyua kwa kudhihirisha kudra yangu. Mwonyaji mmoja alikuja duniani lakini dunia haikumkubali, lakini Mungu Atamkubali, na kwa mashambulizi makali Atadhihirisha ukweli wake. Mwenezi.]

Yaani, kutakuwa na fitina moja hapa, basi fanya subira. Na Mungu Atakapojidhihirisha juu ya mlima wa matatizo, Atausaga tikitiki. Huu ni ufunuo wa *Barahine Ahmadiyya*. Lakini wakati wa kuandika maneno haya pia nilipata ufunuo mmoja nao ni huu:

سَلامت بَر تو اے مَردِ سَلامَت

[Tafsiri: Amani iwe juu yako, Ewe mtu wa amani. Mwenezi.]

نَصَرَ اللّٰہِ قَرِیْبٌ ۔ یَاْتِیْکَ مِنْ کُلِّ فَجٍّ عَمِیْقٍ ۔ یَاْتُوْنَ مِنْ کُلِّ فَجٍّ عَمِیْقٍ ۔ یَنْصُرُکَ اللّٰہُ مِنْ عِنْدِہٖ ۔ یَنْصُرُکَ رِجَالٌ نُوْحِیْ اِلَیْھِمْ مِنَ السَّمَاءِ ۔ لَا مُبَدِّلَ لِکَلِمَاتِ اللّٰہِ ۔ اِنَّا فَتَحْنَا لَکَ فَتْحًا مُبِیْنًا ۔

Yaani, Mapadri na Waislamu wenye sifa za Kiyahudi hawatakuridhia. Na hao wamemfanyia Mungu wana na mabinti. Waambie kuwa Mungu ndiye Yule Aliye Mmoja na Asiyehitaji, hana mwana wala si baba wa yeyote wala hakuna anayefanana naye. Na watu hawa watafanya hila. (Hii inaashiria kutokea kwa bishara kumhusu Atham.) Na Mungu pia Atafanya hila kwamba Atawapa muhula kidogo ili wafurahie mawazo yao ya uongo. Na kisha Akasema kuwa wakati huo fitina moja itazushwa na Mapadri na Waislamu wenye sifa za Kiyahudi. Basi, subiri kama walivyosubiri Manabii wenye imara. Na umwombe Mungu Adhihirishe ukweli wako, yaani omba dua kuwa udanganyifu waliofanya Mapadri na Waislamu wenye sifa za Kiyahudi kuwadanganya watu, udanganyifu huo uondoke. Na kisha Akasema, usikate tamaa na rehema ya Mungu, kwani rehema ya Mungu itakuja haraka baada ya kupita siku hizi za majaribio. Msaada wa Mungu utakuja kutoka katika kila upande. Watu watakufikia kutoka sehemu za mbali. Kwa kuonyesha ishara, Mungu Atakupatia msaada kutoka kwake, yaani Ataonesha ishara

ya moja kwa moja, na pia watasaidia wale ambao Sisi wenyewe Tutawateremshia wahyi nyoyoni mwao kutoka mbinguni. Yaani baadhi ya ishara Tutazidhihirisha kupitia njia nyingine. Ndiyo maana kuwa baadhi ya bishara zitadhihirika moja kwa moja, na kwa kudhihirika baadhi yake watu watakuwa njia ambao Tutawatilia mwelekeo nyoyoni mwao. Maneno ya Mungu kamwe hayatashindwa kutimia, wala hakuna yeyote anayeweza kuyazuia. Baada ya hila za Mapadri Tutakupatia ushindi ulio dhahiri kabisa.

Ndani ya ufunuo huu Mwenyezi Mungu kwa maneno ya wazi Amesema kuwa kwanza Mapadri na Waislamu wenye sifa za Kiyahudi wataufícha ukweli wa bishara moja kwa njia ya hila ili ukweli wako uendelee kufichikana na usidhihirike. Kisha baadaye itakuwa hivi kuwa Sisi Tutanuia kuwa ukweli wako udhihirike, na uhakika wa bishara zako ubainike. Hapo sisi tutadhihirisha ishara za aina mbili. Moja, zile ishara ambazo ndani yake kutakuwa hamna mkono wa binadamu, kama vile ilidhihirishwa mapema sana kuwa makala hii itazishinda makala zote ndani ya Mkutano wa kidini. Na hautakuwa mkono wa binadamu katika kutimiza bishara hii. Na ndivyo ilivyotokea. Bali juhudi za kiupinzani zilifanyika,

na kila mmoja alikuwa akitaka kuwa makala yake ishinde. Hatimaye, kulingana na bishara makala yangu ikashinda. Pili, ndani ya funuo za *Barahine Ahmadiyya* mlikuwa na ahadi kuwa Tutadhihirisha ishara zile ambazo ndani yake mtakuwa na mkono wa binadamu. Basi, sawasawa na hiyo, bishara kumhusu Lekhram ilitimia, maana ishara hii ilidhihiri kupitia njia fulani, na mtu alimwua Lekhram. Basi, ni dhahiri kuwa kuhusu bishara hii Mwenyezi Mungu Akamtilia moyoni wa mtu fulani ili amwue, na Akampa fursa kwa kila jiha ili atimize kazi yake.[23] Hivyo basi, Mwenyezi Mungu kabla ya kuelezea habari za ushindi mkubwa kwa kudhihirisha bishara, Alipotaja sentensi mbili, ya kwanza يَنْصُرُكَ اللّٰهُ مِنْ عِنْدِهٖ — Mungu Atakusaidia kutoka kwake Mwenyewe — na ya pili يَنْصُرُكَ رِجَالٌ نُوْحِيْ اِلَيْهِمْ مِنَ السَّمَآءِ۔ — Watakusaidia wale Tutakaowafunulia kutoka mbinguni — sababu

[23] Imeandikwa ndani ya magazeti ya *Pesa Akhbar* na *Safiir Government* kuwa Lekhram alikuwa na mahusiano yasiyo halali na mwanamke fulani, yaani yeye aliuawa na jamaa fulani wa mwanamke huyo. Mauti ya fedheha kiasi gani haya. Kama hiyo inaitwa kifo cha kuwa 'shahidi', basi yapasa kusema kuwa yeye amekwisha kuwa 'shahidi' kwa 'kisu' cha jicho la mwanamke, hatimaye kisu hicho hicho kwa sura ya kutisha kilimchoma. Kama sababu ya kuuawa ni hii, basi huu ndio uthibitisho imara wa maisha yake 'matakatifu' ya Lekhram. Mwandishi.

ya kupambanua huku ni kuwa Mwenyezi Mungu Amesema haya kwa kuwaaibisha mapadre kuwa kama ninyi mlitaka kuificha ishara yetu moja, haidhuru, badala yake Sisi Tutadhihirisha ishara mbili. Ishara moja itakayotokana na mkono Wetu moja kwa moja, na ya pili itafanywa kwa mikono ya watu Tutakaowatilia mioyoni mwao kufanya vile, ndipo ushindi mkubwa utakuwepo. Sasa, hebu tazameni kwa uadilifu na angalieni kwa imani kuwa ishara hizi mbili, yaani ishara ya mkutano wa dini na ishara ya kifo cha Lekhram zimedhihirika miaka kumi na saba baada ya kuchapishwa kwa Baraahiine Ahmadiyya, je hii inaweza kuwa ni uwezo wa mwanadamu?

Hii pia ni dhahiri kuwa kabla ya mkutano wa dini matangazo yenye ufunuo yaliyochapishwa ndani yake ilikuwa imeandikwa wazi wazi kuwa Mungu Amenihabarisha kuwa makala haya yatayashinda makala mengine yote, na ndivyo ilivyokuwa. Tazameni magazeti ya *Civil Military Gazette*, *Observer*, *Mukhbir Deccan*, *Pesa Akhbar, Sirajul Akhbar*, *Mushiir Hind*, *Waziir Hind Sialkot*, *Saadiqul Akhbar* Bahawalpur. Hivyo hiki kilikuwa ni kitendo moja kwa moja cha Mwenyezi Mungu kuwa kinyume cha matakwa ya kila moyo Akawafanya wakiri kwamba makala haya yameshinda. Lakini katika

ishara ya pili, mwuaji akatiliwa moyoni mwake hamu ya kuua. Na kwa njia hii ya kuwaonyesha mahuluku wa Mungu ishara zote mbili, ya moja kwa moja na ya kupitia kwa watu, Akaivunjilia mbali mara moja hila ya Mapadri, Masheikh wa Kiislamu na Mabaniani. Na haikuyumkinika kuachana kwao na shari zao pasipo Mungu kudhihirisha ishara za wazi wazi kama hizi, ndiko Anakoashiria ndani ya ukurasa wa 506 wa *Barahine Ahmadiyya* na Anasema kuwa:

لَمۡ يَكُنِ الَّذِيۡنَ كَفَرُوۡا مِنۡ اَهۡلِ الۡكِتَابِ وَالۡمُشۡرِكِيۡنَ مُنۡفَكِّيۡنَ حَتّٰى تَاۡتِيَهُمُ الۡبَيِّنَةُ وَكَانَ كَيۡدُهُمۡ عَظِيۡمًا

Yaani, haingewezekana kwa Wakristo na wapinzani walio Waislamu na Mabaniani kwamba wangeacha kukataa kama wasingepata ishara ya wazi wazi. Na hila yao ilikuwa kubwa sana. Kisha baada ya hapo ndani ya ukurasa huo huo Akasema kuwa kama Mungu Asingefanya hivyo, machafuko yangetapakaa duniani. Hii inaashiria kwenye jambo hili kuwa mapadre waliwatilia watu shaka kuhusu bishara ya Atham kwa kuificha. Sasa kama bishara iliyomhusu Lekhram ambaye kebehi zake zilithibitisha kuwa yeye si mwenye kurejea, ingebaki fiche hivi hivi tu, basi ukweli wote ungepotea kabisa na mawazo ya watu wasiojua yangechafuka sana na majahili wangekaribia kumkana hata Mungu.

Hivyo, Mmiliki wa mbingu na ardhi Alitaka kuwa Lekhram awe fidia ya dhihirisho la ukweli, na kwa kudhihirisha ukweli wa dini ya kweli awe dhabihu. Hivyo, ikawa vile Alivyotaka Mungu. Huruma ya mtu mmoja kuuawa ipo tu, lakini jambo hili ni la kutoa gizani mioyo mingi kwamba baada ya ishara ya mkutano wa dini, Mungu Ameonyesha ishara hii yenye shani adhimu. Yapasa kila roho isujudie Dhati Yule Ambaye Akimfisha mtu mmoja Akaweka msingi wa kuwafufua maelfu ya wafu. Kisha ufunuo huu unaashiria kwenye bishara hii hii iliyomo ndani ya ukurasa 522 wa *Barahine Ahmadiyya* kuwa:

بخرام کہ وقت تو نزدیک رسید و پائے محمدیاں بر منار محکم تر افتاد۔[24]

پاک محمد مصطفیٰ نبیوں کا سردار۔[25]

رب الافواج اس طرف توجہ کرے گا۔اس نشان کا مدعا یہ ہے
کہ قرآن شریف خدا کی کتاب اور میرے منہ کی باتیں ہیں۔[26]

Basi, ishara yenye shani adhimu iliyoahidiwa ndani ya ufunuo huu ndiyo tu ambayo sawa nayo Neno la Islam limeshinda kuafikiana na ufunuo huu. Na katika

---

[24] Tembea kwa furaha kwani wakati wako umekurubia, na mguu wa wafuasi wa Muhammad umeshaimarika juu ya mnara mrefu sana.

[25] Muhammad Mtukufu Mteule[saw], kiongozi wa manabii.

[26] Mola wa majeshi Ataelekea upande huu. Shabaha ya ishara hii ni kuhakikisha kuwa Kurani Tukufu ni kitabu cha Mungu na ni maneno yatokayo kinywani Mwangu.

ukurasa 557 wa *Barahine Ahmadiyya* ishara hii hii imeelezwa ambayo sentensi yake ya kwanza ni 'Mimi Nitaonyesha mng'ao wangu'. Yaani, Nitadhihirisha ishara moja ya kijalali. Na ndani ya kitabu cha *Surma Chashime Aria* mna kashfi moja ya tangu miaka kumi na mmoja iliyopita ambayo muhtasari wake ni kuwa Mungu Ameonyesha ishara moja ya damu. Damu hiyo ikadondokea kwenye nguo, ambayo ipo mpaka sasa. Damu hiyo ilikuwa ni nini? Ilikuwa ni damu hiyo hiyo ya Lekhram. Mwinamieni Mungu, kwani Yu Mkuu, Hamtegemei yeyote!!!

Baadhi ya watu wa gazeti la Aria walistaajabu kuwa bishara iliyotolewa kuhusu Lekhram, muda wake ulielezwa, siku ilielezwa, njia ya kifo ilielezwa, mambo haya yanawezekanaje bila msingi wa njama kubwa. Basi, toleo maalum la gazeti la *Samachaar* Lahore la 10 Machi 1897 na toleo maalum la *Anise Hind* Meerut la 10 Machi 1897 yalitema sumu sana. Mhariri wa Anise Hind, ndani ya ukurasa wa 13 wa toleo lake, aliandika pia, "Tulipata wasiwasi pale pale alipotabiri Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian kuhusu kifo chake, waila je Bwana huyu alikuwa na elimu ya ghaibu?" Sasa ibainike kuwa hao mabwana wote wenyewe wanataka iamuliwe kuwa je Mungu Alimpa mtu huyu elimu ya ghaibu? Na je inawezekana kwa

Mungu kufanya hivi? Basi, wakati huu tunaandika kwa mfano baadhi ya bishara nyingine ili baada ya kutazama mifano hii, macho ya Waariya yafumbuke, nayo ni hii:

**Mosi**: Bishara ya kifo cha Ahmad Beg Hoshiarpuri ambaye kumhusu yeye iliandikwa kuwa yeye atakufa ndani ya muda wa miaka mitatu, na ni lazima kwamba kabla hajafa aione misiba mingine pia. Hivyo, baada ya tangazo hili yeye akauona msiba wa kifo cha mwanaye, kisha tukio la ghafla la kufariki kwa dada yake mpenzi lilitokea mbele ya macho yake, na baada ya hapo ndani ya muda wa miaka mitatu yeye mwenyewe akafariki huko Hoshiarpur.[27]

[27] Bishara hii ilikuwa na sehemu mbili. Moja ilimhusu Ahmad Beg, na ya pili ilimhusu mkwewe. Na ndani ya baadhi ya funuo za bishara zilizotangazwa hapo kabla mlikuwa na sharti hili kuwa kwa wakati wa kuhofu na kutubu kifo kitaahirishwa. Hivyo, ni masikitiko kuwa Ahmad Beg hakupata bahati ya kufaidika na sharti hili, kwani wakati huo, kwa bahati yake mbaya, yeye na jamaa zake wote waliichukulia bishara hii kuwa ni hila na udanganyifu wa kibinadamu, na wakaanza kufanya dhihaka na mzaha. Na wao daima walikuwa wakifanya dhihaka na mzaha mpaka wakati wa bishara ukawadia na Ahmad Beg akaaga dunia kwa shambulio la taifodi kwa siku moja mbili tu. Ndipo macho yao yakafumbuka na wakapatwa na wasiwasi juu ya mkwe pia, na wanawake wakatishika, wakashughulikia toba na sala na saumu. Na kwa hofu mioyo yao ikatetemeka. Hivyo, ilikuwa lazima kuwa

Sasa semeni kuwa kuhusu kifo chake nilifanya njama kwa kuungana na nani? Je kuungana na maradhi ya taifodi?

**Bishara ya pili** ilihusu msiba wa Sheikh Mihrali tajiri wa Hoshiarpur aliyetuhumiwa kwa mauaji. Sheikh huyo yupo hai katika Hoshiarpur. Mwulizeni kuwa kabla ya dalili za kesi hii kudhihiri, mimi baada ya kupata habari toka kwa Mungu wangu, nilimwarifu au hapana?

**Bishara ya tatu** kumhusu Jaji Sardar Muhammad Hayat Khan ilitolewa wakati Sardar huyo alipotuhumiwa kinyume cha haki. Sasa yapasa iulizwe kuwa bishara yoyote ilitolewa kumhusu bwana huyo kuuondolewa tuhuma kabla ya wakati au imebuniwa sasa. Nami nakumbuka kuwa bishara hii imeelezwa pia ndani ya *Barahine Ahmadiyya*.

**Bishara ya nne** kumhusu Seyid Ahmad Khan K.C.S.I. ilifanywa ndani ya tangazo la tarehe 1 Februari 1886 baada ya kupata ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwamba karibu atapatwa na msiba

---

wakati wa hofu ya daraja hili Mwenyezi Mungu Angetenda sawa na sharti lake. Basi, ni wapumbavu sana na waongo na wadhalimu wanaosema kuwa bishara iliyomhusu mkwe haikutimia. Bali ilitimia kwa uwazi kulingana na hali iliyoko sasa. Na sehemu ya pili inasubiriwa. Mwandishi.

mkubwa. Sasa inatakiwa Sayid Ahmad Khan aulizwe kuwa je baada ya bishara hii alipata msiba mkubwa wa aina hiyo au la, ambao usiwe huzuni ya kawaida bali liwe ni jambo ambalo litatetemesha maisha.

**Bishara ya tano** niliitoa kuhusu kuzaliwa kwa mwanangu Mahmud kwamba sasa atazaliwa, naye atapewa jina Mahmud. Na kwa ajili ya kuitangaza bishara hii vipeperushi vyenye karatasi za kijani vilichapishwa ambavyo vipo mpaka sasa na viligawanywa kwa maelfu ya watu. Basi, mtoto huyu akazaliwa ndani ya muda wa bishara, na hivi sasa yumo ndani ya mwaka wa tisa.[28]

**Bishara ya sita** ilifanywa kumhusu Sharif ambaye ni mwanangu wa tatu, na ilitangazwa sana kabla ya

---

[28] Baadhi ya majahili, kwa sababu ya ujahili tu wanaeleza shaka kuwa pale lilipotolewa tangazo la mtoto wa kiume, kwa nini mtoto wa kike kazaliwa. Lakini hao wanajua vizuri kuwa katika lawama hii wanafanya hiana tupu, kama wao ni wakweli, basi watuonyeshe kuwa katika tangazo la kwanza iliandikwa kuwa katika mimba ya kwanza tu mvulana atazaliwa moja kwa moja. Na kama muda haukuelezwa, kwa kuzaliwa katika tangazo hili, je Mwenyezi Mungu Hakuwa na hiari ya kutimiza ahadi yake wakati Alipotaka. Naam, ndani ya Tangazo la Kijani, kwa maneno yaliyo wazi kabisa, kulikuwa na ahadi ya kuzaliwa mvulana bila kuchelewa. Basi, Mahmud kazaliwa. Yenye shani kubwa iliyoje bishara hii! Kama ipo hofu ya Mungu, fikirieni kwa moyo uliotakasika. Mwandishi.

wakati katika kijitabu Nuurulhaq. Basi sawasawa nayo mtoto wa kiume akazaliwa, ambaye sasa kwa fadhili ya Mungu atakamilisha miaka miwili katika siku chache.

**Bishara ya saba** iliyomo katika tangazo la mwaka 1886 ilimuhusu Dilip Singh kwamba atashindwa kuelekea Panjab, na mamia ya Mabaniani na Waislamu walielezwa bishara hii katika mikutano ya hadhara.

**Bishara ya nane** ilihusu matokeo ya Mkutano wa Dini kuwa ndani yake makala yangu itazishinda makala zote. Na vipeperushi hivyo vikatawanywa kwa maelfu ya Mabaniani na Waislamu mjini Lahore na maeneo mengine kabla ya wakati. Sasa ulizeni gazeti la *Civil Military*, pia ulizeni *Observer, Mushire Hind, Wazire Hind na Pesa Akhbar na Sadiqul Akhbar*, *Sirajul Akhbar*, na someni *Mukhbire Deccan* kwa makini ili mjue kwamba ufunuo wa Mungu ulidhihirisha kwa nguvu kubwa kiasi gani ukweli wake.

**Bishara ya tisa**[29] ilihusikana na kesi ya jinai ya

[29] Tanbihi: Kuuawa kwa Pandit Lekhram kwa njia hii kunatoa funzo kwa Waaria, nalo ni hili kuwa wasijaribu kumwinginza Mwislamu yeyote mpya katika dini ya Kibaniani. Kama mtu anataka kusilimu, basi wamwache asilimu. Mwishoni

mkazi mmoja wa Qadian, Bashimbar Das. Yaani Bashimbar Das alikuwa amefungwa jela mwaka mmoja, na nduguye, jina lake Sharampat, ambaye ni Mwariya mwenye jazba aliniomba kwa unyenyekevu kumwombea na pia akaniuliza matokeo yake yatakuwaje.[30] Mimi nikafanya maombi na katika kashfi

---

wameshamwona yule aliyejiunga na Ubaniani matokeo yake yakawa nini. Pili, ndani ya tukio hili kuna funzo hili pia kwamba wasitamani tena kumtafuta Lekhram wa pili, yaani mfano wake katika mdomo mchafu. Lakini kama kwa hakika jambo lile ni sahihi lililoandikwa katika gazeti la *Pesa Akhbar* na *Safir,* yaani sababu ya kuuawa kwake ni uasherati tu, na tendo hili ni la baba au mume wa mwanamke mwenye ghera, sawa na rai za wengi kulingana na kauli ya *Pesa Akhbar*, basi yapasa kumtafuta mhubiri mwenye mieneno mizuri. Kama kwa mujibu wa kauli ya *Pesa Akhbar* habari iliyoenea zaidi ndiyo hii kuwa sababu ya tukio la mauaji ni uhusiano usio halali, basi ni la ajabu kwa nini habari hii haitiwi maanani na kufanyiwa uchunguzi, na kwa nini taarifa hazichukuliwi za Mabaniani hawa waliotamka maneno hayo. Si muhali kwamba hakika yenyewe ndiyo sawa na methali hii, "Kikulacho ki nguoni mwako." Mwandishi.

[30] Tanbihi: Baadhi ya watu miongoni mwa Wakristo wanatoa lawama kuwa ingawa bishara kumhusu Lekhram ilitimia, lakini baada ya kufa kwake Mabaniani hawakumtazama kwa mtazamo wa dhila. Udhuru wa aina hii kutokea mdomo wa Mkristo ni jambo la kusikitisha sana. Sasa waadilifu waeleze kwamba wakati tulipoweka kutimia kwa bishara kuwa ni kigezo cha ukweli wa Islam, na Mungu kwa kumuua Lekhram Akawapa Waislamu ushindi juu ya Mabaniani, basi, katika hali hii si Lekhram tu

nikaona nimekwenda katika ofisi ile ilimokuwemo faili ya kifungo chake. Nikaifungua ile faili na kukata neno 'mwaka' na mahali pake nikaandika 'miezi sita'. Kisha kwa njia ya ufunuo nikaambiwa kuwa faili itarudi kutoka mahakama kuu na badala ya mwaka itabakia miezi sita, lakini hataachiliwa huru.[31] Kwa

---

bali dhehebu zima hili limepungukiwa heshima kidini. Kama ni heshima ya maiti, basi je ni jambo la heshima kupasuliwa maiti kwa mkono wa daktari? Na hali ya heshima ya mwenendo ni hii kwamba katika *Pesa Akhbar* la 13 Machi 1897 imeandikwa,"Habari inayojulikana sana ya kuuawa kwa huyu mtu ni kuwa huyu alikuwa na uhusiano usio halali na mwanamke fulani na hiyo ndiyo inayosemwa kwa jumla na kuaminiwa." Mwisho. Hivyo, utakuwa na mfano gani mkubwa wa dhila kuliko huu kwamba kafa pia na sababu yake ni uasherati, sawa na wanamji wengi. Mwandishi.

[31] Tanbihi: Ishara moja kwa wenye busara ni hii kwamba Sheikh Najfi alikuwa ameahidi kuonyesha ishara katika dakika arobaini, na mimi katika muda wa siku arobaini kuanzia tarehe 1 Februari 1897. Tazameni maelezo ya pembeni ya tangazo la 1 Februari 1897 ukurasa wa 3 amabayo ibara yake ni hii: Katika muda huo, yaani katika siku arobaini, ishara ilidhihiri kwangu, lakini toka kwake, yaani kwa sheikh Najfi haikudhihirika chochote, basi hiyo ndiyo dalili ya ukweli wangu na uwongo wake. Hivyo, kuanzia tarehe 1 Februari 1897 hadi siku thelathini na tano kupita, yaani ndani ya muda wa siku arobaini, ishara ya mauti ya Pandit Lekhram ikatokea. Bwana Najfi aeleze hii kuwa kuanzia 1 Februari 1897 hadi leo dakika ngapi zimekwisha pita. La kusikitisha ni kuwa Najfi hata hakuonyesha kuanguka kutoka mnara wowote. Kama ndiyo kujigamba na kujisifu tu, basi sheikh Najdi ni afadhali

hivyo nikamwelezea *Sharampat* Mwaria, aliye hai mpaka sasa, habari hizi zote za kashfi kwa uwazi kabisa. Na nilipomwambia na mambo yakatokea vivyo hivyo, yeye akaniandikia, "U mja mwema wa Mungu, kwa hiyo Akakudhihirishia mambo ya ghaibu". Kisha nikachapisha ufunuo na kashfi nzima katika *Barahine Ahmadiyya*. Mtu huyu Sharampat ni Mwariya adui mkali ambaye, nifikirivyo mini, hata hamjali Mungu akiihami dini ya Aria. Lakini hata hivyo, Mungu Alimfanya yeye kuwa shahidi wangu. Kama mimi nimeongopa hata sawa na chembe katika habari hii, basi yeye kwa kula kiapo achapishe tangazo moja lenye maudhui haya kuwa, "Mimi kwa kula kiapo cha Permeshar ninasema kuwa habari hiyo ni uongo mtupu; na kama si uongo, basi adhabu kali inishukie katika muda wa mwaka mmoja."[32] Basi, kama adhabu isiyo ya kawaida haimshukii ambayo hata kwamba watu wasema kuwa hii ni adhabu ya Mungu, basi mnihilikishe kwa

kuliko ma-Najfi mia.

[32] Chochote kilichoelezwa kuhusu habari ya Sharampat, hakuna kupiga chuku ndani yake hata chembe. Mimi nikiapa kwa jina la Mwenyezi Mungu nasema kuwa hii ni kweli na sahihi kabisa. Hivyo, mtu yeyote akinituhumu kwa kuongeza maneno na kutia chumvi, yeye anafanya dhuluma, na dawa ya dhuluma ni ile ile niliyoishaandika. Mwandishi.

njia yoyote mnayotaka. Ndani yake kuna sharti hili kutoka kwangu kuwa adhabu hiyo isipitie binadamu bali iwe moja kwa moja adhabu ya kimbingu.

Hii inawezekana akatae tu ili kuihami kaumu yake, au bila ya kiapo alichoambiwa kula atoe tangazo pia, kwani sijaona hofu ya Mungu ndani ya kaumu hii, lakini haiwezekani kuwa yeye ale kiapo hata kama Waaria wengine wamwue. Lakini kama akila kiapo, basi ghera ya Mungu itaonyesha ishara kubwa sana, itaonyesha ishara ambayo uamuzi utatolewa humu humu duniani na ardhi itajaa kwa nuru ya kimbingu.

**Ishara ya kumi** ni hii kuwa miezi mitatu au minne kabla ya kufariki kwa Pandit Dayanand, Mungu Alinipasha habari ya kifo chake, nami nikampa habari hizi yule yule Mwaria ambaye ameishatajwa hapo kabla, na nikawaambia watu wengine wengi kadha. Basi, baada ya ufunuo huo mpaka muda ulioelezwa juu habari ya kifo cha Pandit huyo ilifika. Bishara hii pia imeandikwa ndani ya *Barahine Ahmadiyya*. Kama Mwaria huyo akikataa, basi jibu langu ni lile lile nililoishatoa hapo kabla.

**Bishara ya kumi na moja** ni hii kuwa Mwenyezi Mungu kwa njia ya ufunuo Aliniambia kuwa nimejaliwa balagha na ufasaha wa kimwujiza katika

lugha ya Kiarabu, na katika jambo hili hakuna atakayenishinda. Bishara hii inaashiriwa ndani ya *Barahine Ahmadiyya* ukurasa 239 ambamo Amesema:

إِنْ هٰذَا إِلَّا قَوْلُ الْبَشَرِ وَأَعَانَهُ عَلَيْهِ قَوْمٌ آخَرُوْنَ ۔ قُلْ هَاتُوْا بُرْهَانَكُمْ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِيْنَ ۔ هٰذَا مِنْ رَّحْمَةِ رَبِّكَ يُتِّمُ نِعْمَتَهُ عَلَيْكَ لِيَكُوْنَ آيَةً لِّلْمُؤْمِنِيْنَ

Yaani, wapinzani watasema kuwa hii ni kauli ya mwanadamu na watu wengine wamemsaidia. Sema, leteni dalili juu yake kama m wakweli, yaani hakikisheni kwa kufanya mashindano. Bali hii ni kutokana na rehema ya Mungu, ili Akukamilishie neema yake, na ili iwe ishara kwa ajili ya waaminio. Yaani hii itakuwa ishara moja juu ya ukweli wako. Na hivyo ndivyo ilivyotokea.[33] Katika kipindi hiki mimi niliandika vitabu vingi vizuri sana katika lugha ya Kiarabu kwa kutunza ubora wa utungo na balagha na ufasaha, na nikawashawishi wapinzani washindane dhidi yake mpaka nikawawekea zawadi za rupia elfu tano kama wakiweza kuandika mfano wake. Lakini dhidi ya vitabu hivi hawakuweza kuandika

---

[33] Bishara hii inatiliwa nguvu na ni ufunuo ule wa *Barahine Ahmadiyya* ambapo imeandikwa: يَا أَحْمَدُ فَاضَتِ الرَّحْمَةُ عَلٰى شَفَتَيْكَ Yaani, Ee Ahmad! Rehema yatiririka midomoni mwako, yaani, ufasaha na balagha. Mwandishi.

chochote. Basi, kama hiki hakingekuwa kitendo cha Mwenyezi Mungu, mamia ya vitabu vingeandikwa dhidi ya hivyo, hususan katika hali hii ambapo msingi wa ukweli na uongo uliwekwa juu ya hivyo tu na kwa maneno ya wazi ilikuwa imetajwa kuwa kama wao waweze kuvunja ishara hii kwa kitabu chochote dhidi yake, basi dai letu litabatilika. Lakini watu hao wakashindwa kabisa kushindana. Na vivyo hivyo wale Mapadre wanaompachika jina la sheikh mtu yeyote jahili wa kawaida anayeritadi, wakashindwa kabisa kushindana kiasi kwamba hawakuthubutu hata kuelekea upande huo. Na ubora wa bishara hii ni kuwa hii iliandikwa miaka kumi na sita au kumi na saba kabla ya kuwepo kwa vitabu hivi vya Kiarabu. Je mwanadamu anaweza kufanya hivi?!!

**Bishara ya kumi na mbili** iliyoandikwa ndani ya *Barahine Ahmadiyya* kwenye ukurasa wa 238 na 239 ni elimu ya Kurani. Muhtasari wa bishara hii ni kwamba Mwenyezi Mungu anasema kuwa wewe umejaaliwa elimu ya Kurani, elimu itakayofutulia mbali batili. Na ndani ya bishara hii hii Amesema kwamba kuna watu wawili waliopewa baraka nyingi sana, mmoja ni Mwalimu yule ambaye jina lake ni Muhammad Mteule[saw] na mwingine ni huyu Mwanafunzi, yaani mwandishi wa kitabu hiki. Na hii

inaashiria pia kwenye aya ya Kurani Tukufu ambamo Mwenyezi Mungu Mwenye shani adhimu Anasema:

وَاٰخَرِيْنَ مِنْهُمْ لَمَّا يَلْحَقُوْا بِهِمْ [34]

Yaani, Nabii huyo anao wanafunzi wengine pia ambao hawajadhihiri bado, nao watadhihiri katika zama za mwisho. Aya hii iliashiria kwangu mimi tu, kwani kama ilivyoelezwa sasa hivi ndani ya ufunuo, mimi ni miongoni mwa wanafunzi wa Mtume[saw] kiroho. Na bishara hii inayoashiria kwenye yaliyofundishwa na Kurani, kwa kuisadikisha hiyo kitabu '*Karamaatus-Saadikiin*' kiliandikwa ambacho hakuna mpinzani yeyote aliyejielekeza kwacho. Nami naapa kwa jina la Mungu Yule Ambaye uhai wangu umo mikononi mwake kuwa katika kufahamu elimu ya ndani na maarifa ya Kurani nimepewa ushindi juu ya kila roho. Na kama sheikh yeyote mpinzani angejitokeza kushindana na mimi, kama nilivyowaita mara kwa mara, kuja kuandika maelezo ya Kurani, basi Mungu Angemdhalilisha na kumwaibisha. Hivyo, ufahamu wa Kurani niliojaliwa mimi ni ishara moja ya Mungu Mwenye shani. Ninatarajia kwa fadhili ya Mungu kuwa dunia itaona hivi karibuni kwamba katika

---

[34] Na kwa wengine miongoni mwao walio bado kuungana nao. Sura Al-Jumu'a, 62:4

kauli hii mimi ni mkweli. Na kauli ya masheikh kuwa maana sahihi za Kurani Tukufu ni zile tu zinazoweza kufahamika kutoka ndani ya Hadithi sahihi, na kueleza zaidi ya hizo ni dhambi sembuse yaeleweke kuwa ni bora, mawazo haya ni batili tupu. Madai yetu ni kuwa Kurani imekuja kwa kurekebisha kikamilifu na kutakasa kitimilifu na kikamilifu. Na inadai yenyewe kuwa kweli zote kamili zimo ndani yake, kama isemavyo:

فِيهَا كُتُبٌ قَيِّمَةٌ[35]

Hivyo, katika hali hii ni lazima kwamba mpaka pale panapoweza kuenea maarifa na elimu za kimbingu mpaka hapo mafundisho ya Kurani Tukufu yawe yamefika. Na si mimi tu ninayesema jambo hili, bali Kurani yenyewe inainasibisha sifa hii kwake na inajiita kitabu kamili kuliko vitabu vyote. Hivyo basi ni dhahiri kuwa kama katika maarifa na elimu za kiungu ingebaki hali fulani isiyotaja Kurani Tukufu, hapo Kurani Tukufu haingekuwa na haki ya kujiita jina kitabu kamili kuliko vitabu vyote. Hatuwezi kuzipa Hadithi daraja zaidi ya hii kwamba hizo ni kama maelezo ya yale mambo yaliyotajwa kwa ufupi

[35] Ndani yake yamo mafundisho ya kudumu. Sura Al-Bayyina, 98:4

ndani ya Kurani. Ni majahili sana na wasiofaa wale watu ambao hawaisifu Kurani Tukufu namna ilivyo ndani ya Kurani Tukufu, bali wanajaribu kuishusha kwenye daraja dogo la kawaida. Ilmuradi, hii pia ni bishara moja niliyojaliwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu ambayo hakuna mpinzani yeyote aliyeweza kuikabili na Mungu Akawadhalilisha maadui wote. Juu ya maarifa ya kimuujiza ya Kurani yasiyo na mipaka kuna hoja moja hii pia kwamba maana yake ya dhahiri na ya kawaida anaijua kila mwaminio na fasiki, Mwislamu na kafiri, na hakuna sababu asiijue, sasa manabii na wenye maarifa wana ubora gani juu yao? Na tena hii itakuwa na maana gani kuwa:

لَا يَمَسُّهٗٓ اِلَّا الْمُطَهَّرُوْنَ[36]

**Bishara ya kumi na tatu** ni ile iliyoandikwa ndani ya *Barahine Ahmadiyya* ukurasa wa 241, nayo ni hii اَلَا اِنَّ نَصْرَ اللّٰہِ قَرِیْبٌ۔ یَاْتِیْکَ مِنْ کُلِّ فَجٍّ عَمِیْقٍ۔ یَاْتُوْنَ مِنْ کُلِّ فَجٍّ عَمِیْقٍ۔ Yaani msaada wa Mungu utakufikia kutoka sehemu za mbali na watu watakujia kutoka sehemu za mbali. Na hivyo ndivyo ilivyotokea. Na wapinzani wetu pia wanajua kuwa wasaidizi wa Jumuiya yetu wanapatikana hadi pembe za India. Na kutoka Peshawar mpaka Bombay na Madras na mpaka

[36] Hapana atakayeigusa ila waliotakaswa. Sura Al-Waaqi'a, 56:80

Calcatta watu wanafanya safari za mbali na kufika Qadian, na bishara hii ni ya tangu miaka kumi na saba na iliandikwa wakati ambapo kulikuwa hakuna hata alama ya kuja huku kwa halaiki ya watu. Sasa yapasa kufikiri kuwa je hiki ni kitendo cha mwanadamu? Je, mwanadamu ana uwezo kwamba mambo ya siri yaliyofichika ya aina hii ambayo yangedhihiri baada ya muda mrefu ayaeleze kabla yake?

**Bishara ya kumi na nne** iliyomo ndani ya *Barahine Ahmadiyya* ukurasa huo huo wa 239 ni hii:

هُوَ الَّذِیْٓ اَرْسَلَ رَسُوْلَهٗ بِالْهُدٰی وَدِیْنِ الْحَقِّ لِیُظْهِرَهٗ عَلَی الدِّیْنِ كُلِّهٖ۔[37]
لَا مُبَدِّلَ لِكَلِمَاتِ اللّٰهِ۔ ظُلِمُوْا وَاِنَّ اللّٰهَ عَلٰی نَصْرِهِمْ لَقَدِیْرٌ

Yaani, Mungu ni Yule Aliyemtuma Rasuli wake pamoja na mwongozo na dini ya kweli ili Aifanye ishinde dini zote. Hakuna yeyote anayeweza kuyazuia maneno ya Mungu. Walidhulumiwa, na Mungu Atawasaidia. Aya hizi za Kurani

[37] Bishara hii iliyomo ndani ya Hadithi kuwa katika zama za Masihi Mau'udi mila zote zitaangamia isipokuwa Islam, siyo maana yake kuwa hakuna dini itayobaki ila Islam, kwani kutokea hivi ni kinyume cha Kurani Tukufu. Zifikirieni aya zile ambamo imeandikwa kuwa Wayahudi na Wakristo wataendelea kubaki mpaka Kiyama. Bali yamaanisha kuwa dini zote zitakufa na kudhalilika, na zitakufa kwa kulingana na Uislamu, isipokuwa Islam, kwani hii itadhihirisha nuru, uhai na ushindi wake. Mwandishi.

nilizofunuliwa zinanihusu mimi, na Rasuli muradi wake ni aamriwaye na aliyetumwa aliyedhihiri kuipa nguvu dini ya Kiislamu. Muhtasari wa bishara hii ni kuwa Mungu Aliyemwinua Mtume huyu sababu yake ni kwamba kwa mkono wake Aishindishe dini ya Kiislamu juu ya dini zingine zote. Na mwanzoni ni lazima kwamba aliyetumwa huyo na Jumuiya yake wafanyiwe dhuluma, lakini hatimaye utapatikana ushindi na dini hii kupitia huyu aliyetumwa itazishinda dini zote na mila zingine zote zitaangamia kwa hoja. Angalieni, hii ni bishara yenye shani adhimu kiasi gani, na hii ni bishara ile ile ambayo wanazuoni wengi waliendelea kusema tangu mwanzoni kuwa inahusikana na Masihi Mau'udi na itatimia katika zama zake. Na hii iliandikwa ndani ya *Barahine Ahmadiyya* miaka kumi na saba kabla ya madai ya kuwa Masihi Mau'udi ili Mungu Awaaibishe wale wanaoyadhania madai yangu kuwa ni uzushi wa kibinadamu. Barahin chenyewe kinatoa ushahidi kuwa wakati huo sikuwa hata na wazo la kuwa Masihi Mau'udi nami nilikuwa na itikadi ya zamani, lakini ufunuo wa Mungu ulishuhudia wakati huo kuwa wewe ni Masihi Mau'udi. Kwani yale yote yaliyoelezwa na Hadithi za Mtume[saw] kumhusu Masihi, ufunuo wa Mungu ulikuwa umethibitisha

ndani yangu. Hata kwamba ndani ya hii hii *Barahine Ahmadiyya* Akaniita pia jina Isa. Ndani ya ukurasa wa 556 wa *Barahine Ahmadiyya* upo ufunuo huu:

يَا عِيْسٰى اِنِّيْ مُتَوَفِّيْكَ وَرَافِعُكَ اِلَيَّ وَمُطَهِّرُكَ مِنَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا وَجَاعِلُ الَّذِيْنَ
اتَّبَعُوْكَ فَوْقَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا اِلٰى يَوْمِ الْقِيَامَةِ ثُلَّةٌ مِّنَ الْاَوَّلِيْنَ وَثُلَّةٌ مِّنَ الْاٰخِرِيْنَ

Yaani, Ewe Isa! Mimi Nitakufisha kifo cha kawaida na Nitakuinua kwangu na Nitawapa wafuasi wako ushindi juu ya wale watu wanaokupinga. Na wafuasi wako watakuwa wa aina mbili, kundi la kwanza na kundi la nyuma. Aya hii ilimshukia Hadhrat Masihi wakati alipokuwa na wasiwasi mkubwa kuhusu uhai wake kutokana na njama za Wayahudi. Na Wayahudi kwa sababu ya uovu wao walikuwa wanamfikiria kumsulubisha, ili kwa kutiliwa doa la kifo cha tuhuma ahakikishiwe kuwa maluuni, kwani ndani ya Torati ilikuwa imeandikwa kuwa yule atundikwaye mtini amelaaniwa kwa vile msalaba ulikuwa na uhusiano kiasi fulani na wahalifu kwa sababu ya kuwa njia ya zamani ya kuadhibu, na kila mwuaji na mwovu wa daraja la juu alikuwa anaadhibiwa kwa msalaba, hivyo takdiri ya Mungu ikaharamisha msalaba juu ya wakweli ili mtakatifu asishabihiane na mwovu. Hivyo, ni jambo la ajabu kuwa hakuna nabii yeyote aliyekufa msalabani ili ukweli wao usitiliwe shaka mbele ya watu kwa jumla.

Ilmuradi, katika aya hii Mwenyezi Mungu Alimtuliza Hadhrat Masihi katika zama za mahangaiko ambapo Mayahudi walikuwa wanafanya hila za kumfisha msalabani. Sasa aya hii iliyoniteremkia mimi kwa sura ya ufunuo, ndani yake mna ishara hii nyepesi kuwa mimi pia nitapatwa na tukio la aina hii kwamba watu watakula njama ya kuniua au kusulubisha ili mimi nipate adhabu ya wahalifu sugu na ukweli utiliwe shaka. Hivyo basi katika aya hii Mwenyezi Mungu kwa kuniita jina Isa na kwa kuelezea kunifisha, Anaashiria kuwa njama hizi hazitafanikiwa na Mimi Nitakulinda na shari zao. Na mbele ya ufunuo huo kuna ufunuo uliomo kwenye uk. 557, ndani yake imedhihirishwa kuwa lini itatokea hivi na ni alama gani ya siku hiyo. Yaani, njama za aina hii zitakazofanywa kwa kuniua, zitakuwa lini na wakati gani, na mambo gani hayana budi kudhihirika kabla yake. Hivyo, ufunuo ulio baada ya ufunuo huu, ndani yake imeashiriwa habari hii, nayo ni hii: **Mimi Nitaonyesha mng'ao wangu. Kwa dhihirishao la kudra yangu Nitakuinua (haya ni maelezo ya رَافِعُكَ اِلَیَّ). Mwonyaji mmoja alikuja duniani, lakini dunia haikumkubali, lakini Mungu Atamkubali na kwa mashambulizi makali Atadhihirisha ukweli wake.** Katika ufunuo huu, Mwenyezi Mungu Amesema

kwa maneno ya wazi kuwa wakati wa njama za mauaji utakuwa ule ambapo ishara moja ing'aayo itadhihirika kwa sura ya shambulio. Hivyo, baada ya ufunuo huu, kuna ufunuo uliomo kwa lugha ya Kiarabu, huo pia unaashiria kwenye fitina ya mada ya mauaji. Nao ni huu:

اَلْفِتْنَةُ هٰهُنَا فَاصْبِرْ كَمَا صَبَرَ اُولُو الْعَزْمِ ۔ فَلَمَّا تَجَلّٰى رَبُّهٗ لِلْجَبَلِ جَعَلَهٗ دَكًّا ۔ قُوَّةُ الرَّحْمٰنِ لِعُبَيْدِ اللهِ الصَّمَدِ ۔ مَقَامٌ لَا تَتَرَقَّى الْعَبْدُ فِيْهِ بِسَعْيِ الْاَعْمَالِ

Tafsiri yake ni hii kuwa ishara hii ing'aayo itakapodhihiri, wakati huo itaibuka fitina moja.[38]

---

[38] Vikao vya siri na mashauriano ya siri waliyofanya Waaria na Mabaniani kwa kuniua, kuhusiana nayo barua karibu hamsini zimeshanifikia. Baadhi ya barua hizo ni za Mabaniani wasioandika majina yao na baadhi yao ni za Waislamu wenye heshima waliopata taarifa za mashauriano haya. Wakati huu haina haja ya kunakili barua hizo. Hizo zote zimehifadhiwa kwangu. Lakini ninanukuu toka kwenye *Hindu Akhbar* baadhi ya mifano ili ifahamike kuwa jaribio aliolipata Hadhrat Isa kutokana na shari za Wayahudi, ndilo hilo nililolipata mimi. Na kutokana na neno hili la 'fitina' lililopo ndani ya ufunuo: اَلْفِتْنَةُ هٰهُنَا mradi wake ni jaribio lile lile na kwa sababu hii hii pamwe na sababu zingine, niliitwa jina Isa. Fitina ya Wayahudi ilikuwa na sehemu mbili. Sehemu moja ilikuwa ni njama zao za kumwua Hadhrat Isa[as] na sehemu ya pili ilikuwa ni kwamba walikuwa wakichochea serikali ya Kirumi kwa kumkamata na kumwua Hadhrat Isa[as]. Basi, siku hizi pia mambo ni yayo hayo, tofauti ni hii tu kwamba kule walikuwa Wayahudi na hapa ni Mabaniani. Hivyo, sehemu ya kwanza ambayo ni njama za siri za kuniua, mfano wake unajulikana katika makala ile ya

(Hii ni fitina ile ile ya njama ya mauaji ambayo kwa

---

M.R. Bashishar Das aliyoichapishia ndani ya gazeti la *Aftabe Hind*, toleo la tarehe 18 Machi 1897, kwenye safu ya kwanza, ukurasa wa 5, ambayo kichwa chake cha habari ni hiki: "Jihadhari Mirza wa Qadian". Kisha baada yake ameandika kwamba "Hata Mirza Qadiani ni mgeni wa siku chache tu. Mtu hawezi kuepa takdiri yake. Siku hizi fikara za Mabaniani kuhusiana na Mirza wa Qadiani zimevurugika mno. Hivyo Mirza wa Qadiani anapaswa kujihadhari isije akawa pia dhabihu ya Idi kubwa." Halafu ndani ya gazeti la *Rahbare Hind* , Lahore, la 15 Machi 1897, imeandikwa katika safu ya kwanza ya ukurasa wa 14, "Inasemekana, Mabaniani watapanga auliwe yale mtu wa Qadiani."

Na sehemu ya pili inayohusiana na kuichochea serikali, imebainishwa katika magazeti yafuatayo yanayotolewa na Mabaniani: Gazeti la *Panjab Samachar* la 27 March 1897 ambalo ni gazeti la Mabaniani linalochapishwa Lahore, linaichochea Serikali kwenye uk. 5 hivi: "Kwanza kabisa, iliyoleta wazo hili (yaani wazo la njama ya mauaji) ni bishara ya Mirza Ghulam Ahmad wa Qadiani." Tena, kwenye uk. 6 wa gazeti hili hili imeandikwa, "Bwana Mirza anakubali kwamba kifo cha bwana Pandit kilitakiwa kutokea tarehe 2 Shawali." Yaani ikatokea vile vile ile ishara iliyokuwa ndani ya utabiri kuhusiana na tarehe 2 Shawali. Basi, hii ni dalili ya kutosha kwamba mauaji haya yalitokea kwa njama za yule aliyetoa utabiri. Kisha imeandikwa ndani ya toleo la tarehe 10 March 1897 la gazeti hili hili: "Bwana fulani (yaani mimi), alitoa utabiri huu pia ndani ya kitabu chake, *Mau'ud Masihi,* kwamba Pandit Lekhram atakufa katika hali yenye uchungu

mnasaba wake mimi nilikuwa nimeitwa kuwa 'Ewe

sana, ndani ya muda wa miaka sita, mnamo siku ya Idi." Sasa, gazeti hili linaielekeza serikali likitaja jina la Idi kwamba kutoa habari kama hii ni dalili ya njama za binadamu. Lakini amefanya makosa katika kuieleza siku ya Idi; ndani ya Ufunuo wa Mungu mmeashiriwa siku ya pili ya Shawali.** Halafu imeandikwa kwenye ukurasa wa pili wa gazeti hili hili: "Aliteuliwa mtu kwa kuua. Huku muda wa utabiri wa mwandishi wa *Mau'ud Masihi* ulikuwa karibu pia, kwani labda mwaka 1897 ulikuwa ni wa sita na 5 Machi ya mwaka huu ilikuwa ni Idi ya mwisho ya mwaka wa sita." Ndani yake makosa yaliyomo hayahitaji kuelezwa. Kwa vyovyote, mradi wa maneno haya ni kwamba njama hii ilikuwa imepangwa kwamba auawe siku ya Idi au siku inayoikaribia Idi. Kisha kwa kulititilia nguvu wazo hili, anaandika ndani ya gazeti hili hili kwamba: "Mauaji haya ni matokeo ya njama madhubuti iliyofanywa na watu kadhaa kwa kufikiria kwa muda mrefu ambayo mashauriano yake yalikuwa yakiendelea kwa muda mwingi karibu na Amritsar na Gurdaspur na kandokando ya huko Delhi na Bombay. Je si yawezekana sana kwamba chanzo cha njama hii ndio watu wale waliokuwa wakisema hadharani kwa njia ya maandiko na maongezi kwamba watamwua Pandit, na zaidi ya hayo ni hii kwamba Pandit atakufa ndani ya muda fulani na siku fulani katika hali ya uchungu. Je mpinzani wa Aria Dharam aliye mwandishi maalum wa vitabu vichache hahusiki na njama hii?" Katika habari hii, gazeti hili linataka kuieleza serikali kwamba

**Katika ufunuo, Mwenyezi Mungu Amemwita Lekhram kwa jina la عِجْلٌ جَسَدٌ لَّهٗ خُوَارٌ Yaani, ndama ya Samiri. Ndani yake pia kuna ishara

Isa' ndani ya ufunuo uliotajwa. Yaani, fitina ya kunuia

---

hii hii kwamba atakufa katika siku za idi, kwani mpaka sasa imeandikwa katika Torati kwamba ndama ya Samiri pia iliangamizwa siku ya idi na siku ya pili ya idi pia ni kama siku ya idi. Mwandishi.

mtu wa aina hii aliyeweka muda, akaitaja siku ya mauaji na akaendelea kusema kwa mdomo kwamba atakufa siku fulani, je huyo hahusiani na njama za mauaji haya? Kisha gazeti lingine liitwalo *Akhbare Aam* limeandika kuhusiana na muuaji ya Lekhram katika toleo lake la 16 March 1897, ukurasa wa 3, kwamba: "Habari za uvumi wa aina aina zimeenea, na mwenendo wa Bwana wa Qadian ni wa ajabu sana… Kwa masikitiko makubwa sana inabidi kukubali kwamba Bwana Mirza wa Qadian analazimika kwamba alipotabiri mauaji ya Lekhram kwa nguvu ya ufunuo basi kwa nguvu hiyo hiyo ya ufunuo atuambie mwuaji wake ni nani?" Kisha mhariri wa *Akhbare Aam* anaandika ndani ya toleo lake la 10 March 1897 kwamba: "Kama tukio la aina hiyo lingemtokea bwana Deputy, yaani Atham, ambalo madhara yake aliyavumilia Lekhram, hapo hali ingekuwa tofauti." Yaani, katika hali hii serikali lazima ingemkamata yule aliyetoa utabiri. Vivyo hivyo, gazeti la *Anise Hind,* Meerut, likiashiria kuuawa kwa Lekhram, linaandika ndani ya toleo lake la Machi: "Tulihisi hofu wakati ule ule ambapo Mirza Ghulam Ahmad Qadiani alitoa utabiri kuhusiana na kifo cha Lekhram. Je alikuwa na elimu ya ghaibu?"

Na vivyo hivyo ndani ya magazeti mengine mengi ya Mabaniani wamedhihirisha mawazo yao ya kuleta ufisadi kwa namna mbalimbali. Nami naona kwamba hakuna haja ya kuandika zaidi ya hayo, kwani katika Panjab kelele za kuleta uchafuzi zinapigwa sana, na atakuwa kwa nadra sana asiyejua habari hii. Mwandishi.

kuniua au kusulubisha). Ndani ya ufunuo huu kwanza niliitwa jina Isa, na kisha ikaahidiwa kuwa 'Mimi Nitakufisha'. Na aya ile ile iliyomo ndani ya Kurani Tukufu kuhusiana na ahadi ya kifo cha Hadhrat Isa, ikafunuliwa kunihusu mimi mnyenyekevu kuwa:

يَا عِيْسٰى اِنِّيْ مُتَوَفِّيْكَ وَرَافِعُكَ اِلَيَّ

Na kama nilivyoandika sasa hivi, bishara hii ilihitajika pia kwa ajili ya Hadhrat Isa kwa kuwa wakati huo kutokana na vitisho vya kila siku vya Wayahudi, maisha yake yalikuwa hatarini. Na Wayahudi walikuwa wanamtishia mauti waliyoyafahamu ni mauti ya wahalifu na ambayo sawa na Torati pia ukweli wa mtu hutiliwa doa. Ndiyo maana Mwenyezi Mungu katika wakati wa hatari wa namna hii Akamwepusha na kifo kichafu na cha laana cha aina hii. Basi katika ufunuo huu niliofunuliwa — uliokuwa ni aya hii hii — kuna bishara nzuri sana iliyotabiriwa miaka 17 mapema tangu siku ya leo, nayo kwa sauti ya juu inaeleza kuwa tukio hilo litatukia hapa pia. Na kusema kwa kuniita jina Isa, kuwa "Ewe Isa, Mimi Nitakufisha na Nitakuinua kwangu," kwa kweli ni kuonyesha picha ya tukio lile lililomsibu Hadhrat Isa[as]. Na tukio lile lilikuwa ni kuwa Wayahudi walitaka kumwua

kwa nia hii kuwa wathibitishe kuwa yu mwongo. Nao walichukua hatua hii kuwa sisi tutamwua kwa kumsulubisha, na anayesulubiwa huwa mlaaniwa. Na maana ya laana ni kuwa mtu anakosa imani, anapotoka na kuwa mbali na Mungu na kuachwa naye, na kwa njia hii utathibitika uongo wake. Na Mungu Akamtuliza kuwa wewe hutakufa kifo kitakachokuwa na matokeo kuwa u mlaaniwa, mbali na Mungu na kutengwa naye; bali Mimi Nitakuinua kwangu, yaani Nitathibitisha u karibu nami sana.[39] Na Wayahudi watashindwa katika shabaha yao hii. Hivyo, ndani ya maana ya neno رَفْعٌ mlikuwa na bishara moja pia iliyofichika ya kuja kwa Mtume wetu[saw], kwani ukweli ulioahidiwa kudhihiri sana ukatokea kwa kudhihiri kwa Mtume wetu[saw]. Na Mwenyezi Mungu Hakumwacha Nabii wake mmoja

[39] Ahadi hii hata mimi pia nilipewa kuwa Mimi Nitakufisha, na Nitakuinua kwangu. Na aya ile ile kwa njia ya ufunuo Ameiteremsha kwa ajili yangu mimi pia, ambayo maulamaa wetu wanamaanisha kunyanyua kimwili. Na mimi nimekwisha thibitisha kwa hoja kuwa aya hii imefunuliwa kwa ajili yangu pia. Je kunihusu mimi pia yafaa kuwa na itikadi kuwa mimi nitainuliwa mbinguni pamoja na mwili wangu? Mkisema kuwa ufunuo wako hauthibitiki, basi udhuru huu utakuwa mbovu, kwa sababu bishara safi iliyomo katika ufunuo huu imeshadhihiri tayari, basi kwa dalili hii hii ukweli wa ufunuo umethibitika. Mwandishi.

mkweli bila ushahidi.

Ilmuradi, bishara hii hii kunihusu mimi imo ndani ya *Barahine Ahmadiyya* kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na iliishachapishwa miaka 17 mapema tangu leo. Basi, ufunuo huu ulifunuliwa kwa sababu ile ile ambayo ilikuwa ni sababu ya huo kufunuliwa kwa Hadhrat Masihi sawa na hali aliyokuwa nayo. Yaani, kama vile wakati ule ufunuo huu ulivyomshukia Hadhrat Isa ili aambiwe kabla ya wakati kwamba utafanyiwa njama za mauaji, na Mimi Nitakuokoa, ndivyo ilivyo shabaha ya ufunuo huu pia. Kama kuna tofauti, basi ni hii tu kuwa wakati ule waliokula njama za mauaji walikuwa ni Wayahudi na sasa ni Mabaniani. Na Wayahudi waliifikiria njia hii ya kumkadhibisha Hadhrat Masihi kwamba kwa kumfisha msalabani itajulikana yu mlaaniwa kwa mujibu wa Torati, na mjumbe mkweli hawezi kuwa mlaaniwa. Hivyo, kwa njia hii kuwa kwake mwongo kutathibitika nyoyoni mwao. Na kwa sababu ya mwisho wa maisha wenye fedheha kama hii hakutakuwa na yeyote wa kutaja hata jina lake. Ilikuwa ni huzuni kubwa ya kifo hiki hiki iliyompa Hadhrat Isaas jazba ya kufanya maombi usiku kucha, na alipotundikwa msalabani wa ikamtamkisha "Eli

Eli lama sabaktani"[40]. Waila Nabii anaweza kuwa na huzuni gani ya kifo chake! Kaumu hii shujaa huikanyaga huzuni ya kifo chini ya miguu. Woga wa aina hii tuwezaje kuunasibisha kwa moyo wa Nabii! Bali, ilikuwa ni hofu ya fitina ya laana iliyomwumiza moyo wake. Mwishoni, Mungu Akamwokoa mja huyo. Na ndani ya bishara ya *Barahine Ahmadiyya* mna ishara hii kuwa njama hii hii dhidi yako itakula kaumu moja. Basi, siku hizi baada ya kifo cha Lekhram, Mabaniani wakafanya hivyo hivyo na wanaendelea kufanya. Lakini kwa kunikadhibisha wamefikiria jiha hii nyingine kwamba ikiwezekana, basi huyu pia tumwue karibu na idi, na kwa njia hii kwa kuiharibu bishara ya Mungu waifutilie mbali adhama ya Kiislamu mioyoni, na wawaelekeze watu upande huu kuwa kama vile Lekhram alivyouawa kwa muafaka wa bishara iliyotolewa kabla, vivyo hivyo mtu huyu pia alivyouawa kutokana na bishara yetu iliyotolewa kabla. Hivyo basi, kama ule unaweza kuwa ufunuo wa Mungu, neno letu pia linatakiwa kuitwa ufunuo wa Mungu.

Hivyo, kwa njia hii duniani kutazuka vurugu na watu kwa kumwona maiti moja wa Waislamu

[40] Mungu wangu Mungu wangu, mbona Umeniacha!

kulingana na maiti moja wa Mabaniani watafikia uamuzi kuwa njama zote mbili ni za kibinadamu. Kwa njia hii uongo wa mtu huyo utathibitika kwa urahisi. Hivyo basi Wayahudi na Mabaniani wako pamoja katika shabaha ya kukadhibisha, ila tu wakafikiria jiha mbili mbalimbali. Hivyo, Mungu Alifahamisha miaka kumi na saba mapema tangu wakati huu kwamba kama Wayahudi walivyoshindwa katika shabaha yao, ndivyo Mabaniani watakavyoshindwa pia katika shabaha yao. Na kwa maneno ya wazi Akafahamisha kuwa njama hii ya mauaji itafanywa wakati ambapo ishara moja ing'aayo itadhihiri kwa sura ya mashambulizi, na baada ya shambulio hilo kutazuka fitina moja, mfano wa fitina iliyofanywa kuhusu Masihi. Na pamoja na ufunuo uo huo kuna ufunuo kwa lugha ya Kiarabu ambao unamaanisha kuwa Mungu Ataiondolea mbali milima ya matatizo, na hayo yote yatafanyika kwa nguvu ya Rahmani.

Na katika kuuunga mkono ufunuo huu huu kuna ufunuo mmoja kwenye uk. 506 wa Brahine Ahmadiyya, ambamo mna ahadi ya ishara ya wazi wazi kwa ajili ya Mabaniani na Wakristo, kama Alivyosema:

لَمْ يَكُنِ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا مِنْ اَهْلِ الْكِتَابِ وَالْمُشْرِكِيْنَ مُنْفَكِّيْنَ حَتّٰى

تَأْتِيَهُمُ الْبَيِّنَةُ وَكَانَ كَيْدُهُمْ عَظِيمًا۔

Yaani, washirikina na Wakristo hawangeacha kukadhibisha bila kuona ishara ya wazi wazi na hila yao ilikuwa kubwa sana. Na kisha Akasema kuwa kama Mungu Asingefanya hivyo dunia ingechafuliwa. Hii ni ishara ile ile ya wazi wazi iliyoelezwa mahali pengine kwa neno la mng'ao, ambayo ni ishara ya kifo cha Lekhram. Na ni dhahiri shahiri kuwa Mwenyezi Mungu Ameidhihirisha ishara hii kwa uwazi kabisa, maana ndani ya bishara hii ulielezwa muda, ilielezwa siku ya pili ya Idi, na ilielezwa kifo kitatokea kwa njia ya mauaji, na maneno ya kashfi yalielekeza wazi kabisa kuwa kifo kitatokea siku ya Jumapili na kitatokea wakati wa usiku. Basi, mambo yote haya yalidhihirika vivyo hivyo kama yalivyosemwa hapo kabla. Na tuhuma ya Mabaniani ya njama, na tuhuma ya nia ya mauaji hawezi kutia shaka katika usafi wa bishara hii, maana sasa hivi tumeisha elezea kuwa ndani ya *Barahine Ahmadiyya* bishara hii imo kuwa wakati wa kudhihiri ishara hii kutakuwa na fitina moja, na fitina hiyo itafanana na fitina ile waliyoanzisha Wayahudi kuhusiana na Hadhrat Isaas. Yaani juhudi ya kumwona msalabani kupitia serikali au wenyewe kula njama ya kumuua.

Na hapa ikumbukwe kuwa Mabaniani kadha na

wapinzani wetu wengine wanataka kutia mavumbi juu ya bishara hii. Hiyo haitakuwa kamwe, kwani hiki ni kitendo cha Mwenyezi Mungu, kwa hiyo Mwenyezi Mungu kabisa Hatakiacha kipotee. Bali Yeye siku hadi siku Atadhihirisha usafi wake. Na kadri watu watakavyoendelea kuielewa bishara hii, ndivyo watakavyovutika kwake. Je, haitoshi kwa ajili ya adhama ya bishara hii kuwa zaidi ya maelezo yote yaliyomo ndani ya bishara hii, bishara hii ilielezwa katika *Barahine Ahmadiyya* pia miaka kumi na saba kabla ya kutokea hiyo.

**Bishara ya kumi na tano** ni bishara inayomhusu Deputy Abdullah Atham, ambayo ilitimia kwa uwazi sana. Ndani ya ufunuo wa bishara inayomhusu Atham huyo mlikuwa na sharti la wazi kuwa kama ataelekea kwenye haki, basi kifo kitaahirishwa. Naye akathibitisha kurejea kwenye haki katika muda wa bishara kwa kauli yake na vitendo vyake. Yeye si tu aliikiri hofu bali ndani ya muda wa bishara akakaa faraghani mfano wa mfu.[41] Katika kipindi hicho,

---

[41] Atham ndani ya muda wa bishara, uliokuwa miezi kumi na mitano, akaachana na tabia zake za kufanya mabishano na mijadala kiasi hiki kwamba mfano wake haupatikani katika maisha yake yote ya kabla. Yeye ndani ya muda huu hakuandika hata mstari mmoja wa upinzani. Hivyo, huu ni uthibitisho dhahiri na wazi juu

safari moja alipata homa, hapo akasema akilia "Hae, mimi nimekamatwa". Yeye katika kipindi hicho akaacha mijadala yote kana kwamba hakuwa na ulimi kinywani. Ndani ya siku za muhula alionyesha mabadiliko yake ya ajabu, kana kwamba yeye siye Atham yule. Hivyo basi ingawa mabadiliko haya na hofu na huzuni vilivyoonekana usoni mwake vilikuwa ni dalili ya kutosha ya kurejea kwake lakini zaidi ya hilo akatoa ithibati hii pia kuwa mimi nikamwambia kwamba Mwenyezi Mungu Ameniambia kuwa wewe ndani ya muda ule lazima ulikuwa unaogopa na lazima ukajitenga na mwenendo wa ujasiri wa Kikristo na ukaathirika na heba ya Islam, ambayo ni aina mojawapo ya kurejea. Na kama jambo hili si sahihi, basi wewe unatakiwa ule kiapo, nasi tutakukabidhi rupia elfu nne bila kuchelewa, lakini hakula kiapo wala hakuthibitisha tuhuma zake za uongo kwa kunishtaki ambazo akazitaja kuwa msingi wa kuogopa kwake, yaani lawama hii kwamba sisi tulimtumia nyoka aliyefundishwa, na tukamtumia baadhi ya maaskari wenye silaha. Hivyo, kwa mambo haya ilithibitika kabisa kuwa lazima alirejea. Na ilikuwa pia katika ibara ya ufunuo

---

ya jambo hili kuwa yeye ndani ya siku za bishara alijitenga na tabia zake za zamani, na huku ndiko kulikuwa ni kurejea. Mwandishi.

kwamba kama hataendelea kuwa imara katika kurejea kwake na ataificha haki, hapo atakufa haraka. Basi, yeye kwa kuificha haki akafariki ndani ya miezi saba kuanzia tangazo la mwisho. Sawa na ufunuo, kufa kwake pia kunatoa ushahidi wa wazi kuwa kwa sababu ya kurejea tu aliweza kuishi kwa siku chache. Hili jambo ni wazi kabisa kuwa ndani ya ufunuo wa Mungu mlikuwa na jiha moja ya kuishi kwa ajili ya Atham na jiha moja ya kufa. Basi, sawa na maneno ya bishara, Mungu Akatimiza jiha zote mbili. Je, nafasi ya kuishi iliyo sharti la ufunuo imetungwa baadaye na haikuandkiwa katika ufunuo wa kwanza? Kama fahamu ni pungufu kiasi hiki, basi fahamuni kwa njia rahisi kuwa ndani ya maneno ya ufunuo hawiya lilitajwa na ukamilifu wa *hawiya* ulikuwa umetafsiriwa kuwa ni mauti. Sasa hebu semeni kweli kuwa je Atham ndnai ya muda wa bishara hakuwa anaishi katika hali ya wasiwasi ambayo ni mfano wa *hawiya*? Je, mnaweza kusema kuwa yeye alikuwa na amani na utulivu? Je, hii si kweli kuwa yeye baada ya kutoka nje ya muda ule na kwa kuung'ang'ania Ukristo alikufa katika miezi saba kuanzia tangazo letu la mwisho? Je, mnaweza kuonyesha kuwa mpaka sasa amekaa mahali fulani akiwa hai? Je, haya ni maneno ambayo mtu hawezi kuyaelewa? Sasa,

kama kung'ang'ania kukataa siyo kukosa imani, ni nini basi? Ukweli wenyewe ni kuwa dunia haiwezi kufurahi kwa jiha yoyote ile. Atham akawa mpole na kaona haya na moyo wake ukajaa hofu, hivyo Mungu sawa na sharti la ufunuo, katika siku za hofu Akaahirisha mauti. Lakini watu wa dunia wakasema, "Kwa nini Atham hakufa?" Na Lekhram hakuhofu hata kidogo na akaonyesha kejeli, basi Mwenyezi Mungu Akamhilikisha ndani ya muda kabisa, hapo watu wa dunia wakasema, "Kwa nini Lekhram amekufa, lazima kulikuwa na njama za kisirisiri". Hivyo, yule aliyeepushwa kufa ndani ya muda, juu yake pia makelele ya wapinzani yakazuka kwamba kwa nini alisalimishwa, na yule aliyekamatwa ndani ya muda juu yake pia kelele zikapigwa kwamba kwa nini amekamatwa.

Na kama habari inayomhusu Lekhram ilivyomo ndani ya *Barahine Ahmadiyya* miaka kumi na saba iliyopita, ndivyo hivyo habari inayomhusu Atham pia ilivyomo ndani ya *Barahine Ahmadiyya*. Mtu ambaye atasoma kwa makini ukurasa wa 241 wa *Barahine Ahmadiyya*, atalazimika kukubali kuwa kwa kweli ndani ya *Barahine Ahmadiyya* fitina hii ya Ukristo imetabiriwa iliyotokea baada ya kupita muda wa Atham. Kwa kufikiria mambo haya imani

ya mwaminio inapata nguvu, lakini ni masikitiko kuwa wapinzani wetu siku hadi siku wanazidi tu katika kukosa imani, haijulikani wameandikiwa nini ndani ya bahati yao. Hali za masheikh zinasikitisha zaidi, kwani hao waliambiwa bishara inayomhusu Atham kupitia Hadithi, lakini hawakujali kitu taarifa hii. Mtu mwenye busara atakapofungua ukurasa wa 241 wa *Barahine Ahmadiyya* na ndani yake baada ya habari ya Wakristo na hila zao na bishara ya ufichaji wa haki atasoma ufunuo huu: اَلْفِتْنَةُ هٰهُنَا فَاصْبِرْ كَمَا صَبَرَ أُولُو الْعَزْمِ, kisha kwa kuendelea mbele kwenye ukurasa wa 511, baada ya kutajwa mzushi mmoja Mwislamu jasiri, atakaposoma ufunuo huu: اَلْفِتْنَةُ هٰهُنَا فَاصْبِرْ كَمَا صَبَرَ أُولُو الْعَزْمِ , na kisha akiendelea mbele atakaposoma ufunuo huu tena kwenye ukurasa wa 557 baada ya maelezo juu ya ishara moja inayong'aa: اَلْفِتْنَةُ هٰهُنَا فَاصْبِرْ كَمَا صَبَرَ أُولُو الْعَزْمِ, hapo kwa kufikiria fitina hizi tatu zilizoandikwa miaka kumi na saba kabla ya wakati huu ndani ya *Barahine Ahmadiyya* kwenye uk. 241, uk. 511 na uk. 557, lazima swali litazuka moyoni mwake kuwa fitina hizi tatu ni za aina gani ambazo mojawapo katika hizo inawahusu Wakristo na nyingine yamhusu Mwislamu fulani mwenye hila na moja inahusikana na wakati wa kudhihirika ishara fulani ya wazi wazi. Kisha atakapoanza

kuyatafuta matukio atakuta kuna matata makubwa matatu yatakayokuja mbele ya macho yake ambayo kila moja katika hayo linastahili kuitwa fitina kubwa sana. Ndipo kwa kuangalia elimu ya kina ya Mungu lazima atamsujudia Yule Aliyetoa habari hizi wakati ilipokuwa hamna hata alama ya fitina hizi tatu. Kama fitina hizi tatu ziwekwe kama fumbo mbele ya ayajuaye hayo matukio, yeye mara moja atajibu kuwa fitina moja inahusu bishara juu ya Atham, iliyodhihirishwa na Wakristo na wasaidizi wao Waislamu mabahili, yaani Waislamu wale ambao ndani ya bishara hii wametajwa kuwa Wayahudi. Na fitina ya pili ni ya Muhammad Husain Batalawii ya kukufurisha. Na ya tatu ni fitina ile iliyozushwa na Mabaniani baada ya kudhihirika ishara ya Mungu. Hizo ni fitina tatu zilizodhihiri kama rabsha yenye kelele nyingi ambazo Mungu Alikuwa Ametoa habari zake miaka kumi na saba iliyopita!!!

Hakuna anayeweza kulikataa jambo hili kuwa miongoni mwa fitina hizo tatu kulikuwa hakuna fitina yoyote iliyokuwa bila vurugu na makelele ya kaumu na kila moja ilikuwa imejaa harara ya hali ya juu sana, na katika kila moja ikatokea vurugu isiyo ya kawaida. Na fitina ya Wakristo ilikuwa imetokea wakati Atham alipopatikana kuwa hai baada ya

muda wa bishara. Mapadri walikuwa wanajua vizuri kuwa ndani ya ufunuo kuhusu bishara mlikuwa na sharti la wazi kwamba Atham katika hali ya kurejea — ambalo ni tendo la moyoni — hatakufa ndani ya muda, na hili pia walijua sana kuwa Atham lazima aliendelea kuogopa heba ya bishara, na ndani ya siku za muda hakuweza kubaki imara katika ushupavu wake wa Kikristo, na kwa kukimbia vikao vyao akaenda kukaa faraghani Firozpur. Na hao walijua vizuri sana kuwa wakati alipougua alitamka pia kwamba "Nimekamatwa", nao walijua sana kuwa yeye kitabia alikuwa na roho ya kuogopa. Nao walielewa barabara kuwa yeye kwa vitendo vyake alidhihirisha hofu wala hakuonyesha uimara, na akazibadili hali zake za awali za chuki kiasi hiki kuwa ndani ya muda uliowekwa hakuchapisha hata makala ya misitari miwili ndani ya gazeti lolote dhidi ya dini ya Islam, wala hakuchapisha kijitabu kama yalivyokuwa mazoea yake tangu zamani, wala hakufanya mjadala na Mwislamu yeyote. Bali alipitisha siku kama vile mtu amefunga saumu ya kukaa kimya. Kisha la ajabu ni kuwa kwa ahadi ya kupewa rupia elfu nne pia hakula kiapo. Na Martin Clark akashindwa akimshauri kwa kung'ang'ani sana, lakini hakufungua mashtaka mahakamani. Pia hakuweza kuthibitisha tuhuma

za kuhusu nyoka aliyefundishwa n.k. Kutokana na sababu zote hizo, Mapadri wakatambua kwa yakini kwamba yu mwoga na hawafu. Na baada ya muda kwisha pia akalia kwa kukumbuka kisa chake. Lakini Mapadri hawakumwogopa Mwenyezi Mungu, na wakapitapita masokoni mwa Amritsar wakisema angalieni Bwana Atham yuko hai na bishara imethibitika kuwa ya uongo. Masheikh wengi wenye tabia chafu waliokuwa Waislamu wa jina, na mabunga wachache waandishi magazeti wapendao dunia wakaungana nao, na wakawa ndugu zao katika kulaani, kushutumu kukadhibisha na kutusi, na kwa harara sana wakaiaibisha Islam. Hapo ikawa nini! Wakristo wakapata nafasi nyingine zaidi. Basi, wakaanza kunengua kwa kejeli kuanzia Peshawar mpaka Ilahabad, na Bombay na Calcutta, na mpaka kufikia miji ya mbali sana wakaidhihaki dini ya Islam. Na Masheikh hao wote wenye sifa za Kiyahudi na waandishi magazeti walikuwa pamoja nao kwa furaha sana na kushikana mikono. Laana ya Mungu ilikuwa inawashukia kutoka mbinguni, lakini walikuwa hawaioni. Wakati huo walikuwa chini ya ghadhabu ya Mungu, lakini kwa sababu ya harara ya nafsi walikuwa kama vipofu. Hao wakati huo walikuwa wenye kusadikisha sauti ya shetani na

hawakuijali sauti ya mbinguni hata kidogo. Katika siku hizo mhariri mmoja Mwislamu bunga asiye na bahati akaandika kutoka Lahore ndani ya gazeti lake kwa kumwambia Atham na kwa kutaja jina langu kuwa, "Bwana Atham, utawafanyia hisani viumbe wa Mungu kama utamwadhibisha mtu huyu kwa kumshtaki mahakamani". Huyo mpumbavu kwa maneno yake hayo yenye hamaki alitaka kumwita mfu, lakini kwa vile alikuwa ameishakufa, kwa hiyo hakuweza kutikisika. Na Mwenyezi Mungu Anajua kuwa mimi mwenyewe nilikuwa nataka kuwa kama Atham hakula kiapo afadhali angefungua hata mashtaka. Lakini Atham alikuwa ni mfu. Heba ya bishara ya Mungu Aliye Hai ilikwisha mhilikisha. Japo kidhahiri alionekana yu hai, lakini hakuwa na uhai ndani yake. Mimi ninasema kweli kabisa kuwa kama watu hao wote wangemkata vipande vipande, hata hivyo yeye asingenishtaki mahakamani. Na kama ningempatia hata rupia milioni kumi, kamwe asingekula kiapo. Moyo wake ulikuwa uliishanikubali na ulimi ukakana. Nami najua sana kuwa kuhusu jambo hili kulikuwa hakuna mwingine aliyekuwa shahidi mkubwa wa ukweli wangu kuliko Atham. Ilmuradi, mapadri kwa kuficha ukweli kuhusu habari ya Atham wakaonyesha kebehi sana,

na kuanzia Amritsar wakarandaranda katika Panjab na miji mikubwa mikubwa ya India na kutoa miigo ya kubeza, na wakapiga makelele na vurugu kiasi kwamba tangu mwanzo wa utawala wa Kiingereza hadi leo haupatikani mfano wake. Na katika furaha hiyo ya uongo ambayo dhidi yake dhamiri zao zilikuwa zinawalaumu wakaonyesha mfano mbovu sana. Wakanitumia barua nyingi zilizojaa matusi machafu, wakapiga kelele na kufanya maringo kana kwamba wamebahatika kupata maelfu ya ushindi, na wakachapisha maelfu ya vipeperushi, lakini hata hivyo kwa harara hiyo yake maiti ya Atham haikuweza kutikisika. Na katika furaha ya ushindi huu wa uongo, yeye hakuweza kuchapisha hata kipeperushi cha kurasa mbili. Bali alichapisha ndani ya gazeti moja kuwa fitina zote hizi na makelele yaliyofanywa na Wakristo yamefanyika kinyume cha ridhaa yangu, mimi siafikiani nao. Na ingawa akaficha ushahidi wa kweli, lakini akakaa kimya pasipo kufanya uadui wala ujanja, hadi sawa na ufunuo wa Mungu akafa ndani ya miezi saba kuanzia tangazo letu la mwisho. Ilmuradi, hii ilikuwa ni fitina kubwa sana ambamo dini ya Kiislamu ilifanyiwa mzaha na ambamo Masheikh wenye bahati mbaya na Waislamu wengine majahili walijidhalilisha kwa kuungana

na mapadri, na wakaikadhibisha bishara ya ufunuo bila haki na wakaidhalilisha sana dini ya Kiislamu. Sasa someni uk. 242 wa *Barahine Ahmadiyya* kwa makini na fanyeni uadilifu kwamba kwa uwazi namna gani habari ya fitina hii imo humo, na namna gani imeandikwa wazi wazi kuwa kwanza Wakristo watafanya hila na kisha ukweli utadhihirika.

Fitina ya pili, iliyokuwa ya daraja la pili, ilikuwa fitina ya Muhammad Husain Batalawii kunikufurisha. Ndani yake pia kelele na vurugu za umma hazikuwa kidogo kuliko kelele za mapadri. Katika tukio la fitina hiyo wakufurishaji na wakadhibishaji karibu elfu saba au nane walikusanyika huko Delhi ndani ya Msikiti wa Ijumaa dhidi yangu. Kama usingekuwepo msaada wa Mungu, vurugu yenye hatari ingetokea. Ilmuradi, mwanzilishi wa fitina hii alikuwa Muhammad Husain Batalawii, na Nadhir Husain wa Delhi alikuwa pamoja naye ambaye kumhusu yeye Mwenyezi Mungu Alisema ndani ya ufunuo uliopo katika uk. 511 تَبَّتْ يَدَا اَبِيْ لَهَبٍ وَّتَبَّ۔ مَا كَانَ لَهٗ اَنْ يَّدْخُلَ فِيْهَا اِلَّا خَائِفًا. Yaani, mikono yote miwili ya Abu Lahab imeangamia iliyoandikia fatuwa ya kukufurisha, naye mwenyewe pia akaangamia. Haikumpasa kujiingiza ndani ya shauri hili isipokuwa kwa kuogopa. Fitina hii pia ilienea kuanzia Peshawar mpaka Calcutta,

Bombay, Haidarabad na miji yote ya Panjab na India. Na Waislamu majahili kama *maraafidhiin* wakaona ni thawabu kunilaani. Mahusiano baina ya Waislamu yakavunjika, ndugu akatengana na ndugu, na baba akajitenga na mwanaye. Kuamkiana kukakataliwa, hata kusalia sala ya maiti ya mmoja wa Jamaat yetu ikafahamika kuwa ni ukafiri.

Fitina ya tatu, iliyopo kwenye daraja la tatu, ni fitina ile iliyoletwa na Mabaniani sasa juu ya kifo cha Lekhram wakati wa dhihirisho la ishara ya wazi kabisa, na hao kadri ya uwezo wao wakaifikisha fitina hadi kilele chake. Wakapanga mipango ya kuniua na wanaendelea kupanga, wakaichochea serikali na wanaendelea kuchochea.[42] Kwa vile pamoja na fitina hii kuna ishara moja ya wazi wazi ambayo ilitetemesha mioyo ya wapinzani na ushindi adhimu umepatikana, na vipofu wengi wameanza kuona, kwa hiyo fitina hii iko kwenye daraja la tatu.

Hizo ni fitina tatu zilizoelezwa ndani ya *Barahine Ahmadiyya* miaka kumi na saba iliyopita tangu leo. Sasa kama Mwislamu au Mkristo au Baniani mwenye chuki sana akiwekewa mbele yake kitabu

---

[42] Tarehe 8 April 1897 kupitia Mkuu wa Polisi wa wilaya, nyumba yangu ilipekuliwa. Mwandishi.

hiki *Barahine Ahmadiyya* aonyeshwe hizi sehemu tatu za fitina, na aulizwe kwa kula kiapo kuwa je fitina hizi zote tatu zimeishatokea au hapana, na je, haya yaliandikwa ndani ya *Barahine Ahmadiyya* kama bishara au hapana, na je, matukio haya matatu yaliyodhihirika kwa nguvu sana hayaelezi na hayatoi ushahidi kwamba kwa kweli fitina moja ilitokea kwa Wakristo pia, ambamo mlikuwa na kelele na vurugu za malaki ya watu, na makundi kwa makundi kwa kujaa hamaki walikuwa wanapita masokoni, na kutoa miigo ya kubeza. Na fitina ya pili kwa kweli ilitoka kwa Muhammad Husain Batalawii ambaye aliwachochea vikali Waislamu dhidi yangu na akawatenganisha ndugu na ndugu, baba na watoto, marafiki na marafiki, na akaukatisha udugu. Na fitina ya tatu ilidhihirika kutoka kwa Mabaniani wakati wa mauti ya Lekhram na kwa sababu ya husuda ya kudhihiri ishara ya Mungu. Katika harara ya fitina hii watoto kadhaa wasio na hatia wakauawa. Mjini Rawalpindi karibu watu arobaini walipewa sumu, nami nikatishwa kuuawa, na juhudi za kuichokoza serikali zikafanywa, na haijulikani kuwa baadaye watafanya nini.[43] Sasa, hebu semeni kuwa je hii siyo kweli

[43] Tarehe 8 April 1897, nyumba yangu ilifanyiwa upekuzi. Mwandishi.

kuwa zile fitina tatu zimedhihiri kama zilivyokuwa zimeelezwa kwa uwazi na kwa kirefu hizo fitina tatu ndani ya *Barahine Ahmadiyya*? Je, Muhammad Husain wa Batala au Sayyid Ahmad Khan K. C. S. I, au Nazir Husain wa Delhi, au Abdul Jabbar wa Ghazni au Rashid Ahmad Gangohi, au Muhammad Bashir wa Bhopal, au Ghulam Dastagir wa Kusur, au Abdullah Tonki, Profesa wa Lahore, au Maulawii Muhammad Hasan Chifu wa Ludhiana wanaweza kula kiapo kuwa fitina hizo tatu zilizotajwa ndani ya *Barahine Ahmadiyya* zikiwa bishara hazikudhihirika? Kama mtu yeyote kati ya hao anaukataa ukweli wa ufunuo wangu, kwa nini anawaangamiza watu, ale kiapo dhidi yangu kuwa fitina zote tatu zilizotajwa ndani ya *Barahine Ahmadiyya* kama bishara, bishara hizo hazijatimia; na kama zimetimia, basi Ewe Mungu Mweza, katika siku arobaini na moja Ututeremshie adhabu ile iwateremkiayo wahalifu. Basi, isipoteremka katika siku arobaini na moja ile adhabu inayoteremka kutoka mbinguni kwa mkono wa Mungu na bila kupitia mtu, na inamwangamiza mwongo kama moto uteketezao, basi mimi nitakuwa mwongo na shughuli zangu zote zitakuwa za uongo, na kwa hakika mimi nitastahili kubeba laana zote. Na kama akionyesha katika zama hizi kutoka kwa

mtu mwingine bishara za aina hii ambazo mwenye kuzieleza mwenyewe aliishawatangazia wampingao na wamwafikio, kwa kupitia maandishi yake na vitabu vilivyochapishwa kabla ya wakati, nazo katika taadhima yake ziwe sawa na bishara zangu, ambamo nguvu za Mungu zionekane, hapo pia mimi nitakuwa mwongo. Na kwa ajili ya kiapo itakuwa lazima kwa yule mtu anayekubali kuapa kwamba aje Qadian na aape mbele yangu, mimi sitakwenda kwa yeyote yule. Hii ni kazi ya dini, hivyo wale watu pamoja na kujigamba kuwa Mashekhe wakizembea, basi hao wenyewe watathibitika kuwa waongo. Wakimshinda mtu kama mimi ambaye wanamtaja dajal basi kana kwamba wataiepusha dunia yote na maovu. Na wakati wa kula kiapo sharti hili litakuwa la lazima sana kuwa mimi kabla ya kiapo chao nitazieleza mbele yao hoja na dalili za bishara hizo kwa masaa mawili kamili katika mkutano wa hadhara wasije wakaangamia kwa kufanya haraka na pia ili hoja itimie kwao. Na hawatakuwa na haki ya kutamka neno hata moja mbali na kula kiapo. Watasikiliza maelezo yangu kwa masaa mawili wakiwa kimya kabisa. Kisha baada ya kula kiapo sawa na mfano ulioelezwa watakwenda majumbani mwao. Na ikumbukwe kuwa nimetia jina la Sayyid Ahmad

Khan miongoni mwa wakataaji kwa sababu hii kwamba yeye anaukataa ufunuo ule wa Mungu bali na hata wahyi pia unaoshuka kutoka kwa Mungu na unakuwa na adhama ya elemu ya ghaibu ndani yake. Kwa kuwa yeye pia sasa amefikia umri mrefu, mimi sipendi kwamba yeye kwa kufuata mawazo ya Ulaya kama kipofu aende kaburini na kosa hili. Sasa yeye ingawa asijali na alidhihaki jambo hili, lakini mimi nimeishafikisha niliyotakiwa kufikisha; naogopa isije nikaulizwa kwa nini sikumfikishia ujumbe mtu mmoja mpotovu.

Baadhi ya majahili wanasema kuwa kwa nini kila mara bishara za adhabu na kifo hutolewa. Wajinga hao hawajui kuwa kila Nabii alikuwa anatoa bishara za maonyo. Kama hii si sawa, basi ina maana gani kuwa wapinzani watakufa kwa pumzi ya Masihi Mau'udi.

Ilmuradi hawa ni watu tisa waliochaguliwa kwa ajili ya kuapa, kwani kila mmoja wao analo kundi la watu pamoja naye. Hivyo, kwa kufikia maamuzi pamoja naye, kimatokeo maamuzi ya kundi lake yatakuwa yamefikiwa yenyewe. Mada ya kiapo itakuwa ni hii hii kuwa bishara hizi hazikutimia, wala hazikutajwa ndani ya *Barahine Ahmadiyya* hapo kabla. Jambo

hili linatakiwa kukumbuka vizuri kuwa ingawa wakataaji kutokana na ujahili na upumbavu wao wanakadhibisha kila jambo na wanaichukulia kila bishara kuwa kinyume cha kweli, lakini ukadhibishaji wao ule uliozalika kwa sura ya fitina ya hatari sana na ukafikia hadi vurugu amabayo pamoja nayo ikatokea ghasia kubwa sana na yakatokea matokeo hatari, huo ukatokea mara tatu tu, na huo ukaitwa ndani ya *Barahine Ahmadiyya* kuwa fitina kubwa tatu. Na kitabu hiki yaani *Barahine Ahmadiyya* kimeshaenezwa nchini kote, bali hata katika nchi za Uarabuni na Uajemi miaka kumi na saba iliyopita toka leo. Na fitina hizi tatu jinsi zilivyodhihiri kwa nguvu na adhama na kwa kelele za kuogofya sana zilivyoenezwa hadi pembe zote za nchi hii, hili si jambo lililofichikana kwa yeyote. Bali wanaume kwa wanawake na Waislamu kwa Mabaniani wa Punjab na India wanazikumbuka fitina hizo kiasi hiki kwamba haitarajiwi kamwe kuwa kumbukumbu za fitina hizo tatu ziweze kufutika kwenye kurasa za historia. Basi, mtu yeyote baada ya kupata taarifa za matukio ya fitina hizi tatu ya kutisha akipenda kuangalia habari hizi ndani ya *Barahine Ahmadiyya* au kwa kusoma bishara za fitina hizi tatu ndani ya *Barahine Ahmadiyya* apende kuuangalia mfano wake katika matukio

yaliyotukia, basi katika hali zote hizi mbili atapata yakini kamili kuwa ndani ya *Barahine Ahmadiyya* zimetajwa fitina hizi hizi tatu zilizokwisha tokea, au useme hivi kuwa fitina zile tatu zilizoshuhudiwa kutokea ni zile zile tatu zilizoandikwa mapema ndani ya *Barahine Ahmadiyya*. Sasa fikirieni kuwa bishara iliyomhusu Atham ambayo waliipigia kelele Wakristo na Mashekhe wenye sifa za Kiyahudi, na bishara iliyomhusu Lekhram ambayo kuihusu hiyo Waariya walizusha tufani, hizo mbili zimeimarika juu ya mwamba gani madhubuti. Enyi kizazi cha Waislamu, msivuke mipaka kupita kiasi. Yumkini, mtu sawa na akili na ijtihadi yake aione rai moja kuwa ni sahihi, lakini kwa kweli rai hiyo iwe yenye makosa, na yawezekana kuwa amdhanie mtu fulani kuwa mwongo, lakini kwa kweli yu mkweli. Kabla yenu watu wengi walidanganyika. M kitu gani hata kwamba msidanganyike. Hivyo, ogopeni na chagueni njia ya ucha Mungu ili msiingie katika mtihani. Mimi ninasema mara kwa mara kuwa kama kitendo hiki kingekuwa cha mwanadamu, kingeishaangamizwa kitambo, na kabla ya mikono yenu kuinuka, Mkono wa Mungu Ungekiangamiza. Angalieni, Mungu Anasema:

فَلَا يُظْهِرُ عَلٰى غَيْبِهٖٓ اَحَدًا ۙ اِلَّا مَنِ ارْتَضٰى مِنْ رَّسُوْلٍ[44]

Yaani, elimu ya ghaibu haidhihirishwi ila kwa mitume waliochaguliwa. Sasa fikirieni na kwa makini sana msome kitabu hiki kuwa je ghaibu ile iliyoelezwa ndani ya aya hii haikuelezwa kikamilifu? Mimi nawaambieni kweli kweli kuwa kile mlichoonyeshwa ninyi, kama wangeonyeshwa vipofu wale waliopita kabla ya karne hii, hao wasingebaki kuwa vipofu. Sasa baada ya kuupata mwanga, msiukatae. Mungu Yuko tayari kuwapeni macho yenye nuru na Yuko tayari kuwajalieni mioyo iliyotakasika. Yeye kwa namna mpya Anataka kujidhihirisha kwenu. Amenyoosha Mikono yake kutengeneza mbingu mpya na ardhi mpya, kwa hiyo msilete vizuizi na inameni upesi kwa wema. Msijidhulumu nafsi zenu wala msiwe maadui wa dhuria zenu ili Mungu Awahurumieni, na ili Yeye Asamehe dhambi zenu na Azitilie baraka siku zenu. Hebu angalieni, mbingu yafanya nini, na namna Mungu Anavyoivuta ardhi? Ni masikitiko kuwa nyinyi mmesahau hata mwanzo wa karne.

**Bishara ya kumi na tano** inayofanana sana na bishara ya Atham na bishara ya Lekhram ni ufunuo ule uliochapishwa baada ya kupita muda wa Atham ndani ya kijitabu *Anwaarul Islam*, nao ni huu:

---

[44] Sura Al-Jinn, 72:27-28

اِطَّلَعَ اللهُ عَلٰى هَمِّهٖ وَ غَمِّهٖ وَلَنْ تَجِدَ لِسُنَّةِ اللهِ تَبْدِيْلًا ۔ وَلَا تَعْجَبُوْا وَلَا تَحْزَنُوْا
وَ اَنْتُمُ الْاَعْلَوْنَ اِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِيْنَ ۔ وَبِعِزَّتِيْ وَ جَلَالِيْ اِنَّكَ اَنْتَ الْاَعْلٰى ۔
وَ نُمَزِّقُ الْاَعْدَاءَ كُلَّ مُمَزَّقٍ ۔ اِنَّا نَكْشِفُ السِّرَّ عَنْ سَاقِهٖ ۔ يَوْمَئِذٍ يَّفْرَحُ
الْمُؤْمِنُوْنَ ۔ ثُلَّةٌ مِّنَ الْاَوَّلِيْنَ وَ ثُلَّةٌ مِّنَ الْاٰخِرِيْنَ ۔ هٰذِهٖ تَذْكِرَةٌ فَمَنْ شَاءَ
اتَّخَذَ اِلٰى رَبِّهٖ سَبِيْلًا ۔

Yaani, Mungu Aliona kuwa moyo wa Atham umejaa huzuni na majonzi. Nawe hutakuta mabadiliko ndani ya suna ya Mungu. Yaani, Yeye kwa ajili ya moyo unaoogopa Anaiahirisha bishara ya adhabu, hiyo ndiyo suna Yake. Na tena Akasema kuwa tukio lililotokea usilionee ajabu, na kama mtakuwa imara juu ya imani, hatimaye ushindi utakuwa wenu. Na Ninaapa kwa Heshima na Jalali Yangu, kuwa wewe ndiwe utakayekuwa mshindi mwishoni. Nasi Tutawafanya maadui vipande vipande. Tutayaonyesha kwa uwazi mambo yaliyofichikana ya bishara ya ufunuo. Siku hiyo, waaminio watafurahi, kundi la kwanza pia na kundi la nyuma vilevile. Huu ni ukumbusho kutoka kwa Mungu, basi atakaye na akubali. Sasa, angalieni kuwa bishara hii ni ya zaidi ya miaka mitatu, yaani ni ya wakati ule ilipokuwa siku ya mwisho ya muda wa Atham. Ndani yake mlikuwa na ahadi ya Mwenyezi Mungu kuwa athari hii ya bishara inayowatilia wapumbavu mashakani, Tutaidhihirisha kwa uwazi. Hivyo,

baada ya ishara kuhusu Lekhram, sawa na ahadi Yake, Akaliweka wazi jambo hilo lililofichikana, na Akaziweka mbele bishara za *Barahine Ahmadiyya* mfano wa kioo. Hivyo, hii ni fadhili Yake juu ya zama hizi kwamba Alifungua chemchemi ya maarifa mapya. Amebarikiwa yule aichukuaye hisa kutoka ndani yake. Na Aliposema kuwa wakati ule kundi la kwanza pia litafurahi na kundi la nyuma vilevile, bishara zote hizi zimetimia wakati huu. Hivyo, kwa kudhihiri ishara ya Lekhram nguvu za imani za waaminio zikaongezeka na wakapata furaha ile ambayo ni vigumu kukadiria. Maelfu ya waaminio walijawa na jazba na kwa harara ya maono ilionekana kupitia machozi ya furaha, kana kwamba walimwona Mungu Aliyefichika kwa macho yao. Tukio hili la ajabu limetokea kwamba Mabaniani na Waariya walilia kwa ajili ya huzuni ya Lekhram, na kundi la waaminio na wakweli lililia kwa furaha ya kuongezeka maarifa. Ndani ya uk. 242 wa *Barahine Ahmadiyya* mna funuo zifuatazo zilizokuwa ni bishara, nikaiona mimi ikitimia kikamilifu baada ya ishara hiyo hiyo, nayo ni hii:

اَصْحَابُ الصُّفَّةِ ۔ وَمَا اَدْرٰكَ مَا اَصْحَابُ الصُّفَّةِ ۔ تَرٰی اَعْيُنَهُمْ تَفِيْضُ مِنَ الدَّمْعِ يُصَلُّوْنَ عَلَيْكَ ۔ رَبَّنَا اِنَّنَا سَمِعْنَا مُنَادِيًا يُّنَادِیْ لِلْاِيْمَانِ وَ دَاعِيًا اِلَى اللّٰهِ وَ سِرَاجًا مُّنِيْرًا ۔ اَمْلُوْا ۔

Tafsiri: Wakaaji wa chumba, nawe unajuaje wakaaji

wa chumba ni nani! Utaona machozi yanatiririka kutoka machoni mwao. Watakusalia. Ee Mungu Wetu, sisi tulimsikia mwitaji mmoja ambaye anatangaza Jina Lako na kuwaita watu kwenye imani, na kuwakaribisha kwa Mungu Mmoja Asiye na mshirika, na ni siraji moja imulikayo. Andikeni. Na ndani ya bishara ya *Anwarul Islam* iliyotajwa juu imeandikwa pia wazi wazi kuwa baada ya ishara hii, kundi lingine pia litaungana na Jamaat hii na makundi hayo mawili yataifurahia ishara hiyo. Basi, bishara hiyo sasa inatimia. Na barua nyingi za wapinzani wengi za unyenyekevu zinafululiza kuja kuwa sisi tulikuwa na makosa. فَالْحَمْدُ لِلّٰهِ عَلٰى ذٰلِكَ

**Bishara ya kumi na sita:** Kwenye uk. 227 wa *Barahine Ahmadiyya* kuna bishara moja kumhusu Mwaria mmoja, jina lake ni Malawa Mal, yeye mpaka sasa yuko hai. Mtu huyu alipata kuugua ugonjwa wa kifua kikuu. Siku moja alikuja kwangu akiwa amekata tamaa na maisha, akalia sana kwa uchungu mkubwa. Mimi ninakumbuka kuwa siku hiyo alikuwa ameota ndoto ya kutisha pia. Ninavyokumbuka ndoto ilikuwa hivi kuwa nyoka mwenye sumu amemwuma, na sumu imepenya mwili mzima. Ndoto hii ilikuwa imemhuzunisha sana. Na hapo kabla, homa nyepesi iliyokuwa inazidi baada ya kula chakula ilikuwa

imemtia wasiwasi mkubwa. Hivyo, yeye alikuwa katika hali ya kukosa utulivu na karibu kukata tamaa. Yeye alinijia na akalia. Ndipo moyo wangu ukalainika juu ya hali yake nami nikamwomba Mungu Aliye Mmoja kwa ajili ya Mwaria huyo, kama nilivyokuwa nimemwombea yule Mwaria wa awali, jina lake Sharampat. Ndipo nikafunuliwa ufunuo huu uliomo ndani ya *Barahine Ahmadiyya*, Uk. 227 قُلْنَا يَا نَارُ كُوْنِيْ بَرْدًا وَّ سَلَامًا Yaani, Sisi Tukauambia moto wa homa, "Uwe baridi na salama". Basi, papo hapo yeye aliyekuwepo akapewa habari ya ufunuo huu, na watu wengine wengi pia wakaambiwa, kuwa huyo lazima atapona kutokana na baraka ya maombi yangu. Basi, hata wiki moja ilikuwa haijapita ambapo Mwaria huyo kwa fadhili ya Allah akapona. Ingawa hali ya sasa ya Waaria ndiyo hii kwamba kutoa ushahidi wa kweli ni mbaya zaidi kwao kuliko mauti. Lakini mimi kwa kula kiapo cha Mwenyezi Mungu ninasema kuwa tukio hili ni la kweli kabisa na ndani yake hamkutiwa chumvi hata kidogo. Endapo ningekuwa na shaka juu ya sehemu yoyote ya madhumuni ya matukio haya, mimi kamwe nisingeyaandika matukio haya. Na kutia chumvi na kuongezea maneno ni kazi ya watu waliolaaniwa. Na matukio yote hayo mawili ya Sharampat na Malawamal yameishaandikwa ndani

ya *Barahine Ahmadiyya* tangu miaka kumi na saba iliyopita. Hivyo basi, wale watu wanaokuwa na shaka kwa nini funuo huwa za madhara tu kwa wapinzani, hao wafikirie juu ya funuo hizi mbili, kwani hao wote wawili ni Waaria. Kazi yetu ni kuwahurumia viumbe wote. Hebu Waaria wenyewe watoe mfano wowote kama wao wamefanya huruma ya aina hii kwa Mwislamu yeyote. Mimi ninasema kweli kabisa kuwa kuwahurumia viumbe wa Mungu kwa upendo wa kweli haiyumkiniki kwa yeyote ila Mwislamu wa kweli. Naam, inawezekana kwa kuonwa tu na watu, lakini wengine hawawezi kuwa na mambo hayo kwa moyo safi mkunjufu sawa sawa na mafunzo. Waislamu wanapenda ukarimu kiasili, ndiyo maana hata katika kula na kunywa pia hawatengani na Mabaniani. Lakini ndani ya Mabaniani chuki pia ni alama ya ubahili. Naam, ghadhabu ya Mungu kumwangukia mwasi hata akiwa Mwislamu au Mkristo au Baniani, ni jambo jingine; hilo halihusiani na kanuni ya huruma.

Na nilipoapa wakati wa kueleza matukio ya Waaria hao wawili, sababu yake ni kuwa mimi sina yakini kuwa hao hawatakuwa tayari kuficha ukweli kwa uchache kiasi hiki kwamba wanitungie tuhuma kuwa huyu akapunguza na kuongeza katika matukio

sahihi. Na pia nimekula kiapo kwa sababu siku hizi Waaria wanayo bughuda makhsusi na Uislamu.

Na mimi mara ya pili tena nikiapa kwa Mungu Mwenye shani ninasema kuwa hakuna tofauti yoyote hata sawa na chembe ndani ya kueleza matukio haya. Mungu Yupo, na Anaujua sana uongo wa mwongo. Kama nimeongopa au nimepunguza au kuzidisha matukio haya hata sawa na chembe, basi yamlazimu sana mwenye kudhania hivi kuwa achapishe tangazo kwa kiapo cha Mungu kuwa mimi najua kuwa mtu huyu amesema uongo, au amepunguza na kuzidisha. Na kama hakufanya, basi adhabu ya kukadhibisha inishukie mimi ndani ya mwaka mmoja. Nami pia sasa hivi nimeishakula kiapo. Hivyo, kama nitakuwa mwongo, au nitakuwa nimepunguza au kuzidisha habari hizo, basi adhabu ya uongo na uzushi huu itabidi kunipata. Lakini, kama nimeandika kwa uaminifu kamili — na Mwenyezi Mungu Anajua kuwa mimi niliandika kwa uaminifu kamili — basi Mungu Hatamwacha mkadhibishaji bila kumwadhibu. Fahamuni kwa yakini kuwa Mungu Yupo, na daima Yeye Huusaidia ukweli. Kama mtu ainuke kwa kutahini, basi ndiyo shabaha yangu hasa, kwani kwa mtihani Mungu Atatoa uamuzi baina yetu na wapinzani wetu. Hii ni fursa nzuri pia kwa

Masheikh wapinzani wetu kwamba wawahamasishe watu kama walivyojaribu kumhamasisha Atham. Kutolewa kwa maamuzi kutaleta baraka kwa kila mmoja, hivyo dunia itajua kuwa Mungu Yupo na Anapokea dua za wakweli. Dayanand na mwanafunzi wake Lekhram wameondoka dunia hii, lakini wameuacha nyuma uvundo wa udaharia, ubahili na chuki. Na mimi nataka uvundo huo uondolewe mbali, kwa hiyo mimi nataka maamuzi yafanywe baina ya Mwaria huyu pia kwa njia ya kiapo kama alivyoombwa Mwaria wa awali. Nami najua kwa yakini, bali ninaona kwa macho, kuwa Mungu Yu Msaidizi wa ukweli, na Yu Adui wa mpinzani wa ukweli. Kutoa ushahidi wa jambo la kweli si vigumu kwa mtu mwaminifu, lakini siku hizi ni vigumu sana kwa Waaria. Ilmuradi, kama kuna mkadhibishaji, akiwa Mwaria huyu au Mwaria yule, basi kwa kula kiapo afanye maamuzi nami. Mimi ninajua kuwa Mungu Yule Ambaye ni Mungu wetu ni moto unaoangamiza, Yeye kamwe Hatamwacha mwongo. Lakini mtu akiwa mkweli, basi hapati hasara. Sasa, angalieni, huu ndio unaoitwa uthibitisho kwamba ukweli wa bishara hii yenye baraka kuhusikana na wapinzani wa dini umedhihirishwa. Kutakuwa na ithibati gani duniani zaidi ya hii kuwa maadui wa

aina hii wa dini kama walivyo Waaria wa siku hizi wawe mashahidi wa ukweli wa bishara za Mungu. Je, ushahidi wa namna hii na ishara zilizopo za aina hii wanazo Wakristo pia? Kama zipo, basi itoeni angalau moja kwa mfano. Hivyo, eleweni kwa yakini kuwa Mungu Mkweli ni Mungu Yule tu Ambaye Kurani Tukufu inaita Kwake. Mengine yote kinyume chake ni kumwabudu binadamu au kuyaabudu mawe. Hakuna shaka kuwa Masihi bin Mariamu pia amekunywa maji kutoka ndani ya chemchemi hii tunamokunywa sisi. Na bila shaka yeye pia amekula katika tunda lile ambamo tunakula sisi, lakini mambo haya yana uhusiano gani na uungu na yanahusikaje na utoto wa Mungu? Wakristo wamebuni njia ya ajabu ya kumwunda mungu aliyebanwa, yaani laana, kama haipo laana, basi uungu ni bure, na utoto wa Mungu ni upuuzi tu. Lakini kwa mwafaka wa wataalamu wote wa lugha, maana ya maluuni ni mtu ambaye moyo wake uwepo mbali na Mungu, akose imani na kuritadi, awe adui wa Mungu, awe mwenye moyo mweusi awe mbaya zaidi kuliko mbwa, nguruwe na nyani kama Torati pia inavyotoa ushahidi. Je, hata kwa sekunde moja maana hii inaweza kukubaliwa kwa ajili ya Masihi ? Je, yeye aliwahi kufikiwa na zama ambapo akawa si mpendwa wa Mungu? Je, aliwahi kufikiwa

na wakati ambapo hakubaki kuwa mpendwa wa Mungu? Je alifikiwa na wakati ambapo moyo wake ulimkataa Mungu? Je, aliwahi kukusudia kuachana na imani? Je, iliwahi kutokea kuwa yeye alikuwa adui wa Mungu na Mungu Alikuwa adui yake? Basi, kama haikuwa hivyo, yeye alipata sehemu gani katika laana ambayo wokovu wote uliitegemea? Je, Torati haitoi ushahidi kuwa asulubishwaye ni mlaaniwa? Basi, kama anayesulubishwa huwa mlaaniwa, bila shaka laana ile inayokuwa kama kawaida matokeo ya kusulubiwa, huenda ikamwangukia Masihi. Lakini, muradi wa laana kama inavyokubaliwa duniani ni kuwa mbali na Mungu na kumwasi. Laana siyo kupatwa na msiba, bali laana ni kuwa mbali na Mungu, na kumchukia Mungu na uadui kwa Mungu. Na kulingana na kamusi mlaaniwa ni jina la shetani. Sasa fikirini kwa ajili ya Mungu kuwa je yapasa kuwa mkweli mmoja achukuliwe kuwa adui wa Mungu na mwasi wa Mungu, bali aitwe jina shetani, na Mungu Akubaliwe kuwa Adui wake? Ingekuwa bora kuwa Wakristo wangekubali kuingia jahanamu, lakini wasingemfanya yule mtu mteule kuwa mlaaniwa na shetani. Ulaaniwe ule wokovu usioweza kupatikana bila ya kuwakubali wakweli kuwa mashetani, wasio na imani. Kurani Tukufu imedhihirisha vizuri sana

ukweli kuwa ikamwepusha Yesu na uchafu wa laana kwa kumwokoa katika kifo cha msalaba. Na Injili pia inatoa ushahidi huu huu, kwani Yesu alijifananisha na Yona. Na hakuna Mkristo yeyote asiyejua kuwa Yona hakufa ndani ya tumbo la nyangumi. Na kama Yesu alikuwa mfu kaburini, sasa mfu ana uwiano gani na aliye hai? Na aliye hai na mfu wanafananaje? Kisha hili pia linajulikana kuwa Yesu baada ya kuokoka kutoka msalabani akawaonyesha wanafunzi wake majeraha yake. Basi, kama alipatiwa maisha ya pili kijalali kwa nini majeraha ya maisha yake ya kwanza yakabaki? Je, kulibakia kasoro kidogo ndani ya nguvu ya kijalali? Na kama kasoro ilibaki, basi itarajiweje kuwa majeraha haya yataweza kupona hadi Siku ya Kiama. Hivi ni visa visivyo na maana vilivyowekewa boriti ya Uungu. Lakini waja wakati bali umeshawadia kuwa kama vile pamba inavyochambuliwa, vivyo hivyo Mwenyezi Mungu Atakavyovifanya visa vyote hivi kuwa chembe chembe na kupoteza heweni. Ni masikitiko kuwa watu hawa hawafikiri kuwa huyu alikuwa mungu wa namna gani ambaye majeraha yake yalihitaji kutengenezewa marhamu. Mmeshasikia kuwa vitabu vya zamani vya tiba vilivyomo katika kumbukumbu za Wakristo, Warumi, Wayahudi na vya Majusi

ambavyo vipo mpaka sasa, vinatoa ushahidi kuwa kwa ajili ya majeraha ya Yesu marhamu yalitengenezwa yanayoitwa jina Marhamu ya Isa ambayo mpaka sasa imo ndani ya vitabu vinavyoorodhesha madawa. Haiwezi kusemwa kuwa marhamu hayo yalitengenezwa labda kabla ya zama za unabii wake, kwani marhamu haya yalitayarishwa na wanafunzi wake na kabla ya unabii wanafunzi walikuwa wapi? Haiwezi kusemwa kamwe kuwa kulikuwa na sababu nyingine fulani ya kupata majeraha siyo msalaba, maana katika miaka mitatu ya unabii hakuna tukio lolote la aina hii linaloweza kuthibitika isipokuwa tu tukio la msalaba. Na kama kuna dai la namna hiyo, basi jukumu la kuleta thibitisho ni juu ya mdai. Ni jambo la aibu: mungu huyu, majeraha haya na marhamu haya! Na nani awezaye kuficha hakika zilizo sahihi kabisa na za kweli? Na ni nani anayeweza kupigana vita na Mungu? Kwa kudumu Mzima na Mhifadhi wa milele ni Mungu tu huyu wa pekee Ambaye Ameepukana na umbo na eneo. Hana mwanzo wala mwisho. Na kwa mungu mwongo yatosha tu kuwa yeye kwa miaka 1900 alitumikisha sarafu za bandia za uungu wake. Kumbukeni, uungu huu wa uongo utaisha haraka sana. Siku zinawadia ambapo watoto wenye bahati njema wa Wakristo

watamtambua Mungu wa kweli, na walioachana zamani watakuja kuungana na Mungu Mmoja Asiye na mshirika huku wakilia. Haya siyasemi mimi bali roho inasema iliyomo ndani mwangu. Kadri mtu anavyoweza kupigana na ukweli na apigane, kadri anavyotaka kufanya hila na afanye bila shaka lakini mwishoni itakuwa hivyo tu. Ni rahisi zigeuke ardhi na mbingu, ni rahisi milima iondoke mahali pake, lakini ahadi hizi haziwezi kubadilishwa.

**Bishara ya kumi na saba**: Bishara hii ni ile iliyoandikwa kwenye uk. 239 wa *Barahine Ahmadiyya*. Nayo ni hii: يُتِمُّ نِعۡمَتَهُ عَلَيۡكَ لِيَكُوۡنَ آيَةً لِّلۡمُؤۡمِنِيۡنَ Yaani, Mungu Atatimiza neema Zake juu yako ili ziwe ishara kwa ajili ya waaminio. Yaani, neema zozote utakazopewa katika maisha ya dunia, zote hizo zitakuwa ni kama ishara. Yaani kauli pia takuwa ni ishara, kama vile watu walivyoona katika mkutano wa dini mjini Lahore na ndani ya vitabu vya Kiarabu. Na kitendo pia kitakuwa ni ishara, jinsi vitendo vya Mungu vinavyodhihirika kama ishara kwa kunipitia mimi. Na watoto pia watakuwa ni ishara, kama Mungu Alivyotoa ahadi ya wazao wema na wenye baraka, na Akatimiza. Na msaada wa mali wa Mungu pia utakuwa ni ishara kama vile Mungu Alivyotoa ahadi ya msaada wa mali ndani ya *Barahine Ahmadiyya*.

Na ahadi hiyo sasa imetimia, na watu walikuja toka mashariki na magharibi, na wasaidizi wameibuka kutoka mashariki na magharibi. Na kama alivyosema kwenye uk. 241 يَنۡصُرُكَ رِجَالٌ نُوۡحِيۡ اِلَيۡهِمۡ مِنَ السَّمَاءِ يَأۡتُوۡنَ مِنۡ كُلِّ فَجٍّ عَمِيۡقٍ, yaani, watu wale watakusaidia Tutakaowatilia mioyoni mwao, nao watakujia kutoka maeneo ya mbali sana kwa njia zenye mashimo. Bishara hii sasa imedhihirika iliyoandikwa miaka 17 kutoka siku ya leo. Nani alijua kuwa watu watashughulika kutoa msaada kwa uaminifu wa kweli na mapenzi ya namna hii. Hebu, angalieni, upo wapi mji wa Madras na upo mbali kiasi gani ambapo kutoka hapo matakwa ya Mwenyezi Mungu yalimleta kwangu Seth Abdur Rahman Haji Allah Rakha pamoja na jamaa na marafiki zake wote ambao baada ya kuja wakazidi katika ikhlasi na huduma kiasi hiki kwamba wakawa na mapenzi kama ya masahaba. Na mji wa Bombay upo wapi ambamo akatayarishwa mwaminifu na mwenye jazba kama Munshi Zainuddin Ibrahim. Na upo wapi Haidarabad Deccan ambamo Jamaat moja yenye jazba na ikhlasi ikatayarishwa. Je, haya si yale mambo yaliyoelezwa kabla ndani ya *Barahine Ahmadiyya*?

**Bishara ya kumi na nane:** Hii ndiyo ile bishara iliyoandikwa kwenye uk. 240 wa *Barahine*

*Ahmadiyya*, yaani hii:

قُلۡ عِنۡدِیۡ شَهَادَةٌ مِّنَ اللّٰهِ فَهَلۡ اَنۡتُمۡ مُؤۡمِنُوۡنَ۔
قُلۡ عِنۡدِیۡ شَهَادَةٌ مِّنَ اللّٰهِ فَهَلۡ اَنۡتُمۡ مُسۡلِمُوۡنَ

Yaani, sema, ninao ushahidi mmoja wa Mungu, je mtauamini? Sema, ninao ushahidi mmoja wa Mungu, je mtaukubali? Sentensi hizi mbili ni kama utabiri, na zinaashiria kwenye ishara za kimbingu ambazo ni kama matabiri, kwani ushahidi wa Mungu huonyesha ishara. Hivyo, baada yake ushahidi huu ukatolewa kuwa mwezi na jua vilipatwa ndani ya mwezi wa Ramadhani kama vile ndani ya Hadithi iliyokuwa imetajwa miongoni mwa alama za Mahdi Mau'udi. Kisha Mungu Alitoa ushahidi wa pili kuwa katika bishara ya Atham Wakristo walifanya hila kwa kuyaficha matukio na Masheikh wenye sifa za Kiyahudi wakaafikiana nao. Na hiyo ilikuwa ni sauti ya kishetani waliyotoa mashetani wa ardhini, yaani masheikh kwa kuwasaidia Wakristo. Kisha baada ya kuficha ushahidi, Mungu Akamwangamiza Atham. Na kwa kuisadikisha bishara hiyo Akadhihirisha ishara kuhusu Lekhram, na hii ilikuwa ni sauti ya kimbingu iliyoifutilia mbali sauti ya kishetani. Haya ndiyo yaliyokuwa yameandikwa ndani ya Hadithi za Mtume[saw] hapo kabla ambayo yakatimia ndani ya

bishara kumhusu Atham. Ushahidi wa tatu wa Mungu ni ile bishara iliyotangazwa kabla ya Mkutano wa Dini. Ushahidi wa nne wa Mungu ulikuwa ni ishara ya kuuawa kwa Lekhram iliyovunja mgongo wa wapinzani. Bishara hii ilielezwa na kuenezwa pamoja na masharti na maelezo ambayo mtu mwenye busara hataweza kuamini kuwa kuyatimiza hayo yanaweza kuwa katika hiari ya binadamu. Kwani, ndani yake muda ulitajwa siku ilitajwa[45] tarehe ilibainishwa,

---

[45] Inathibitika kutokana na Kutoka, mlango 32 kuwa ilinuiwa kuangamiza ndama ya Samiri siku ya idi ya Wayahudi, lakini kuichoma motoni na kuisaga tikitiki na kuifanya mfano wa vumbi kama ilivyoandikwa katika kutoka 32:20, kazi hii ilihitaji fursa. Bila shaka kazi hiyo mbovu iliendelea sehemu fulani ya usiku, maana Hadhrat Musa alishuka wakati ule ambapo sherehe ya kuiabudu ndama ilikuwa imepamba moto, na kipindi hicho aghalabu kilikuwa ni baada ya saa sita. Kisha muda fulani ukapita katika hali ya ghadhabu na hasira. Hivyo, ni jambo la uhakika kuwa kuichoma dhahabu na kuifanya kama mavumbi kungalikuwa kumefikia tamati mpaka sehemu fulani ya usiku inayohesabiwa siku ya pili. Hivyo, Mwenyezi Mungu Alimwita Lekhram kuwa ndama ya Samiri. Ndani ya jina hili siri hii ilikuwa imefichika kuwa yeye atapata kuangamia siku ya pili ya idi kama ilivyokuwa kwa ndama ya Samiri. Na kwa kuwa mara nyingi ndama anachinjwa na kisu, kwa hiyo katika neno *'ijl* – ndama – lililotumika katika ufunuo njia hii ya kifo imefichika. Na bishara kuhusu kifo cha Lekhram kuwa yeye atauawa siku ya pili ya Idi, kuna ule ufunuo wa Mungu ulioandikwa kwenye uk., 54 wa kitabu *Karaamaatus Saadikiin,* yaani سَتَعْرِفُ يَوْمَ الْعِيْدِ وَالْعِيْدُ اَقْرَبُ Ubeti wa kabla yake ni huu: اَلَا اِنَّنِیْ فِیْ کُلِّ حَرْبٍ غَالِبٌ فَکِدْنِیْ بِمَا زَوَّرْتَ فَالْحَقُّ یَغْلِبُ Yaani, mimi katika kila vita ni mshindi, hivyo ufanye hila utakavyo kwa kupamba uongo, lakini ukweli utapata kushinda. Na katika ubeti wa pili mmetolewa maelezo ya ubeti huu kuwa ukweli utashindaje.

Nao ndio huu:

وَبَشَّرَنِيْ رَبِّيْ وَقَالَ مُبَشِّرًا   سَتَعْرِفُ يَوْمَ الْعِيْدُ وَالْعِيْدُ اَقْرَبُ

Yaani, Mola wangu Amenipa bishara, na akiishanipa bishara Akasema kuwa wewe karibuni utaitambua siku ya Idi, yaani siku ya furaha, na Idi ya kawaida itakuwa karibu sana na siku hiyo. Yaani hiyo itakuwa ni siku ya ushindi wa haki. Hivyo, hiyo itakuwa ni Idi ya waaminio, na siku ya Idi ya kawaida itakuwa imeambatana nayo. Na maelezo ya ubeti huo yameandikwa kwenye jalada la kitabu hiki '*Karaamaatus-Saadikiin*' kwenye ukurasa wa mwisho, na neno hili hili وَبَشَّرَنِيْ رَبِّيْ lililo mwanzoni mwa ubeti huu pia lipo hapo nao ndio huu: وَبَشَّرَنِيْ رَبِّيْ بِمَوْتِهٖ فِيْ سِتٍّ سَنَةٍ اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيَةً لِّلطَّالِبِيْنَ. Yaani, Mwenyezi Mungu Amenipa bishara kuwa Lekhram atakufa katika muda wa miaka sita. Na beti zile zinaashiria kwa bishara hii hii ambazo zimo ndani ya kasida katika *Anjame Atham* iliyoandikwa mnamo mwezi Septemba 1896 kwa kumwambia Sheikh Muhammad Husain Batalawii. Na kama vile neno *Ta'rifu* linavyopatikana ndani ya ubeti wa سَتَعْرِفُ يَوْمَ الْعِيْدِ , ndani ya kasida hii pia lipo *Sata'rifu* kwa kumwambia Muhammad Husain. Na kama vile kasida ile ambamo kuna ufunuo huu yaani سَتَعْرِفُ يَوْمَ الْعِيْدِ وَالْعِيْدُ اَقْرَبُ ni kwa ajili ya Muhammad Hussein na iliandikwa kwa kumwambia yeye, vivyo hivyo ndani ya kasida hii pia Muhammad Husain Batalawii ndiye anayeambiwa. Na beti zenyewe ni hizi:

تُبْ اَيُّهَا الْغَالِيْ وَتَأْتِيْ سَاعَةٌ   تُمْسِيْ تَعَضُّ يَمِيْنَكَ الشَّلَّاءِ

Tubu, ewe mpita kiasi, kwani wakati unawadia kuwa utapita ukiuma mkono wako uliopooza.

تَأْتِيْكَ اٰيَاتِيْ فَتَعْرِفُ وَجْهَهَا   فَاصْبِرْ وَلَا تَتْرُكْ طَرِيْقَ حَيَاءٍ

Ishara zangu zitakufikia nawe utazitambua. Hivyo, fanya subira, na usiiache njia ya haya.

اِنِّيْ لَشَرُّ النَّاسِ اِنْ لَّمْ يَأْتِنِيْ   نَصْرٌ مِّنَ الرَّحْمٰنِ لِاِعْلَاءِ

wakati uliainishwa na njia ya mauti ilielezwa, yaani yeye atakufaje, kwa kuugua au kwa kuuawa. Na ishara za bishara zinadhihirisha hii pia kwamba wale watu waliofikisha sifa ya huyu ndama hadi kumwabudu na wakaubatilisha ukweli, na wakamsifu kupita kiasi hao pia mbele ya Mwenyezi Mungu ni kama taifa lile lililomwabudu ndama wa Samiri. Mwenyezi Mungu ndani ya sura Al-A'raaf Anasema:

إِنَّ الَّذِيْنَ اتَّخَذُوا الْعِجْلَ سَيَنَالُهُمْ غَضَبٌ مِّنْ رَّبِّهِمْ وَذِلَّةٌ فِي الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا
وَكَذٰلِكَ نَجْزِي الْمُفْتَرِيْنَ[46]

Yaani, wale waliomwabudu ndama watashukiwa na adhabu ya ghadhabu ya Mungu nao watafikiwa

---

Nitakuwa mbaya kuliko watu wote usiponifikia msaada wa Mungu kwa kuninyanua.

هَلْ تَطْمَعُ الدُّنْيَا مَذَلَّتَ صَادِقٍ هَيْهَاتَ ذَاكَ تَخَيُّلُ السُّفَهَاءِ

Je, dunia inatamani kwamba mkweli atadhalilika? Hili layumkinikaje, bali haya ni mawazo ya watu wapumbavu.

مَنْ ذَا الَّذِيْ يُخْزِيْ عَزِيْزَ جَنَابِهِ اَلْاَرْضُ لَا تُفْنِيْ شُمُوْسَ سَمَاءِ

Ni nani anayeweza kumdhalilisha mpendwa wa Mungu! Je ardhi inao uwezo wa kuliangamiza jua la mbingu?

يَا رَبَّنَا افْتَحْ بَيْنَنَا بِكَرَامَةٍ يَا مَنْ يَّرٰى قَلْبِيْ وَلُبَّ لِحَائِيْ

Ewe Mola wetu, Ufanye uamuzi kati yetu kwa kuonyesha karama, Ewe Yule Mungu Mwenye kuufahamu moyo wangu na kiini cha dhati yangu. Mwandishi.

[46] Sura Al-A'raaf, 7:153

na dhilla katika maisha ya duniani, na vivyo hivyo Sisi Tutawaadhibu watungao uongo. Na hii ni ishara nyepesi kwa wale waabuduo ndama pia ambao katika ibada ya ndama huyu wa pili yaani Lekhram walifikia nia za dhuluma na umwagaji damu. Hakuna kitu kilichofichikana na elimu ya Mwenyezi Mungu. Yeye Alijua sana kuwa Mabaniani pia kwa kumwabudu Lekhram watamfanya ndama. Ndiyo maana Yeye kwa neno 'kadhalika' Akaashiria kwenye kisa cha Lekhram. Kutokana na Torati, mlango wa 32 wa Kutoka aya 35 inathibitika kuwa Mwenyezi Mungu Aliwatumia mauti wana wa Israeli kwa sababu ya kumwabudu ndama. Yaani ugonjwa wa kuambukiza ukazuka kati yao uliowaua. Na wakati wa kutoa habari ya adhabu hii, Mwenyezi Mungu Alisema hii pia kuwa wale watakaoamini, Mimi Nitawaokoa, kama Anavyosema:

وَالَّذِينَ عَمِلُوا السَّيِّئَاتِ ثُمَّ تَابُوا مِن بَعْدِهَا وَآمَنُوا إِنَّ رَبَّكَ مِن بَعْدِهَا لَغَفُورٌ رَّحِيمٌ ○[47]

Yaani, wale ambao katika shauku ya kumwabudu ndama walifanya vitendo viovu, kisha baada yake wakatubia na kuamini, basi Mwenyezi Mungu Atawasamehe madhambi yao baada ya kuamini kwao na kuwarehemu, maana Yeye ni Msamehevu

[47] Sura Al-A'raaf, 7:154

na ni Mwingi wa ukarimu.

Na katika kesi ya Lekhram, aya tukufu inaashiria kuwa wale walioukadhibisha ufunuo pasipo haki na wakapanga hila za mauaji na wakaichochea serikali kuniua na baada ya hapo wakafanya toba na kuamini, hapo Mungu Atawahurumia. Kuhusiana na habari hii nimefunuliwa: يَا مَسِيْحَ الْخَلْقِ عَدْوَانَا Yaani, Ewe Masihi kwa ajili ya viumbe, uzingatie magonjwa yetu ya kuambukiza. Na kwenye uk. 519 wa *Barahine Ahmadiyya* imo ishara kwa habari hiyo kama Anavyosema Yule Mwenye Jina Tukufu:

اَنْتَ مُبَارَكٌ فِي الدُّنْيَا وَ الْاٰخِرَةِ ۔ اَمْرَاضُ النَّاسِ وَبَرَكَاتُهٗ ۔

اِنَّ رَبَّكَ فَعَّالٌ لِمَا يُرِيْدُ

Yaani, umejaaliwa baraka katika dunia na Akhera. Wasaidie watu katika maradhi yao kwa baraka za Mungu, kwani Mola wako Anafanya Atakavyo. Angalieni, hizi ni habari za zama gani, na haijulikani lini zitatimia. Kuna wakati ambapo wanakufa kwa dua, na waja wakati mwingine ambapo watahuika kwa dua.

**Bishara ya kumi na tisa**: Bishara hii iliyopo kwenye uk. 240 wa *Barahine Ahmadiyya*, ni hii:

رَبِّ اَرِنِيْ كَيْفَ تُحْيِي الْمَوْتٰى رَبِّ اغْفِرْ وَارْحَمْ مِنَ السَّمَآءِ ۔ رَبِّ لَا تَذَرْنِيْ

فَرۡدًا وَ اَنۡتَ خَیۡرُ الۡوَارِثِیۡنَ۔ رَبِّ اَصۡلِحۡ اُمَّۃَ مُحَمَّدٍ۔ رَبَّنَا افۡتَحۡ بَیۡنَنَا وَ بَیۡنَ
قَوۡمِنَا بِالۡحَقِّ وَ اَنۡتَ خَیۡرُ الۡفَاتِحِیۡنَ۔ یُرِیۡدُوۡنَ اَنۡ یُّطۡفِئُوۡا نُوۡرَ اللّٰہِ بِاَفۡوَاہِھِمۡ
وَاللّٰہُ مُتِمُّ نُوۡرِہٖ وَلَوۡ کَرِہَ الۡکَافِرُوۡنَ۔ اِذَا جَآءَ نَصۡرُ اللّٰہِ وَالۡفَتۡحُ وَانۡتَھٰی اَمۡرُ
الزَّمَانِ اِلَیۡنَا اَلَیۡسَ ھٰذَا بِالۡحَقِّ۔

**Tafsiri**: Yaani, Ewe Mola wangu, nionyeshe mimi kuwa Wewe Unahuishaje wafu, Ewe Mola wangu, Ghofiri na Rehemu kutoka mbinguni. Ewe Mola wangu, Usiniache peke yangu, na Wewe ndiwe Mbora wa warithi. Ewe Mola wangu, Usuluhishe umati wa Muhammad[saw]. Ewe Mola wangu, Utufanyie maamuzi ya kweli baina yetu na baina ya kaumu yetu, nawe ndiwe Mbora wa waamuzi. Watu hao watanuia kuizima nuru ya Mungu kwa pumzi za vinywa vyao, na Mungu Ataitimiza nuru yake hata kama makafiri wachukie. Msaada wa Mungu utakapokuja na ushindi wake utakaposhuka na mioyo itafululiza kuelekea kwetu na zitaishia kwetu, ndipo itasemwa kuwa je hii haikuwa kweli? Ndani ya ufunuo huu wote mna bishara hii kuwa hakuna budi kaumu ifanye upinzani na ijitahidi kikamilifu kuiangamiza silsila hii, na isipende kabisa kuwa silsila hii iweze kukaa imara. Lakini, Mungu Ataiendeleza silsila hii mpaka dunia itakapogeukia upande huu huu, na baada ya kwamba watu watakuwa wameiacha peke yake, kisha watarejea upande huu huu. Sasa

angalieni kuwa bishara hii imetimia barabara namna gani? Katika zama za *Barahine Ahmadiyya* kulikuwa hakuna kelele za maulamaa, bali yule aliye mwanzilishi wa fitina ya ukufurishaji, yeye alikuwa ameandika maoni yake juu ya kitabu cha *Barahine Ahmadiyya* kwa kukisifu kikamilifu. Kisha baada ya muda mrefu kupita ikazuka tufani ya ukufurishaji, na kwa muda fulani ikaendelea kuonyesha nguvu yake. Na sasa sawa na ufunuo wa Mungu mafuriko hayo yanaendelea kupungua kidogo, na wakati unakuja wa nuru kushinda wazi wazi na giza kushindwa kabisa.

**Bishara ya ishirini**: Bishara hii imo ndani ya *Barahine Ahmadiyya* kumhusu Atham, iliyo kwenye uk. 241. Sisi tumekwisha iandika kwa kirefu. Na muda mrefu umepita tangu Bwana Atham alipoihama dunia hii na kufikia makao yake. Wapinzani wetu sasa hawana shaka kuwa Atham ameishakufa kama alivyokwishakufa Lekhram na kama alivyokufa Ahmad Beg. Lakini kwa sababu ya upofu wao wanasema kuwa Atham hakufa ndani ya muda uliowekwa. Enyi watu wapumbavu, yule mtu aliyekufa sawa na onyo la Mungu, sasa kuna haja gani ya kujadili juu ya muda uliowekwa ama usiowekwa. Hebu onyesheni, yuko wapi sasa, au anakaa mji gani? Mmeisha sikia kuwa yeye ndani ya muda

maalum alianza kupata mchomo wa jahanamu. Yeye akatekeleza sharti, kwa hiyo akaishi siku chache kama nusu mzima, mwishowe moto ule haukumwacha na ukamwunguza.

Huu ni mfano mmoja mkubwa wa kudra za ghaibu za Mwenyezi Mungu kuwa habari ya tukio la Atham ikaandikwa ndani ya *Barahine Ahmadiyya* miaka kumi na saba iliyopita. Kwanza ikaashiria kwenye majadiliano yale yaliyokuwa yamefanyika huko Amritsar kuhusu Umoja wa Mungu na Utatu. Na Alisema kuhusiana na hilo kuwa:

قُلْ هُوَ اللّٰهُ اَحَدٌ اَللّٰهُ الصَّمَدُ لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُوْلَدْ وَلَمْ يَكُنْ لَّهٗ كُفُوًا اَحَدٌ

Kisha ikatolewa habari za hila ya Wakristo waliyoifanya kwa kuuficha ukweli baada ya muda uliowekwa kupita. Kisha ikapashwa habari ya fitina yenye ujanja iliyodhihirishwa na Wakristo kwa harara ya uadui. Kisha mwishoni ikatolewa habari njema ya kudhihiri ukweli. Kisha kwa ufunuo huu uliopo kwenye uk. 241 yaani: اِنَّا فَتَحْنَا لَكَ فَتْحًا مُّبِيْنًا habari njema ya ushindi mkubwa ikabashiriwa. Sasa hebu semeni kuwa je hii ni kazi ya binadamu? Fumbueni macho mkaone bishara kuhusu Atham ina habari zenye shani adhimu namna gani za ghaibu ndani yake.

**Bishara ya ishirini na moja**: Bishara hii imeandikwa

kwenye uk. 241 wa *Barahine Ahmadiyya*:

فَتۡحُ الۡوَلِيِّ فَتۡحٌ وَ قَرَّبۡنَاهُ نَجِيًّا اَشۡجَعُ النَّاسِ
وَلَوۡ كَانَ الۡاِيۡمَانُ مُعَلَّقًا بِالثُّرَيَّا لَنَالَهُ ۔ اَنَارَ اللّٰهُ بُرۡهَانَهٗ

Tafsiri: Ushindi hasa ndio ule ulio ushindi wa walii huyu. Nasi Tumempa ukaribu kwa hadhi ya kuwa msiri. Yu shujaa kuliko watu wote. Kama imani ingekuwa imekwenda kwenye kilimia, yeye angeileta kutoka huko. Mungu Atainurisha dalili yake.

**Bishara ya ishirini na mbili**: Bishara hii pia imo ndani ya *Barahine Ahmadiyya* uk. 241, nayo ni hii:

اِنَّكَ بِاَعۡيُنِنَا يَرۡفَعُ اللّٰهُ ذِكۡرَكَ وَيُتِمُّ نِعۡمَتَهٗ عَلَيۡكَ فِي الدُّنۡيَا وَالۡاٰخِرَةِ

Yaani, u mbele ya macho Yetu. Mungu Atakunyanyulia kumbukumbu yako, na Atakutimizia neema zake katika dunia na Akhera. Na Aliposema kuwa Atakunyanyulia kumbukumbu yako, maana yake ni kuwa watu mahususi wa dunia na dini watakutaja kwa sifa, na wenye vyeo vya juu watashughulikia kukusifu. Sasa je, si ajabu kwamba mtu anayehesebiwa kuwa kafiri na hakiri na anaitwa kuwa ni dajali na shetani, awe na mwisho huu kuwa watu wenye vyeo vikubwa wa kidini na kidunia watamsifu kwa mioyo ya kweli.

**Bishara ya ishirini na tatu**: Bishara hii imeandikwa kwenye uk. 242 wa *Barahine Ahmadiyya*:

إِنِّیْ رَافِعُكَ إِلَیَّ ۔ وَأَلْقَیْتُ عَلَیْكَ مَحَبَّةً مِّنِّیْ وَبَشِّرِ الَّذِیْنَ اٰمَنُوْٓا اَنَّ لَهُمْ قَدَمَ صِدْقٍ عِنْدَ رَبِّهِمْ ۔ وَاتْلُ عَلَیْهِمْ مَا اُوْحِیَ إِلَیْكَ مِنْ رَّبِّكَ وَلَا تُصَعِّرْ لِخَلْقِ اللّٰهِ وَلَا تَسْئَمْ مِنَ النَّاسِ ۔

Tafsiri: Mimi Nitakuinua Kwangu na kutoka Kwangu Nitakutilia upendo. Yaani, baada ya watu kukufanyia uadui na bughudha mara watarudishwa kwenye upendo, kama ilivyo katika alama za Mahdi Mau'udi. Na kisha Akasema, wale watu watakaokuamini uwapashe habari njema kuwa mbele ya Mola wao wana daraja kamili. Na uwasomee ule wahyi Ninaokuteremshia Mimi. Usiwape kisogo watu wala usichoke kukutana nao. Baada ya hapo nikafunuliwa: وَ وَسِّعْ مَكَانَكَ Yaani, panua nyumba yako. Katika bishara hii Ameelezwa wazi kuwa siku ile inakuja ambapo wenye kukuzuru watafurika mpaka itakuwa vigumu kwa kila mmoja kuonana nawe. Basi wakati huo usidhihirishe kuudhika wala usichoke kuonana na watu. Subhanallah! Bishara hii ni yenye shani kubwa namna gani! Na imeelezwa miaka kumi na saba hapo kabla toka leo ambapo katika kikao changu pengine watu wawili au watatu walikuwa wanakuja, tena kwa siku moja moja. Hiyo inathibitisha namna gani elimu ya ghaibu ya Mungu!

**Bishara ya ishirini na nne**: Bishara hii imo ndani ya *Barahine Ahmadiyya* kwenye uk. 489, nayo ni hii:

اَنْتَ وَجِيْهٌ فِيْ حَضْرَتِيْ اِخْتَرْتُكَ لِنَفْسِيْ۔ اَنْتَ مِنِّيْ بِمَنْزِلَةِ تَوْحِيْدِيْ وَ
تَفْرِيْدِيْ فَحَانَ اَنْ تُعَانَ وَ تُعْرَفَ بَيْنَ النَّاسِ۔

Yaani, u mwenye heshima kwangu. Nimekuchagua wewe. U kwangu kama Tauhidi yangu na Umoja Wangu. Hivyo, wakati umewadia ambapo utasaidiwa na wewe utafanywa mashuhuri baina ya watu. Hii bishara ni ya wakati ule ambapo hata ndani ya kijiji hiki kidogo pia watu wengi hawakunijua. Na sasa ambapo miaka 17 imepita baada ya bishara hii, sawa na muradi wa bishara, nimepata kujulikana kiasi hiki kwamba hata pengine watoto na wanawake pia wa kaumu nyingine wa nchi hii hawatakosa kunijua. Yule mtu ajuaye habari za zama hizi mbili[48] kuwa ule wakati ulikuwaje na sasa ukoje, bila kusita roho yake itasema kuwa elimu hii ya ghaibu yenye shani adhimu ni mbali na nguvu za binadamu, kama kwa ilivyo nguvu ya nzi mbali na kazi ya ndovu mwenye nguvu nyingi mno.

**Bishara ya ishirini na tano**: Bishara hii imo ndani

[48] Tanbihi: Mimi mnyenyekevu Sirajul Haq Jamali nimeziona kwa fadhili za Allah zama zote mbili, na imani imeongezeka. Na ninamwomba Mungu kuwa katika siku zijazo Atuonyeshe upeo wa ukamilifu na maendeleo ya Imam huyu wa haki na maasumu, na Atuzidishie imani kwa kuweka pamoja na mkweli huyu. (Jamali)

ya *Barahine Ahmadiyya* kwenye uk. 490, nayo ni hii:

سُبْحَانَ اللّٰهِ تَبَارَكَ وَتَعَالٰى زَادَ مَجْدَكَ يَنْقَطِعُ اٰبَاءُكَ وَيُبْدَءُ مِنْكَ۔

Tafsiri: Ametukuka Yule Mungu Aliye Mwenye baraka na Mtukufu. Utakatifu wako Ameuzidisha Yeye. Sasa itakuwa hivi kuwa jina la mababu yako litakatika na hakuna yeyote atakayewakumbuka kwa kudumu, na Mungu Ataweka dhati yako kuwa msingi wa ukoo wako.

Katika bishara hii kuna ahadi mbili. (1) Ya kwanza ni kuwa Mungu Ataumba watoto mastadi na wema katika ukoo huu. Na ya pili ni kwamba chanzo cha heshima na adhama nitafanywa mimi. Na bishara ile iliyotolewa juu ya mwana aliyebarikiwa, kwa kweli ufunuo huo pia ni sehemu mojawapo ya ufanuo huu huu. Wakati ule wapumbavu walipiga kelele kuwa karibu na zama za kutolewa bishara mvulana hakuzaliwa bali alizaliwa binti. Kelele zote hizi zilikuwa kwa sababu hii kwamba wapumbavu hao wakafikiri kuwa ni lazima bishara itimie moja kwa moja pasipo kuzaliwa mtoto mwingine katikati, na ndani ya funuo Mungu Hakusudii hivi, bali hata kama mabinti elfu moja wazaliwe kisha mvulana wa sifa hizo azaliwe, hapo pia itasemwa kuwa bishara imetimia. Naam, kama ndani ya ufunuo wa Mungu neno moja kwa moja pasipo mwingine kuzaliwa

katikati lingekuwepo, hapo ingekuwa hakuna budi kudhihirika bishara kulingana na neno hili.

**Bishara ya ishirini na sita**: Bishara ya ishirini na sita kwenye uk. 491 wa *Barahine Ahmadiyya* ni hii:

وَمَا كَانَ اللّٰهُ لِيَتْرُكَكَ حَتّٰى يَمِيْزَ الْخَبِيْثَ مِنَ الطَّيِّبِ وَاللّٰهُ غَالِبٌ عَلٰى اَمْرِهٖ وَلٰكِنَّ اَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُوْنَ

Tafsiri: Mungu Hatakuacha wewe mpaka Apambanue baina ya safi na uchafu. Na Mungu ni Mshindi juu ya jambo lake, lakini watu wengi hawajui.

**Bishara ya ishirini na saba**: Bishara hii imo ndani ya *Barahine Ahmadiyya*, uk. 492, nayo ni hii: اَرَدْتُّ اَنْ اَسْتَخْلِفَ فَخَلَقْتُ اٰدَمَ Yaani, Mimi Nilikusudia kuweka Khalifa, hivyo Nikamwumba Adam. Na katika sehemu nyingine kuhusu maelezo yake kuna ufunuo huu: وَقَالُوْا اَتَجْعَلُ فِيْهَا مَنْ يُفْسِدُ فِيْهَا قَالَ اِنِّيْٓ اَعْلَمُ مَا لَا تَعْلَمُوْنَ Yaani, watu wakanena kuwa Unamfanya mtu kama huyo kuwa Khalifa atakayefanya ufisadi ardhini. Mungu Akasema, Mimi Ninakijua kitu fulani ndani yake ambacho nyinyi hamna habari nacho, kama Alivyosema ndani ya ufunuo mwingine katika *Barahine Ahmadiyya* hicho hicho: اَنْتَ مِنِّيْ بِمَنْزِلَةٍ لَا يَعْلَمُهَا الْخَلْقُ Yaani, wewe unalo daraja mbele yangu ambalo dunia haina habari nalo. Sasa ni dhahiri kuwa bishara

hii ilishachapishwa ndani ya *Barahine Ahmadiyya* tangu miaka 17 iliyopita, na fitina ile inakoashiria bishara hii ikadhihirika baada ya miaka mingi. Hivyo, mashekhe wakaniita mimi mfisadi. Fatuwa za kunikufurisha zikaandikwa. Nadhir Husain wa Delhi (iwe juu yake anavyostahiki) akaweka msingi wa kukufurisha. Na Muhammad Husain Batalawii kama makafiri wa Makka akichukuwa jukumu la huduma hii akaandikisha fatuwa za kukufurisha juu yake kutoka kwa watu maarufu na wasiokuwa maarufu. Na kama vile inavyojulikana kutokana na ufunuo wa Mungu kuwa ndani ya *Barahine Ahmadiyya* taarifa ilikuwa imeishatolewa hapo kabla kwamba fatuwa za namna hii zitaandikwa. Na Hadithi za Mtume[saw] pia zilieleza kuwa Mahdi Mau'udi atatolewa fatuwa ya kumkufurisha. Hivyo, yote yaliyoandikwa yakatimia.

Bishara ya ishirini na nane: Bishara hii imo ndani ya *Barahine Ahmadiyya* kwenye uk. 496, nayo ni hii:

يُحْيِى الدِّيْنَ وَيُقِيْمُ الشَّرِيْعَةَ يَا آدَمُ اسْكُنْ اَنْتَ وَزَوْجُكَ الْجَنَّةَ۔ يَا مَرْيَمُ اسْكُنْ اَنْتَ وَزَوْجُكَ الْجَنَّةَ يَا اَحْمَدُ اسْكُنْ اَنْتَ وَزَوْجُكَ الْجَنَّةَ۔ نَفَخْتُ فِيْكَ مِنْ لَّدُنِّيْ رُوْحَ الصِّدْقِ

Tafsiri: Ataihuisha dini na atasimamisha sheria. Ewe Adamu, wewe na mwenzako ingieni Peponi. Ewe Mariamu, wewe na mwenzako ingieni Peponi. Ewe Ahmad, wewe na mwenzako ingieni Peponi. Mimi

Nimekupulizia roho ya ukweli kutoka Kwangu. Hii ni bishara yenye shani adhimu. Na kwa majina matatu kuna ishara kwenye matukio matatu yajayo ambayo karibuni watu watayajua. Na katika ufunuo huu neno ladun lililotumika maelezo yake yamejulikana kwa njia ya kashfi kuwa Malaika mmoja anasema ndani ya ruya kuwa mahali hapa *ladun* ulipofikishwa, ni mahali ambapo mvua yadumu kunyesha na mvua haikatiki hata mara moja.

**Bishara ya ishirini na tisa**: Hii ni ile bishara iliyoandikwa ndani ya *Barahine Ahmadiyya* kwenye uk. 506, nayo ni hii:

لَمْ يَكُنِ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا مِنْ اَهْلِ الْكِتَابِ وَالْمُشْرِكِيْنَ مُنْفَكِّيْنَ حَتّٰى تَأْتِيَهُمُ الْبَيِّنَةُ

Na kisha Akasema kuwa kama Mungu Asingefanya hivi giza lingetanda duniani. Hii inaashiria kwenye ishara ya Mungu itakayolinda dunia isiangamie. Na maana ya ufunuo ni kuwa haikuyumkinika kuwa watu wa Kitabu na Mabaniani wangejiepusha na chuki na uadui kama Nisingewapatia ishara ya wazi wazi. Na kama Nisingefanya hiyo, giza lingetanda duniani na ukweli ungetiwa mashakani.

**Bishara ya thelathini:** Hii ni bishara ile iliyoandikwa ndani ya *Barahine Ahmadiyya* ukurasa

wa 515, nayo ni hii:

إِنَّا فَتَحْنَا لَكَ فَتْحًا مُّبِينًا لِّيَغْفِرَ لَكَ اللَّهُ مَا تَقَدَّمَ مِن ذَنبِكَ وَمَا تَأَخَّرَ

Yaani, Sisi Tutakupa ushindi mmoja wa wazi wazi ili Sisi Tukusamehe madhambi yako ya nyuma na ya mbele. Istiara hii Ameitumia kuonyesha ridhaa yake. Kwa mfano, Bwana fulani anakaa na mtumwa wake kwa hekima namna ambavyo wapumbavu wanadhani kuwa yeye amemkasirikia, ndipo ghera ya Bwana yamhamasishika kufanya jambo fulani kwa kumpatia mtumwa huyo heshima, kana kwamba Amemsamehe dhambi zake zote za nyuma na mbele. Yaani, anaonyesha ridhaa kwa namna ambavyo watu hupata yakini kuwa mpole kama huyo hatamkasirikia katu. Hii ni bishara yenye shani adhimu. Kisha baada yake kwenye ukurasa huo picha moja imeoneshwa. Picha hiyo ni yangu, mavazi ya kijani, na picha ni yenye heba sana, mithili ya mkuu wa majeshi mshindi mwenye silaha, na kwa upande wa kulia na kushoto wa picha imeandikwa haya: حُجَّةُ اللهِ الْقَادِرِ۔ سُلْطَان اَحْمَد مُخْتَار[49], na tarehe iliyoandikwa ni hii: Siku ya Jumatatu 19 Dhilhija 1300 sawa na 23 Oktoba 1883, sawa na 6 Kaatak 1940 Bikrami. Ibara hizi zote zipo kwenye uk. 515 na uk. 516 wa *Barahine Ahmadiyya*. Kashfi

[49] Hoja ya Mwenyezi Mungu Mweza. Sultani Ahmad Mteule. Mfasiri.

hii inaonesha kuwa ishara moja itadhihiri kwa njia ya silaha. Basi, tukio la Lekhram lilitokea hivyo tu. Kisha baadaye kwenye uk. 516, mna ibara ya ufunuo huu:

اَلَيْسَ اللهُ بِكَافٍ عَبْدَهُ۔ فَبَرَّأَهُ اللهُ مِمَّا قَالُوْا وَكَانَ عِنْدَاللهِ وَجِيْهًا ۔ فَلَمَّا
تَجَلّٰى رَبُّهٗ لِلْجَبَلِ جَعَلَهُ دَكًّا وَّاللهُ مُوْهِنُ كَيْدِ الْكَافِرِيْنَ۔ وَلِنَجْعَلَهٗ اٰيَةً
لِّلنَّاسِ وَرَحْمَةً مِّنَّا وَكَانَ اَمْرًا مَقْضِيًّا

Yaani, je Mungu Hamtoshei mtumishi wake? Basi Mungu Akamwondolea tuhuma ile waliyombambikizia makafiri. Naye mbele ya Mungu yu mwenye heshima. Na Mungu Alivunja vipande vipande milima ya matatizo na Akaidhoofisha hila ya makafiri. Nasi Tutamfanya kuwa ishara moja kwa rehema Yetu, na ilikuwa imekadiriwa hivyo tangu mwanzo. Ndani ya ufunuo huu, Mwenyezi Mungu Anadhihirisha kuwa baada ya Lekhram kuuawa, Mabaniani watatuhumu kuwa zilifanywa njama za mauaji, na watafanya hila moja ili tuhuma hiyo ipate nguvu. Sisi Tutadhihirisha kuondolewa tuhuma hizo kwa huyu mpokeaji wa funuo, na tutavunja hila yao, na shida zote zitaondolewa kwa urahisi.

Sasa sio lazima kuwa tumwelekeze yeyote kwenye bishara hii. Waadilifu wafikiri wenyewe na wasiharibu Akhera yao kwa kuyakataa mambo haya ya ghaibu ya wazi wazi.

Yafaa kukumbuka hili pia kuwa ndani ya bishara hii Lekhram amelinganishwa na ndama. Ndani yake mna milingano kadha. (1) Kwanza ni kwamba kama vile ndama ya Samiri hakuwa na uhai, vivyo hivyo huyu pia hakuwa na uhai, na roho ya ukweli haikuwemo ndani yake (2) Pili ni hii kwamba kama vile kutoka ndani ya ndama asiye na uhai, sauti isiyo na maana ilikuwa inatokea vivyo hivyo ndani ya huyu pia sauti isiyo na maana ilikuwa inatokea. (3) Wa tatu ni kuwa kama vile ndama asiye na uhai aliangamizwa siku ya Idi, vivyo hivyo huyu pia aliangamizwa siku za Idi. (4) Wa nne ni kuwa kama vile ndama ile ilikuwa imetengenezwa kwa mapambo ya dhahabu ya taifa, vivyo hivyo ndama huyu pia alikuwa ametengenezwa kwa sababu ya mali ya jamii. (5) Wa tano ni kwamba kama ndama ile mwishoni ikawa sababu ya adhabu mbalimbali na mateso kwa ajili ya wazushi wa kaumu, ndivyo utakavyokuwa mwisho wa wazushi wamwabuduo ndama huyu.

**Bishara ya thelathini na moja**: Hii ni ile bishara iliyoandikwa kwenye uk. Wa 522 wa *Barahine Ahmadiyya*. Nayo ni

بخرام کہ وقت تو نزدیک رسید و پائے محمدیاں بر منار بلند تر محکم افتاد۔ پاک محمد مصطفیٰ نبیوں کا سردار۔ خدا تیرے سب کام درست کر دے گا اور تیری ساری مرادیں تجھے دے گا۔ رب الافواج اس طرف توجہ کرے گا۔ اس نشان

کا مدعا یہ ہے کہ قرآن شریف خدا کی کتاب اور میرے منہ کی باتیں ہیں جناب الٰہی کے احسانات کا دروازہ کھلا ہے اور اسکی پاک رحمتیں اس طرف متوجہ ہیں۔

Ufurahi, kwani wakati wako umekurubia na miguu ya Waislamu imeimarika juu ya mnara mrefu. Mtukufu Muhammad Mteule Mkuu wa Manabii. Mungu Atakusavazishia kazi zako zote na Atakupatia matumaini yako yote. Mola wa Majeshi Ataelekea upande huu. Kusudi la ishara hii ni kuwa Kurani Tukufu ni Kitabu cha Mungu na ni maneno kutoka Mdomoni Mwangu. Mlango wa hisani za Mungu u wazi na rehema Zake takatifu zinaelekea upande huu.

**Bishara ya thelathini na mbili**: Hii ni ile bishara iliyoandikwa kwenye uk. 556 na 557 wa *Barahine Ahmadiyya,* nayo ni hii:

يٰعِيْسٰى اِنِّىْ مُتَوَفِّيْكَ وَرَافِعُكَ اِلَىَّ وَجَاعِلُ الَّذِيْنَ اتَّبَعُوْكَ فَوْقَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا اِلٰى يَوْمِ الْقِيَامَةِ ۔

Mimi Nitaonyesha mng'ao Wangu. Nitakunyanyua kudhihirisha kudra yangu. Mwonyaji mmoja amekuja duniani, lakini dunia haikumkubali, lakini Mungu Atamkubali na kwa mashambulizi makali Atadhihirisha ukweli wake اَلْفِتْنَةُ هٰهُنَا فَاصْبِرْ كَمَا صَبَرَ اُولُو الْعَزْمِ . Bishara hii ilimhusu Lekhram, ambayo ilitimia na maelezo yake yameisha tolewa, na ishara zingine

zilizobakia zitakuja pia. Na kuhusiana na hiyo, ufunuo huu umo ndani ya *Barahine Ahmadiyya* kwenye uk. 560 na uk. 510:

وَ يُخَوِّفُوْنَكَ مِنْ دُوْنِهٖ۔ اَئِمَّةُ الْكُفْرِ۔ لَا تَخَفْ اِنَّكَ اَنْتَ الْاَعْلٰى يَنْصُرُكَ اللّٰهُ فِيْ
مَوَاطِنَ۔ اِنَّ يَوْمِيْ لَفَصْلٌ عَظِيْمٌ

Yaani, makafiri watakuogopesha, lakini mwishoni wewe tu ndio utapata ushindi. Mungu Atakupa ushindi ndani ya medani. Siku Yangu itakuwa ni siku ya hukumu kubwa.

يُظِلُّ رَبُّكَ عَلَيْكَ وَ يُغِيْثُكَ وَ يَرْحَمُكَ يَعْصِمُكَ اللّٰهُ مِنْ عِنْدِهٖ وَاِنْ لَّمْ
يَعْصِمْكَ النَّاسُ۔ وَ اِنْ لَّمْ يَعْصِمْكَ النَّاسُ يَعْصِمُكَ اللّٰهُ مِنْ عِنْدِهٖ اِنِّيْ
مُنَجِّيْكَ مِنَ الْغَمِّ اَنْتَ مِنِّيْ بِمَنْزِلَةٍ لَا يَعْلَمُهَا الْخَلْقُ كَتَبَ اللّٰهُ لَاَغْلِبَنَّ اَنَا وَ
رُسُلِيْ لَا مُبَدِّلَ لِكَلِمٰتِهٖ

(Tafsiri) Mungu Atakutilia kivuli cha rehema Yake na Atasikia kilio chako na Atakurehemu. Yeye Mwenyewe Atakuokoa, ingawa asikuokoe yeyote miongoni mwa watu. Nasema tena kuwa ingewaje asikuokue yeyote kati ya watu lakini Yeye Mwenyewe Atakuokoa. Mimi Nitakuepusha na huzuni. Wewe una ukaribu ule na Mimi wasioujua watu. Mungu Amekwisha andika kuwa Nitashinda Mimi na Wajumbe wangu. Basi maneno ya Mungu hayatabadiliki kamwe.

**Bishara ya thelathini na tatu**: Bishara hii

imeandikwa ndani ya *Barahine Ahmadiyya* uk. 558 na 559. Nayo ni hii:

سَلَامٌ عَلَيْكَ يَا اِبْرَاهِيْمُ اِنَّكَ الْيَوْمَ لَدَيْنَا مَكِيْنٌ اَمِيْنٌ۔ حِبُّ اللهِ خَلِيْلُ اللهِ۔ اَسَدُ اللهِ اَلَمْ نَجْعَلْ لَكَ سُهُوْلَةً فِيْ كُلِّ اَمْرٍ بَيْتُ الْفِكْرِ ۔وَبَيْتُ الذِّكْرِ۔ وَ مَنْ دَخَلَهٗ كَانَ اٰمِنًا ۔ مُبَارِكٌ وَ مُبَارَكٌ وَ كُلُّ اَمْرٍ مُبَارَكٍ يُجْعَلُ فِيْهِ۔ رُفِعَتْ وَ جُعِلَتْ مُبَارَكًا۔ وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَ لَمْ يَلْبَسُوْا اِيْمَانَهُمْ بِظُلْمٍ اُولٰٓئِكَ لَهُمُ الْاَمْنُ وَهُمْ مُّهْتَدُوْنَ۔

Tafsiri: Salaam iwe juu yako ewe Ibrahim. Leo U mwenye hadhi Kwetu na mwaminifu, rafiki wa Mungu, halili wa Mungu, simba wa Mungu. Tumekufanyia urahisi katika kila jambo. Baitul-Fikri na Baitudh-Dhikri. Na yeyote aingiaye humo amekuwa salama. Ile Baitudh-Dhikri inabariki na imebarikiwa. Na kila kazi ya baraka itafanywa humo. Na wale watu walioamini na hawakuichafua imani na dhuluma yoyote, hao ndio watapewa amani na hao ndio watakaoongoka.

Baitud-dhikri muradi wake ni ule msikiti uliojengwa juu ya paa ya nyumba. Na ufunuo huu: مُبَارِكٌ وَ مُبَارَكٌ وَ كُلُّ اَمْرٍ مُبَارَكٍ يُجْعَلُ فِيْهِ, unaeleza mwaka wa ujenzi wa msikiti huu. Isitoshe, hii ni bishara ya baraka za baadaye ambazo kudhihiri kwake msingi umewekwa sasa.

**Bishara ya thelathini na nne**: Bishara hii imo ndani ya *Barahine Ahmadiyya* iliyoandikwa kwenye

ukurasa wa 521, nayo ni hii:

وہ تجھے بہت برکت دے گا یہاں تک کہ بادشاہ تیرے کپڑوں سے برکت ڈھونڈیں گے

Yeye Atakupa baraka nyingi hata kwamba wafalme watatafuta baraka katika nguo zako. Na kuna kashfi moja kuhusu hii, nayo ndiyo kwamba niliona ndani ya kashfi kuwa ardhi iliongea na mimi ikasema: يَا وَلِيَّ اللهِ كُنْتُ لَا أَعْرِفُكَ. Yaani, Ewe walii wa Mungu, mimi nilikuwa sikutambui.

**Bishara ya thelathini na tano**: Sheikh Muhammad Husain Batalawii, mwenye gazeti la *Isha'atu Sunnah*, ambaye ndiye mwanzilishi wa kunikufurisha na ambaye juu ya shingo yake upo mzigo wa dhambi ya wakufurushaji wote baada ya Nadhir Husain wa Delhi, na ambaye athari zake kidhahiri ni mbovu na zenye hali ya kukatisha tamaa. Nimepata kujua mara tatu kuhusiana naye kuwa atajiondoa katika hali yake hii ya upotovu, na kisha Mungu Atafungua macho yake. وَاللهُ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ[50]

Na safari moja niliona ndani ya ndoto kana kwamba nimekwenda nyumbani kwa Muhammad Husain na pamoja nami kuna kundi moja, nasi tulisali pale nami niliongoza. Nikafikiria kuwa nimefanya kosa

[50] Na Mungu Ana uwezo juu ya kila kitu. Mwenezi

katika sala kuwa ndani ya sala ya Adhuhuri au Alasiri nilikuwa nimeanza kusoma Sura Fatiha kwa sauti kubwa. Kisha nikatambua kuwa sikuisoma Sura Fatiha kwa sauti kubwa bali ni Takbira tu ndiyo niliyotamka kwa sauti kubwa. Na tulipomaliza sala, nikamwona Muhammad Husain amekaa mbele yetu. Wakati huo namwona kama mwenye rangi nyeusi na yuko rabana kabisa. Mimi nikaona haya kuangalia upande wake kisha katika hali hiyo hiyo yeye akaja kwangu. Nikamwambia kuwa je wakati haujafika kwamba wewe ufanye suluhu, na je unataka suluhu ifanywe na wewe? Yeye akasema ndiyo. Basi, yeye akanisogelea sana na akanikumbatia. Wakati huo yeye alikuwa kama mtoto mdogo. Kisha nikasema kuwa ukitaka, usamehe maneno niliyosema kwako yaliyokuumiza, na ukumbuke vizuri kuwa mimi sikusema chochote isipokuwa kwa nia safi, nasi tunaiogopa siku ile nzito ya Mungu tutakaposimama mbele Yake. Yeye akasema kuwa mimi nimesamehe. Ndipo nikasema, uwe shahidi kwamba nimekusamehe maneno yote yaliyotoka mdomoni mwako na nimekusamehe wewe kunikufurisha na kunikadhibisha. Ndipo baada ya hapo yeye akaonekana kwa kimo chake cha asili na nguo nyeupe zikaonekana. Kisha nikasema, leo yametimia nilivyoona ndani ya ndoto.

Kisha mtangazaji akatangaza kuwa mtu mmoja jina lake ni Sultan Beg yumo katika gharighari ya mauti. Nikasema, hivi karibuni atakufa, maana nimeonyeshwa ndani ya ndoto kuwa itapatikana suluhu siku ya kifo chake. Kisha nikamwambia Muhammad Husain kuwa mimi niliona ndani ya ndoto kwamba alama ya siku ya suluhu ni hii kuwa siku hiyo Bahauddin atafariki. Muhammad Husain akisikia neno hili akaona kwa mtazamo wa heshima sana, na akastaajabia kama vile mtu anavyostaajabia adhama ya tukio la kweli, na akasema, hii ni kweli kabisa, na kwa hakika Bahauddin amefariki. Kisha nikamwalika kwenye maakuli, yeye baada ya kutoa udhuru kidogo akakubali mwaliko wangu. Kisha nikamwambia kuwa mimi niliona pia ndani ya ndoto kuwa suluhu itapatikana moja kwa moja. Basi ikatokea kama nilivyoona. Hii ilikuwa ni siku ya Jumatano, na tarehe ilikuwa 13 Desemba 1894.

**Bishara ya thelathini na sita**: Bishara ya thelathini na sita — kama nilivyokwisha andika ndani ya kitabu cha Izaala Auhaam — ni hii kuwa Mwenyezi Mungu Alinipasha habari kuwa umri wako utakuwa miaka themanini, ama utapungua kidogo au utazidi kidogo. Na ufunuo huu ni wa tangu muda wa miaka karibu ishirini au ishirini na miwili, ambao watu

wengi waliambiwa na hata ndani ya *Izaala Auhaam* pia uliandikwa na kuchapishwa.

**Bishara ya thelathini na saba**: Bishara ya thelathini na saba ni hii kuwa Mwenyezi Mungu Ameniambia kuwa wakati wa matangazo yaliyochapishwa kukabiliana na kaumu ya Aria, Mapadri na Masingasinga, mtu yeyote atakayejitokeza kukabiliana nami, Mungu Atanisaidia mimi katika uwanja huo. Vivyo hivyo ziko bishara nyingine zilizoandikwa ndani ya vitabu vingine mbalimbali. Na matukio ya namna hii yasiyo ya kawaida yamefikia karibu elfu tano ambayo mashahidi walioyashuhudia hayo wengi wao wangali hai mpaka sasa. Na kila mtu aliyekaa na mimi kwa muda fulani, yeye ameshuhudia kwa macho yake mwenyewe, na wanaendelea kushuhudia. Basi, ni masikitiko kwa watu wenye bahati mbaya wanaosema kuwa mwujiza wowote haukudhihirika kwa Mtume[saw] wala yeye hakutoa bishara yoyote ile. Hao wasiojua hawaelewi kuwa katika hali ambapo nuru na baraka hizi zaendelea kudhihiri kutoka kwa umati wake, ilhali ishara hizo hazidhihiriki kutoka kwa umati wa nabii mwingine yeyote awaye, ni kubatilisha vibaya namna gani kwamba chemchemi kama hii ya baraka ikataliwe. Bali, ukweli ni huu kuwa kama kusingekuwepo dhati

tukufu ya Mtume Mtukufu[saw], basi unabii wa Nabii yeyote usingeweza kuthibitika.

Ni dhahiri kuwa kuelezea tu visa na hadithi siyo uthibitisho. Visa hivi vinapatikana tu ndani ya kila taifa kwa wingi. Ulaaniwe moyo ule ambao uweke msingi wa imani yake juu ya visa tu, hasa wale watu ambao wamemfanya mtoto mnyonge wa binadamu kuwa Mungu. Hiyo ni kuamini bila kuona wala kuchunguza.

Tunapoangalia kwa uadilifu, twamtambua mwanamume mmoja tu ambaye miongoni mwa manabii wote ni Nabii shujaa mwenye daraja la juu, Nabii aliye hai, Nabii mpendwa wa daraja la juu sana wa Mungu, yaani ndiye yule yule kiongozi wa manabii, fahari ya mitume, mkuu wa mitume wote, ambaye jina lake ni Muhammad Mteule, Ahmad mchaguliwa, Amani na rehema za Allah ziwe juu yake, ambaye kwa kumfuata yeye barabara kwa siku kumi, mtu anapata mwanaga ule ambao haukuweza kupatikana hapo kabla kwa miaka elfu. Ni vya aina gani vile vitabu ambavyo hata sisi tukivifuata, vyataka kutufanya tukataliwe, tuachwe na tuwe na moyo mweusi. Je yafaa kuvitambua kuwa unabii hai ambao kwa kuufuata tunakuwa wafu. Tambueni

kwa yakini kuwa hivyo vyote vimekufa. Je mfu anaweza kumpatia mfu mwanga? Kumwabudu Yesu ni kuabudu sanamu tu. Mimi naapa kwa Dhati Yule Ambaye uhai wangu umo mkononi Mwake kuwa kama yeye angekuwa katika zama zangu, angelazimika kutoa kwa unyenyekevu ushahidi juu yangu. Mtu akubali au asikubali, lakini huu ndio ukweli, na ndani ya ukweli kuna baraka kwa kuwa mwanga wake unaiangukia dunia, ndipo kuta zote za dunia zinang'aa, isipokuwa wale waliomo gizani. Hivyo, wasia wa mwisho ndio huu kuwa nuru yote tumeipata kwa ufuasi wa Mjumbe Nabii Ummi, na yeyote atakayemfuata pia ataupata, na atajaaliwa ukubali wa aina hii hata kwamba kutakuwa hakuna lolote lisilowezekana mbele yake. Mungu Hai, Aliyefichika kwa watu, Atakuwa ni Mungu wake na miungu wote waongo watakanyagwa chini ya miguu yake na kupondwa, yeye atabarikiwa kila sehemu na nguvu za kiungu zitakuwa pamoja naye. Na amani iwe kwa yule afuataye mwongozo.

Sasa tunahitimisha kijitabu hiki kwa wasia huu kuwa Enyi mtafutao ukweli, tafuteni ukweli, kwani sasa milango ya mbingu iko wazi. Na Enyi Masheikh wa

taifa letu msioelewa[51], hizi ni siku zile zile za Mungu zilizoahidiwa. Hivyo, fumbueni macho mkaone ardhini kunafanyika nini, na vipi mfalme wa ukweli, Nabii mtakatifu, anakanyagwa chini ya miguu. Je imebaki kasoro yoyote katika kumfedhehesha Nabii huyu mtukufu? Je, haikuwa lazima kuwa katika wakati huu wa tufani ardhini idhihirike chochote mbinguni? Basi, kwa sababu hii Mungu Akamchagua mtumishi mmoja kutoka katika watumishi wake ili Aonyeshe kudra zake na Athibitishe uwepo wake, na Awajulishe wale waufanyiao mzaha ukweli na waupendao uongo kuwa Mimi Nipo, na ni Msaidizi wa ukweli. Kama Yeye katika wakati wa fitina kama hii Asingeonyesha Uso Wake, dunia ingeghariki katika upotovu, na kila nafsi ingekufa katika hali ya kumkataa Mungu na kumkana. Hii ni fadhili ya Mungu kuwa katika wakati ufaao hasa Akashikilia safina ya binadamu. Hii karne ya kumi na nne ilikuwa nini, ilikuwa ni mwezi wa usiku wa kumi na nne ambamo Mungu Ameitandaza nuru Yake ardhini mfano wa shuka. Sasa, je mtapigana na Mungu? Mtakigonga kichwa chenu kwenye ngome ya feleji? Oneni haya kidogo, na msisimame mbele ya ukweli.

[51] Nasema kuhusu maskeikh wa zama hizi yale tu yaliyosemwa mapema katika Hadithi. Mwandishi

Mungu Ameona kuwa ardhi imeungua na bidaa, ushirikina, na maovu, na uchafu ndio unaopendwa na ukweli unakataliwa, basi kama ilivyo desturi Yake tangu zamani Akaelekea kuirekebisha dunia. Maana mabadiliko ya kweli hutoka mbinguni na sio ardhini, na imani ya kweli inapatikana kutoka juu, siyo kutoka chini. Hivyo, Mungu Mrehemevu Akataka Aijadidishe imani na Awaonyeshe ishara wale walioitwa kupitia matangazo au watakaoitwa baadaye. Na Mungu wangu Akasema akiniambia:

اَلْاَرْضُ وَالسَّمَاءُ مَعَكَ كَمَا هُوَ مَعِیْ۔ قُلْ لِّیَ الْاَرْضُ وَالسَّمَآءُ۔ قُلْ لِّیْ سَلَامٌ فِیْ مَقْعَدِ صِدْقٍ عِنْدَ مَلِیْكٍ مُّقْتَدِرٍ۔ اِنَّ اللّٰهَ مَعَ الَّذِیْنَ اتَّقَوْا وَ الَّذِیْنَ هُمْ مُّحْسِنُوْنَ۔ یَاْتِیْ نَصْرُ اللّٰهِ۔ اِنَّا سَنُنْذِرُ الْعَالَمَ كُلَّهٗ۔ اِنَّا سَنَنْزِلُ۔ اَنَا اللّٰهُ لَا اِلٰهَ اِلَّا اَنَا۔

Yaani, mbingu na ardhi zipo pamoja nawe kama zilivyo pamoja Nami. Sema, mbingu na ardhi ni kwa ajili yangu. Sema, amani ni kwa ajili yangu, ile amani iliyoko kwa Mungu Mweza kwenye makao ya ukweli. Mungu Yu pamoja na wale wanaomcha na ambao kawaida yao ni kuwa wanawatendea wema viumbe wa Mungu. Msaada wa Mungu unakuja. Sisi Tutaitanabahisha dunia nzima. Sisi Tutashuka ardhini. Mimi ndimi Mungu Mkamilifu na Mkweli, hakuna yeyote minghairi yangu.

Katika funuo hizo mna ahadi zenye nguvu za msaada wa Mungu, lakini msaada wote huu utakuwa kwa ishara za kimbingu. Ni wadhalimu, wasiojua, na majahili wale wanaodhani kuwa Masihi Mau'udi na Mahdi Mau'udi atakuja na upanga. Maandiko ya unabii yanasema kwa kupaza sauti kuwa katika zama hizi si upanga bali ishara za kimbingu zitasababisha kushinda mioyo, na hata hapo kabla pia Mungu Hakukusudia kuinua upanga, bali wale walioinua upanga ndio waliuawa kwa upanga. Ilmuradi, hizi ni zama za ishara za kimbingu, sio zama za umwagaji damu. Wapumbavu kwa kutoa maelezo mabovu wakaidhihirisha sheria tukufu ya Mungu katika sura mbaya. Nguvu za kimbingu zilizomo ndani ya Islamu, zilikuwa hakuna katika dini nyingine yoyote. Islam haiuhitaji upanga hata kidogo.

Mwandishi

Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian.

23 Dhulkaada 1314 Hijri.

**Shairi la Bwana Munshi Gulabuddin Ruhtasi**

Allah, Allah, ilioje jaha na jalali ya karne ya kumi na nne, imejaaliwa kwa rehema ya Mungu fadhili na uzuri sana kiasi gani!

Ambamo mja mmoja wa Mungu ametumwa na Mungu, ili airudishe tena jamala ya Islam.

Yule ambaye habari ya ujaji wake aliitoa mtoaji habari mkweli, huyu mwenye heshima ameshuka kutoka mbinguni.

Makao yake ni Qadian, jina lake Ghulam Ahmad, kwa sababu yake Islam ikajiondolea mbali mavumbi yake.

Dini inaanza kujadidishwa kwa nguvu na bidii, mwangalieni mtu yeyote, kila mmoja anaongea habari hii hii.

Wenye njaa wameanza kushiba kwa vyakula vya kiroho, wenye kiu wakatosheka sana kwa mvua ya baraka.

Giza la shirk na bida'a lilianza kutoweka na uzuri na jamala ya Tauhidi sasa ikaanza kuonekana.

Siri nyingi zilizokuwa ufichoni za elimu itokayo kwa Mungu zikafunguka. Tukaona

mfano hai wa kashfi na miujiza.

Leo asili za wahyi na ufunuo zimejulikana wazi, siri ya usiku wa Mi'raji na hali ya Tuur imefunguka.

Imebainika leo kuwa Kurani ndio muujiza ulio hai, ulimwengu wote umekubali kuwa ni vigumu kukabiliana nayo.

Kilikatika kichwa cha kila mpinzani kwa upanga wa dalili, dini zingine nazo zikakanywa pia kwa hoja.

Siri za matabiri na za utume zimefunguka, umefahamika uteremsho wenye jalali wa Isa bin Mariamu.

Ikajulikana maana ya miujiza ya unabii, uteremko wa malaika, fadhili za Mungu zinazouteremkia moyo wa mwaminio.

Elimu nyepesi za usufii na siri za uwalii pia zimepata ufumbuzi, wote wakakubali kuwa miujiza pia siyo muhali.

Ilmuradi, matatizo mamia yaliyoshindikana yametatuliwa. Aliyeuliza swali moja, kapewa majibu kumi.

Enyi waadilifu, fikirini zama zilivyogeuka,

wanamsema Isa aliyeahidiwa kuwa kaja dajali.

Manabii na Mawalii huwa mfano wa kioo, huonekana daima sura yako mwenyewe ndani ya kioo.

Wenyewe hawana uwezo wa kuona kama popo, na wanaliaibisha jua lenye uzuri na jamala.

Elimu ya kidhahiri ndiyo pazia kuu, kwa elimu ya batini mtu hupata daima kukamilika.

Je mmesahau kisa cha Musa na Khidhri Khidhri alitenda mambo yaliyomshangaza Musa.

Mfuate Khidhri kwa imani ya kweli, Ewe Gulab, kama unataka kheri katika hali na kauli.

## Orodha ya Mapato ya Mchango kwa ajili ya kutengeneza Nyumba ya wageni, Kisima n.k.

Bw. Munshi Abdul Rahman, Mkuu wa Ofisi ya Generali, Kapurthala, Rupia 4

Bw. Maulawii Sayyid Ahsan wa Amroha, Rupia 4

Bw. Arab Haji Mahdi Baghdadi, Mgeni wa Madras, Rupia 50

Bw. Seth Abdul Rahman Haji Allah Rakha wa Madras, Rupia 50

Wake wa Bw. Fazalud Din wa Bhera, Rupia 50

Bw. Khairud Din wa Sikhwan karibu na Qadian, Rupia 1

Bw. Jalal Din Balani, Wilaya ya Gujrat, Rupia 5

Bw. Abdul Haq, Karanchi wala, Ludhiana, Rupia 5

Ibrahim Sulaiman Kampuni, Madras, Rupia 12

Bw. Seth Dalji Lalji, Madras, Rupia 50

Bw. Seth Saleh Muhammad Haji Allah Rakha, Madras, Rupia 18

Bw. Maulawii Sultan Mahmud, Madras, Rupia 20

Bw. Sheikh Muhammad Jan wa Wazirabad, Rupia 10

Bw. Imamud Din wa Sheikhwan karibu na Qadian, Rupia 1

Bw. Abdul Aziz Patwari wa Sheikhwan, Rupia 5

Bw. Khalifa Nurud Din na Bw. Allah Ditta wa Jammu, Rupia 15

Bw. Seth Ishak Ismail wa Bangalore, Rupia 15

Bw. Mirza Khuda Bakhsh, Mwalimu wa Bw. Nawwab wa Malir Kotla, Rupia 10

Mke wa Bw. Mirza aliyetajwa juu, Rupia 5

Bw. Sheikh Rahmatullah, mfanya biashara wa Lahore, Rupia 101 Anna 4

Bw. Munshi Karam Ilahi wa Mlima wa Simla, Rupia 2

Bw. Nawwab Khan, Mtoza ushuru wa Jhelum, Rupia 20

Bw. Nabii Bakhsh, Chifu wa Batala, Rupia 10

Bw. Muhammad Sadiq wa Sheikhwan karibu na Qadian, Rupia 1

Bw. Maula Bakhsh, mfanya biashara wa ngozi, Dinga, Wilaya Gujrat, Rupia 5

Bw. Muhammadud Din, mfanyabiashara wa viatu, Jammu, Rupia 1 Anna 12

Bw. Allah Ditta wa Jammu, Rupia 1

Bw. Sardar Samand Khan wa Jammu, Rupia 1 Anna 2

Bw. Qutbud Din, Kotla Fakir, Wilaya ya Jhelum, Rupia 5

Bw. Muhammad Shah, Kontrakta wa Jammu, Rupia 5

Bw. Maulawii Muhammad Sadiq wa Jammu, Anna 14 Paisa 2

Bw. Shadi Khan wa Sialkot, Rupia 120

Bw. Fazl Karim Ataa wa Jammu, Rupia 1

Bw. Mualawii Muhammad Akram wa Jammu, Anna 8

Bw. Khwaja Jamalud Din, B.A., wa Jammu, Rupia 8 Anna 2

Bw. Mistri Umar wa Jammu, Rupia 1 Anna 2

Bw. Mufti Fazl Ahmad wa Jammu, Anna 7 Paisa 1

Bw. Ghulam Rasul, mfanyabiashara, Calcatta, sasa katika Jammu, Rupia 5

Bw. Munshi Nabii Bakhsh wa Jammu, Rupia 1

Bw. Sheikh Masihullah wa Shahjahanpur, mpishi wa Msimamizi wa Mito, Multan, Rupia 4

Bw. Zainud Din Muhammad Ibrahim, Mhandisi wa Bombay, Rupia 15

Bw. Mahdi Husain wa Bombay, Rupia 2

Bw. Babu Chiraghud Din, Stesheni Masta wa Layyah, Rupia 2

Bw. Abdullah Khan, ndugu wa Mtoza ushuru, Jhelum, Rupia 10

Bw. Fazl Ilahi wa Kijiji cha Faizullah, karibu na Qadian, Rupia 2

Bw. Abdullah, Theh Ghulam Nabii, karibu na Qadian, Rupia 1

Bw. Abdul Khaliq, Mtililiaji, Amritsar, Rupia 2

Bw. Muhammad Ismail, Mfanyabiashara wa nguo za sufu,

Amritsar, Rupia 5

Mke wa Bw. Abul Aziz Patwari aliyetajwa nyuma, Rupia 2

Bw. Ghulam Husain, Stesheni Masta msaidizi wa Dina, Rupia 1

Bw. Wazirud Din, Mwalimu Mkuu, Sajanpur, Kangarah, Rupia 1

Bw. Fazlud Din, Qadhi Kot, Rupia 1

Mke wa Bw. Nabii Bakhsh mtililiaji wa Amritsar, Rupia 5

Mehar Sawan wa Sheikwan, Rupia 1

Bw. Sayyid Haamid Shah wa Sialkot, Rupia 10

Bw. Muhammadud Din, Konstebo, Rupia 8

Bw. Hakiim Muhammadud Din, Konstebo, Rupia 1

Bw. Sayyid Chiragh Shah, Rupia 1

Bw. Inayatullah, Rupia 1

Bw. Sayyid Amiir Ali Shah, Sajini wa daraja la kwanza, Rupia 5

Bw. Maulawii Qutbud Din wa Baddo Malhi, Rupia 1

Bw. Shah Rukund Din Ahmad Karha, Sajjada Nashin, Rupia 5

Bw. Mirza Niaz Beg, Msimamizi wa mito wilaya ya Multan, Rupia 20

Bw. Hafidh Abdul Rahman wa Layyah, Rupia 5

Bw. Maulawii Abdullah Khan, Rupia 1

Bw. Maulawii Mahmud Hasan Khan wa Patiala, Anna 8

Bw. Sheikh Karam Ilahi wa Patiala, Rupia 10

Bw. Hafidh Nur Muhammad wa Patiala, Rupia 1

Wana wa marehemu Dhahur Ali na mjukuu wa marehemu Akbar Ali, Anna 2

Bw. Sayyid Muhammad Ali wa Madras, Qila Sobha Singh, Rupia 1

Bw. Shamsud Din Muhammad Ibrahim, Bombay, Rupia 6

Bw. Nur Muhammad, Rupia 8

Bw. Mirza Fazl Beg Mukhtar wa Qasur, Rupia 5

Bw. Akbar Ali Shah wa Mojianwala, Wilaya ya Gujrat, Rupia 2

Bw. Hafidh Nur Muhammad, kijiji cha Faizullah, karibu na Qadian, Rupia 1

Bw. Ghulam Kadir wa Theh Ghulam Nabii, karibu na Qadian, Anna 2

Bw. Ghulam Muhammad wa Sheranwala Katrha, Amritsar, Rupia 1

Bw. Nabii Bakhsh, mtililiaji wa Amritsar, Rupia 20

Bw. Jamalud Din, Sheikhwan, Rupia 1

Bw. Khalifa Rashiidud Din, Daktari Mpasuaji msaidizi wa Chakrata, Rupia 5

Bw. Qadhi Ziaud Din wa Qadhi Kot, Rupia 1

Bw. Qadhi Fazalud Din, Anna 8

Bw. Sayyid Khasilat Ali Shah, Mkuu wa kituo cha polisi, Dinga, Rupia 15

Bw. Abul Aziz, mshonaji, Sialkot, Rupia 7

Mke na mama mzazi wa Bw. Shah, Rupia 4

Bw. Sheikh Ataa Muhammad, msimamizi mdogo wa ujenzi, Rupia 5

Bw. Maula Bakhsh Mfanyabiashara wa viatu, Sialkot, Rupia 2

Bw. Sayyid Muhammad, mfanyakazi katika Polisi, Sialkot, Anna 2

Bw. Fazl Din, Sonara wa Sialkot, Rupia 1

Bw. Muhammadud Din, mwandishi wa rufaa, Sialkot, Rupia 5

Bw. Qaadir Bakhsh wa Ludhiana, Rupia 8

Bw. Muhammad Akbar wa Batala, Rupia 10

Bw. Maulawii Ghulam Muhyid Din, mwalimu Nur Mahal, Rupia 1 Anna 4

Bw. Seth Musa wa Manipur, Asaam, Sadr Bazaar, Rupia 71

Bw. Munshi Aziz Ullah wa Sarhind, Postamasta Nadon Kangrah, Rupia 2

Bw. Sheikh Muhammad Husain wa Muradabad karani, Patiala, Rupia 8

Bw. Mustafa na Bw. Murtadha, Bw. Muhammad Afzal na Bw. Muhammad A'zam, Rupia 2

Bw. Sheikh Abdus Samad, mwalimu wa Sanor, Anna 4

Bw. Maulawii Karamud Din, Naibu Mwalimu, Qila Sobha Singh, Rupia 1

Bw. Shihabud Din Shamsud Din wa Bombay, Rupia 4

Bw. Fateh Muhammad Khan Buzdar wa Layyah, Dera Ismail Khan, Rupia 5

Bw. Daktari Burhe Khan wa Qasur, Rupia 15

Bw. Maulawii Muhammad Qari Imamu wa Msikiti Kassaban, Jhelum, Rupia 2

Bw.Chiragh Ali, Theh Ghulam Nabii karibu na Qadian, Rupia 1

Bw. Nizamud Din, karibu na Qadian, Anna 2

Bw. Gulabud Din, Thalwal, Jammu, Rupia 2

Mama mzazi wa Bw. Abdul Aziz Patwari wa Sheikhwan, Rupia 2

Bw. Shahidain, Steshenimasta wa Dina, Wilaya ya Jhelum, Rupia 8

Bw. Muhammad Khan wa Kapurthala, Rupia 8

Bw. Qadhi Muhammad Yusuf wa Qadhi Kot, Rupia 2

Bw. Nur Muhammad Darweshke, Rupia 1

Bw. Ghulam Ilahi, mwashi wa Behra, ndugu zake na wenye mtaa, Rupia 2 Anna 12

Mke wa Bw. Abdul Aziz aliyetajwa juu, Rupia 8

Bw. Munshi Allah Ditta Khan wa Sialkot, Rupia 5

Bw. Hakiim Ahmadud Din, Sialkot, Rupia 1

Bw. Sayyid Nawab Shah, mwalimu, Sialkot, Rupia 2

Bw. Nizamud Din, mwashi, Sialkot, Rupia 5 Anna 11

Bw. Gulab Khan, msimamizi wa ujenzi, Sialkot, Rupia 5 Anna 11

Bw. Ali Gohar Khan, Branch Postamasta Jalandhar, Rupia 5

Bw. Munshi Rustam Ali, Inspekta wa Korti, Gurdaspur, Rupia 25

Bw. Ghulam Rasul Khan wa Ghazipur, Rupia 2

Bw. Babu Ghulam Muhyid Din, Phalor, Wilaya ya Jalandhar, Rupia 2

Bw. Mulla Abdur Rahim wa Ghazni, Rupia 2

Bw. Sharfud Din, Kotla Fakir, Wilayani Jhelum, Rupia 4

Bw. Daktari Abdul Hakiim wa Patiala, Rupia 10

Bw. Sheikh Abdullah na Bw. Ibadullah wa Patiala, Rupia 10 Anna 12

Bw. Maulawii Yusuf wa Sanor, Anna 12

Bw. Hafidh Adhim Bakhsh, Anna 2

Bw. Masta Ghulam Muhammad wa Sialkot, Rupia 1

Bw. Maulawii Abdul Karim wa Sialkot, Rupia 5

Bw. Babu Ataa Muhammad, overseer wa Baraza la mji, Sialkot, Rupia 5

Watu mbalimbali wa Sialkot, Rupia 2

Bw. Qurban Ali, mwashi, Platuni Na 43, Calcutta, Rupia 2

Bw. Munshi Abdul Rahim, Ofisi ya telegramu, Manipur, Rupia 5

Bw. Abdul Ghaffar, mwashi, Platuni Na 44, Danapur, Rupia 2

Bw. Bisharat Mian, Platuni Na 44 Manipur, Rupia 2

Bw. Pir Faiz Ali wa Manipur, Rupia 8

Bw. Sarwar Khan, Jemadari Manipur, Rupia 2

Bw. Khanda, Jemadari Gurdaspur, Rupia 2

Bw. La'l Din, Manipur, Rupia 1

Bw. Hussain Bakhsh, Barakpur, Ardali Bazar, Rupia 5

Bw. Shabrani Banarasi, Rupia 2

Bw. Maulawii Ghulam Ahmad wa Manipur, Azizul Waidhiin, Rupia 30

Mke wa Maulawii aliyetajwa juu, Rupia 5

Bw. Muhammadud Din, Patwari, Balani, Wilaya ya Gujrat, Rupia 1

Bw. Khwaja Kamalud Din, B.A., Rupia 5

Bw. Mufti Muhammad Sadiq wa Bhera, Rupia 10

Bw. Sher Muhammad wa Bakhar, Rupia 2

Bw. Babu Maula Bakhsh wa Lahore, Rupia 1

Zaidi ya haya kuna majina mengine pia yatakayochapishwa katika toleo la pili.

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ [52]

## Mawasiliano Ya Kimaandishi

Katika kipindi hiki mawasiliano ya kimaandishi yaliyofanyika baina yangu na mheshimiwa Khwaja Ghulam Farid Chishti, Mwongozi wa Mtawala wa Bahawalpur, barua zile za pande zote mbili zinachapishwa kwa nia tu ya kuwanufaisha watu wote, huenda mtu yeyote wa Mungu akafaidika nazo وَاِنَّمَا الۡاَعۡمَالُ بِالنِّیَّاتِ [53].

## Barua ile ya kwanza ya Bwana Khwaja iliyochapishwa ndani ya nyongeza ya Anjame Atham kwenye uk. 39.

Kutoka kwa fakiri wa Mlango wa Allah, Ghulam Fariid Sajjadanashin, kwenda kwa Bwana Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian.

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ اَلۡحَمۡدُ لِلّٰہِ رَبِّ الۡاَرۡبَابِ وَالصَّلٰوۃُ عَلٰی رَسُوۡلِہٖ
الشَّفِیۡعِ بِیَوۡمِ الۡحِسَابِ وَ عَلٰی اٰلِہٖ وَ الۡاَصۡحَابِ وَالسَّلَامُ عَلَیۡکُمۡ وَ عَلٰی مَنِ
اجۡتَھَدَ وَ اَصَابَ اَمَّا بَعۡدُ قَدۡ اَرۡسَلۡتَ اِلَیَّ الۡکِتَابَ وَبِہٖ دَعَوۡتَ اِلَی الۡمُبَاھَلَۃِ
وَطَالَبۡتَ بِالۡجَوَابِ وَاِنِّیۡ وَاِنۡ کُنۡتُ عَدِیۡمَ الۡفُرۡصَۃِ وَلٰکِنۡ رَّاَیۡتُہٗ جُزۡءَہٗ مِنۡ
حُسۡنِ الۡخِطَابِ وَسَوۡقِ الۡعِتَابِ اِعۡلَمۡ یَا اَعَزَّ الۡاَحۡبَابِ اَنِّیۡ مِنۡ بُدُوِّ حَالِکَ

[52] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

[53] Na kwa hakika amali huitegemea nia.

وَاقِفٌ عَلٰى مَقَامِ تَعْظِيْمِكَ لِنَيْلِ الثَّوَابِ وَمَا جَرَتْ عَلٰى لِسَانِيْ كَلِمَةٌ فِيْ
حَقِّكَ اِلَّا بِالتَّبْجِيْلِ وَرِعَايَةِ الْاٰدَابِ وَالْاٰنَ اَطَّلِعُ لَكَ بِاَنِّيْ مُعْتَرِفٌ بِصَلَاحِ
حَالِكَ بِلَا ارْتِيَابٍ وَ مُوْقِنٌ بِاَنَّكَ مِنْ عِبَادِاللهِ الصّٰلِحِيْنَ۔ وَ فِيْ سَعْيِكَ
الْمَشْكُوْرِ مَثَابٌ وَقَدْ اُوْتِيْتَ الْفَضْلَ مِنَ الْمَلِكِ الْوَهَّابِ وَلَكَ اَنْ تَسْئَلَ
مِنَ اللهِ تَعَالٰى خَيْرَ عَاقِبَتِيْ وَاَدْعُوْلَكُمْ حُسْنَ مَاٰبٍ وَلَوْلَا خَوْفُ الْاِطْنَابِ
لَازْدَدْتُّ فِي الْخِطَابِ۔ وَالسَّلَامُ عَلٰى مَنْ سَلَكَ سَبِيْلَ الصَّوَابِ۔ فَقَطْ
٢٧ رَجَبْ ١٣١٤ھ مِنْ مَقَامِ چَاچڑَان

فقیر غلام فرید
خادم الفقرا ١٣٠١
مہر

Tafsiri: Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu. Sifa zote njema zinamhusu Mwenyezi Mungu Aliye Mola wa mola wote. Na baraka na amani ziwe juu ya Mjumbe aliye mwombezi wa Siku ya Kiyama, na juu ya ali zake na masahaba wote, na amani iwe juu yako na juu ya kila mmoja ajitahidiye katika njia iliyo sawa. Baada ya hayo, ibainike kuwa kimenifikia kitabu chako ambamo yameombwa majibu kwa ajili ya mubahala. Ingawa nilikuwa sina fursa, hata hivyo nimeisoma sehemu moja ya kitabu hicho kilichokuwa na maneno mema na pia maneno ya kusuta. Basi, Ewe uliye mpendwa sana kuliko kila mpendwa, ufahamu kuwa tangu mwanzo nipo katika hali ya kukuheshimu ili nipate thawabu. Na kamwe ulimi wangu haujatoa neno

lolote kukuhusu wewe isipokuwa neno la heshima na staha na madaha na adabu. Na sasa ninakuarifu kuwa bila shaka ninaikiri hali yako njema na nina yakini kuwa u miongoni mwa waja wema wa Mungu, na juhudi yako mbele ya Mungu ni yenye kushukuriwa ambayo utapata ujira wake. Na fadhili za Mungu Msamehevu Mfalme ziko kwako. Niombee mwisho mwema, nami nakuombea mwisho mwema na bora. Kama nisingekuwa na hofu ya urefu ningeandika zaidi.

وَالسَّلَامُ عَلٰى مَنْ سَلَكَ سَبِيْلَ الصَّوَابِ[54]

Tarehe 27 Rajab, 1314 Hijri, kutoka Chacharan.

## Jawabu la barua

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ نَحْمَدُهٗ وَنُصَلِّيْ عَلٰى رَسُوْلِهِ الْكَرِيْمِ
مِنْ عَبْدِ اللّٰهِ الْاَحَدِ غُلَام اَحْمَدْ عَافَاهُ اللّٰهِ وَ اَيَّدَهُ اِلَى الشَّيْخ الْكَرِيْمِ
السَّعِيْدِ حِبِّيْ فِي اللّٰهِ غُلَام فَرِيْد۔ اَلسَّلَامُ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَةُ اللّٰهِ وَبَرَكَاتُهٗ۔
اَمَّا بَعْدُ فَاعْلَمْ اَيُّهَا الْعَبْدُ الصَّالِحُ قَدْ بَلَغَنِيْ مِنْكَ مَكْتُوْبٌ ضُمِّخَ بِعِطْرِ
الْاِخْلَاصِ وَالْمَحَبَّةِ وَ كُتِبَ بِاَنَامِلِ الْحُبِّ وَالْاُلْفَةِ جَزَاكَ اللّٰهُ خَيْرَ الْجَزَاءِ وَ
حَفِظَكَ مِنْ كُلِّ اَنْوَاعِ الْبَلَاءِ اِنِّيْ وَجَدْتُّ رِيْحَ التَّقْوٰى فِيْ كَلِمٰتِكَ فَمَا اَضْوَعَ
رَيَّاكَ وَمَا اَحْسَنَ نَمُوْذَجَ نَفَحَاتِكَ وَ قَدْ اَخْبَرَ النَّبِيُّ صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمْ
فِيْ اَمْرِيْ وَ اَثْنٰى عَلٰى اَحْبَابِيْ وَ زُمَرِيْ وَقَالَ لَا يُصَدِّقُهٗ اِلَّا صَالِحٌ وَلَا يُكَذِّبُهٗ
اِلَّا فَاسِقٌ فَشَرَفًا لَكَ بِبِشَارَةِ الْمُصْطَفٰى وَوَاهًا لَكَ مِنَ الرَّبِّ الْاَعْلٰى

54 Na Salaam iwe juu ya anayefuata njia iliyo sawa

وَمَنْ تَوَاضَعَ لِلّٰهِ فَقَدْ رُفِعَ وَمَنِ اسْتَكْبَرَ فَرُدَّ وَدُفِعَ وَاِنِّيْ مَازِلْتُ مُنْذُ رَأَيْتُ
كِتَابَكَ وَ اٰنَسْتُ اَخْلَاقَكَ وَ آدَابَكَ اَدْعُوْلَكَ فِي الْحَضْرَةِ وَاَسْئَلُ اللّٰهَ اَنْ
يَتُوْبَ عَلَيْكَ بِاَنْوَاعِ الرَّحْمَةِ وَ قَدْ سَرَّنِيْ حُسْنُ صِفَاتِكَ وَ رَزَانَةُ حَصَاتِكَ
وَ عَلِمْتُ اَنَّكَ خُلِقْتَ مِنْ طِيْنَةِ الْحُرِّيَّةِ وَ اُعْطِيْتَ مَكَارِمَ السَّجِيَّةِ وَ اَحِنُّ
اِلٰى لِقَائِكَ بِهَوَى الْجِنَانِ اِنْ كَانَ قَدْرُ الرَّحْمٰنِ وَ قَدْ سَمِعْتُ بَعْضَ خَصَائِصِ
نَبَاهَتِكَ وَمَاٰثِرَ وَجَاهَتِكَ مِنْ مُخْلِصِيْ اَلْحَكِيْمِ الْمَوْلَوِيِّ نُوْرِ الدِّيْنِ
فَالْاٰنَ زَادَ مَكْتُوْبُكَ يَقِيْنًا عَلَى الْيَقِيْنِ وَصَارَ الْكِبَرُ عِيَانًا وَالظَّنُّ بُرْهَانًا
فَادْعُوا اللّٰهَ سُبْحَانَهُ اَنْ يَبْقٰى مَجْدُكَ وَبُنْيَانُهُ وَ يُحِيْطَ عَلَيْكَ رَحْمَةٌ وَّ غُفْرَانُهُ
وَ كُنْتُ قُلْتُ لِلنَّاسِ اِنَّكَ لَا تَلْوِيْ عِذَارَكَ وَلَا تُظْهِرُ اِنْكَارَكَ فَاَبْشَرْتُ
بِاَنَّ كَلِمَتِيْ قَدْ تَمَّتْ وَ اَنَّ فِرَاسَتِيْ مَا اَخْطَأَتْ وَ رَغَّبَنِيْ خُلُقُكَ فِيْ اَنْ اَفُوْزَ
بِمَرْاٰكَ وَ اُسَرَّ بِلُقْيَاكَ فَاَرْجُوْ اَنْ تَسُرَّنِيْ بِالْمَكْتُوْبَاتِ حَتّٰى تَجِيْءَ مِنَ اللّٰهِ
وَقْتُ الْمُلَاقَاتِ وَالْاٰنَ اُرْسِلُ اِلَيْكَ مَعَ مَكْتُوْبِيْ هٰذَا ضَمِيْمَةَ كِتَابِيْ كَمَا
اَرْسَلْتُهُ اِلٰى اَحْبَابِيْ وَفِيْهَا ذِكْرُكَ وَذِكْرُ مَكْتُوْبِكَ وَ اَرْجُوْ اَنْ تَقْرَءَهَا وَلَوْ
كَانَ حَرَجٌ فِيْ بَعْضِ خُطُوْبِكَ

وَالسَّلَامُ عَلَيْكَ وَعَلٰى اَعِزَّتِكَ وَشُعُوْبِكَ. فَقَطْ مِنْ قَادِيَان..

(Tafsiri): Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema Mwingi wa ukarimu.

Twamhimidia Yeye, na kumsalia Mtume Wake Mtukufu[saw].

Kutoka kwa mtumishi wa Mungu Aliye wa Pekee, Ghulam Ahmad, Allah Amhifadhi na Amsaidie, kwenda kwa Sheikh mheshimiwa mwenye bahati njema, mpendwa wangu kwa ajili ya Mungu, Ghulam Farid. Assalamu alaikum wa Rahmatullahi wa Barakaatuh.

Amani na rehema na baraka za Allah ziwe kwako,

Amma baad, fahamu, Ewe mja mwema, kwamba imeniwasilia barua kutoka kwako iliyopakwa uturi wa ikhlasi na mahaba, ambayo imeandikwa kwa vyanda vya huba na Upendo. Allah Akujaalie malipo bora na Akuhifadhi na kila aina ya balaa. Nimepata harufu nzuri ya ucha Mungu ndani ya maneno yako. Harufu yako njema imeenea sana namna gani! Na mfano mzuiri namna gani wa lafudhi zako!! Nabii s.a.w. alitoa habari kuhusiana nami na akawasifu marafiki zangu na kundi langu na akasema hakuna atakayemsadikisha isipokuwa mwema na hakuna atakayemkadhibisha isipokuwa fasiki. Hivyo ni heshima kwako kwa sababu ya bishara ya Mteule[saw] na hongera kwako kutoka Mola Aliye juu. Na yule aliyenyenyekea kwa ajili ya Allah, akanyanyuliwa, na yule aliyefanya kiburi, akakataliwa na kufukuziliwa mbali. Na tangu niione barua yako na kuzifahamu khulka zako na adabu zako, naendelea kukuombea kwa Mwenyezi Mungu, na ninamwomba Allah kuwa Aelekee kwako kwa rehema za aina aina. Na sifa zako bora na uzito wa rai zako zimenifurahisha, nami nimefahamu kuwa wewe umejaaliwa tabia iliyo huru na umejaaliwa khulka bora, na nina shauku kubwa moyoni ya kukutana nawe, laiti Mwenyezi Mungu

Angelifanikisha jambo hili. Mimi nimeshasikia toka kwa rafiki yangu mwaminifu, Bwana Hakim Maulawii Nurud Din, kuhusiana na baadhi ya sifa za busara zako na matendo yenye sifa ya jaha yako. Na sasa, barua yako imeongeza yakini juu ya yakini, na habari imekuwa kama ni ya kujionea kwa macho na dhana ikawa uhakikisho. Hivyo, ninamwomba Allah Mtakatifu utukufu wako uendelee na kuimarika na rehema Yake na msamaha Wake ukuzingire. Nami nilikuwa nikiwaambia watu kuwa wewe hutaasi wala hutakataa. Basi, nimefurahi kuwa neno langu limetimia na busara yangu haikukosea, na khulka zako zimenivutia kwamba nipate kukuona na nifurahi kukutana nawe. Hivyo, ninatumai kwamba utanifurahisha kwa barua zako hadi uwadie kutoka kwa Mungu wakati wa kukutana nawe. Na sasa pamoja na barua yangu hii nakutumia nyongeza ya kitabu changu kama nilivyowatumia marafiki zangu, na humo zimetajwa habari zako na habari za barua yako, nami natumai kwamba utaisoma hata kama kwa kuzivunja shughuli zako muhimu. Na salamu ziwe kwako na kwa wapendwa wako na wenzako. Basi. Kutoka Qadian.

## Barua ya pili ya Khwaja Sahib

Kwa Janabi Bwana Mirza, mheshimiwa mwenye mema mengi sana, mwenye sifa nyingi mno, muhtaramu, muadhamu, Mirza Ghulam Ahmad, mteule wa Mwenyezi Mungu Mmoja, Mungu Awanufaishe watu kwa kubaki kwake na Anifurahishe kwa kutana naye na Amneemeshe kwa neema zake. Baada ya kutoa salamu iliyo Suna ya Kiislamu, kwa shauku kubwa naomba dua kwa kutukzwa jina na kunyanyuliwa wazi wazi cheo. Imewasili barua yako pamoja na kitabu ulichotuma, iliyojaa kipeo cha huba, iliyokuwa na mahaba na ukarimu, iliyosababisha kuchangamsha na kufurahisha sana mno. Haikufichika kwamba mimi mnyonge, kwa sababu ya mazoea na tabia ya asili sipendi kulaumiana na kujiingiza katika medani ya mahojiano na mijaldala ya bure ili kujikinga na mabishano yasiyo na maana. Kwani, maelekeo ya utashi wa watu wengi yanawazuia wasiutafute ukweli, na tabia ya chuku inazidisha ujahili ndani ya uchunguzi. Pamoja na hayo, hao wanayategemea mambo yasiyo imara, na pasipo kufahamu wanaanzisha makelele, na mavumbi ya ujahili yanayozuka kwa upepo wa ujinga huwaangukia vichwani mwao wenyewe, waila natija

ya matendo huitegemea nia sahihi, na kinaya cha kina chabainika kwa kutoa maelezo. Miongoni mwa baadhi ya wataalamu wa sehemu hii wa zama hizi wametaka niwajibu kwa nini namfikiria mtu (yaani wewe) kuwa mwema ambaye juu yake Maulamaa wameafikiana kuwa mambo fulani yamethibitika ndani yake, na kwa nini unayo dhana njema juu yake. Kwa kuwa maandiko yao yamejaa jadhba kubwa na mpangilio wao wa maneno una moto kama wa radi, kadhalika maandiko yao yanashuhudia mahangaiko yao ya mioyo, ajuaje sana nia ya mtu ni Mwenyezi Mungu peke yake, na kumdhania vibaya mtu yeyote si njia ya watu wema, wala haijuzu kumfahamu mtu kuwa mnafiki au mwenye kujitii nafsi, bila uchunguzi mimi naona uzito kuwadhaina vibaya. Kwani kama wanayo nia safi, basi kosa lao litachukuliwa kuwa ni kosa la ijtihadi. Waila hakika yenywe ni kuwa kadri walivyopata habari zako wenye kutega masikio kusikiliza maneno ya huba, mahaba yako yamezidi moyoni na ikhlasi imeongezeka ambayo mimi nilikuwa nayo. Ninaomba kwamba kwa hisani ya Mungu izuke sababu nzuri na idhihirika saa ile kwamba liondoke pazia la umbali wa kimweli na hijabu ya masafa marefu sana. Na itakuwa ni hisani yako, kama utanitumia makala yako ile iliyosomwa

katika Mkutano wa Dini.

Wassalamu. Salaam sana kwa Maulawii Nuruddin na Sahibzada Sirajul Haq pia.

Mwandishi: Fakiri Ghulam Farid Alchishti Annidhami, kutoka Chachrhan Sharif.

27 Shabani 1314 Hijriyya Nabawiyya. (Muhuri)

**Jawabu**

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ نَحۡمَدُہٗ وَ نُصَلِّیۡ عَلٰی رَسُوۡلِہِ الۡکَرِیۡمِ

Kwa Hadhrat mheshimiwa Sheikh, mhashamu, jalili sharifu, mwenye bahati njema, mpendwa wangu kwa Allah, Bwana Ghulam Farid, Mungu Awe pamoja naye, Amridhie na Amridhishe.

Assalamu alaikum wa rahmatullahi wa barakatuh

Amma baad, barua yako ya kupendeza yenye heshima imewasili iliyonifurahisha sana, ambayo inalingana kabisa na aya hii ya Kurani Tukufu:

اِنِّیۡ لَاَجِدُ رِیۡحَ یُوۡسُفَ لَوۡ لَاۤ اَنۡ تُفَنِّدُوۡنِ [55]

Miongoni mwa maelfu ya wanazuoni na watu wema,

[55] Yuusuf, 12:95

nimehisi kutoka kwa maneno yako harufu njema ya urafiki. Namshukuru Mungu kwamba katika ardhi hii hawakukosekana waja wema wa aina hii ambao hawaiogopi lawama ya yeyote mwenye kulaumu, na wamejaaliwa nuru na busara kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Basi, tabia yako safi sahihi yakuvutia kwenye ukweli, na roho mtakatifu hukusaidia katika kudhihirisha haki. Alhamdu lillahi, tena Alhamdu lillahi, kwamba tumekukuta unayo mambo hayo.

Ewe ndugu mheshimiwa, masheikh wa zama hizi wananielekea kwa kiasi kidogo sana, na fitina zinazuka kila upande. Hapo kabla mpenzi wangu kwa Allah, Haji Munshi Ahmad Jaan wa Ludhiana aliye pia mwandishi wa kitabu cha "Tibbe Ruhani" akawa na itikadi njema kwangu kwa mahaba na ikhlasi sana, na baadhi ya wafuasi wake wabovu wakasema sana kumhusu yeye kuwa juu ya kuwa mtawa na maarufu ameangukia wapi! Yeye alipopata kusikia maneno haya, aliwakusanya wafuasi wake katika kikao fulani na akasema, "Uhakika wenyewe ni huu ya kwamba mimi nimekiona kitu msichokiona. Kwa hiyo, kama mnataka kuvunja uhusiano nami, ni vizuri sana, hata mimi siujali uhusiano kama huu." Kwa kusikia maneno yake haya, wafuasi wake wa kweli wakaanza kulia na wakaonyesha ikhlasi wasiyokuwa nayo

hapo kabla. Yeye alipokutana nami, alisema "Mimi nimepatwa na tatizo la ajabu. Nilifungu nia imara kwamba kama wataachana nami, basi nitawaacha. Lakini mambo yakawa kinyume. Hao wakala kiapo kuwa watanitolea huduma wasizotolea hapo kabla. Mja huyo alifariki dunia aliporudi baada ya kuhiji. Yeye aliwasihi mara kwa mara ndugu zake na jamaa zake wa karibu kuwa daima wawe na uhusiano wa upendo nami. Wakati wa kunuia kwenda kuhiji, aliniandikia kwamba mimi nasikitika sana ya kwamba nimepata sehemu kidogo sana ya zama zako, na umri wangu umepotea katika mambo ya bure. Katika ukoo wake, mwanaye na wanawake kwa wanaume wote waliufuata wasia wake na wakafanya baiati yangu. Na wazao wa mja huyo wakaacha kukaa Ludhiana, wanaishi hapa Qadian tangu muda mrefu.

Kuna mja mwingine ambaye ni Pir Sahibul 'Alam (mwenye bendera). Yeye aliona ndoto kuhusiana nami na baada ya kupata uthibitisho kutoka kwa Mtume[saw], akatoa ushuhuda juu yangu katika kikao kikubwa sana, na akaniandikia barua ambayo pengine umeiona ndani ya Nyongeza ya kitabu Anjame Atham.

Idadi ya wafuasi wangu bado haijafikia kiwango

kile Alichonidhihirishia Mola wangu. Nafikiri hivi sasa idadi ya wafuasi wangu ni elfu nane, wawili au watatu wanaweza kupungua au kuzidi.

Ewe muadhamu na mheshimiwa, silsila hii ni silsila ya Mungu, na ni jengo lililojengwa na mkono wa Mungu Mweza Anayeonyesha siku zote mambo ya ajabu. Naye Haulizwi kuhusu kazi zake ya kwamba kwa nini Amefanya hivyo. Yu Mmiliki, Hufanya Apendavyo. Mbingu na ardhi vinatetemeka kwa hofu yake, na malaika hutetemeka kwa haiba Yake. Yeye ameniita jina Adam katika ufunuo Wake na kusema اَرَدْتُ اَنْ اَسْتَخْلِفَ فَخَلَقْتُ اٰدَمَ . Kwa sababu alijua kuwa mimi pia nitaletewa lawama hii اَتَجْعَلُ فِيْهَا مَنْ يُّفْسِدُ فِيْهَا basi, yeyote anayeniamini ni malaika, sio binadamu, na yule anayenikataa ni Iblisi sio mtu. Hiyo ni kauli ya Mwenyezi Mungu, siyo kauli yangu. فَطُوْبٰى لِلَّذِيْنَ اَحَبُّوْا وَمَا عَادُوْنِيْ وَصَافَوْنِيْ وَمَا اٰذَوْنِيْ وَقَبِلُوْنِيْ وَمَا رَدُّوْنِيْ اُولٰٓئِكَ عَلَيْهِمْ صَلَوَاتُ اللهِ وَاُولٰٓئِكَ هُمُ الْمُهْتَدُوْنَ۔ Na ile nakala ya makala uliyotaka iliyosomwa katika Mkutano wa Dini, sababu ya kuchelewa kutumwa ni hii ya kwamba nilikuwa nikisubiri kupokea sehemu ya makala iliyokwisha chapwa ili nikupelekee. Basi, leo imenifikia sehemu yake moja ambayo ninakutumia. Na inshaallah, siku za usoni, kila mara nitakapopata sehemu zake nyingine nitaendelea kukutumia. Kupendwa kwa

makala hii kunabainika kutokana na jambo hili ya kwamba gazeti la serikali, ambalo haliijali habari ya kawaida bali huchapisha tu habari zile zilizo muhimu, hilo nalo limeisifu makala hii sana hata kuieleza kuwa ni mwujiza. Gazeti la Civil Military laandika kuwa makala hii iliposomwa, watu wote wakatega masikio na kusikia kwa mshangao wa hali ya juu sana. Na pia likaandika kuwa makala hii ilizishinda makala nyingine zote, bali likasema kwamba makala nyingine hazikuwa na thamani yoyote mbele ya makala hii. Basi, hii ni fadhili ya Mungu ya kwamba kalba ya kutokea tukio hilo, Yeye alinipasha habari mapema kwa ufunuo Wake na maneno yake, nami pia nikaeneza tangazo hili la Mungu mapema kwa njia ya kipeperushi. Basi, adhama ya tukio hili ikawa nuru juu ya nuru. Hivyo, tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa jambo hili.

Kuhusiana na malalamiko yote uliyoyaandika juu ya wanazuoni, niseme nini au niandike nini? Kesi yangu na yao iko mbinguni. Kama mimi ni mwongo, na ni mzushi katika elimu ya Mwenyezi Mungu Mwenye heshima, na madai yangu ni uongo, hiana na ulaghai, hapo hakuna adui wangu mkubwa kuliko Mungu. Yeye haraka sana Ataning'olea mbali na kuisambaratisha Jumuiya yangu, kwani Yeye

Hamwachi mzushi akae katika hali ya amani. Lakini kama mimi nimetokana naye na ni kutoka kwake na nimekuja kwa amri yake, na tena sina uhaini wowote katika mambo yangu, hapo hapana shaka Atawafanya watu wanisaidie kama inavyoendelea suna Yake tangu zamani kuwasaidia wakweli. Mimi siogopi laana ya watu hawa; laana ya asili ni ile inayotokea mbinguni. Na kama laana siyo kutoka mbinguni basi, laana ya watu ni jambo rahisi ambalo hakuna mkweli aliyesalimika nayo. Lakini wewe nakuombea kwa Mungu Mwenye enzi, uliyewafukuzilia mbali wapinzani wangu kwa sababu ya tabia yako njema, nitamwomba Mwenyezi Mungu. Basi, Ewe mpendwa wangu, Mungu Awe pamoja nawe, na mwisho wako uwe wenye kusifika.

جَزَاكَ اللهُ خَيْرًا الْجَزَاءِ وَاَحْسَنَ اِلَيْكَ فِي الدُّنْيَا وَالْعُقْبٰى وَكَانَ مَعَكَ اَيْنَمَا كُنْتَ وَاَدْخَلَكَ اللهُ فِي عِبَادِهِ الْمَحْبُوْبِيْنَ۔ آمِينَ

## Shairi la Kiajemi

Ewe mtu wa pekee wa zama hizi katika ukweli na utakaso, Awe pamoja nawe Yule Ambaye jina lake ni Mungu.

Ikunyeshe mvua ya rehema za Yule Rafiki wa tangu azali, na iendelee kung'aa nuru ya Mpendwa wa tangu azali.

Ewe mwanadamu mwenye tabia njema, roho yangu imekuridha. Katika zama hizi za kuadimika watu wenye vipaji nimekukuta wewe pekee u mwanamume.

Kwa hakika binadamu wa kweli huwa wachache, ingawa kuonekana wote waonekana kuwa ni binadamu.

Ewe yule ambaye mwelekeo wa huba yangu uko kwako, ninapata harufu njema ya upendo kutoka kwa mtaa wako.

Hakuna yeyote miongoni mwa watu hawa aliyetuelekea. Jambo hili lilikuwemo tu ndani ya kisimati chako, Ewe mtu mwenye bahati njema.

Watu hawa kila wakati wanitaja kwa kunilaani, na huendelea kuniudhi kwa dhuluma na ujeuri.

Mtu hawi Siddiki machoni mwa Mungu hadi awe kafiri machoni mwa wengine.

Waliniita kuwa kafiri, dajali na mlaaniwa, na kila dhalili akanivizia kuniua.

Waangalie wana-Sarakasi jinsi wanavyo-rukaruka, hao kwa kusudi wanajichezea tu

uhai wao.

Kumsema mwaminio kuwa ni kafiri ni jambo la hatari sana kwa mwenye akili.

Kwani, kukufurisha pasipo haki kwamwangukia kichwani mwenye kukufurisha.

Mpumbavu yule aliyazama ndani ya kufuru iliyojificha, anapigia kelele za hovyo kufuru ya wengine.

Kama angekuwa na habari ya ukafiri wake wa ndani, basi angejiona kuwa mbaya sana.

Tangu watu waliponitenga na kaumu yangu, wamejaribu sana namna ngapi kunikufurisha.

Wakanizushia uongo mbele ya kila mtu, na wakapiga domo kwa hiana.

Ili mtu yeyote ateleze kutokana na uzushi huu, na mtu wa kawaida anifahamu kuwa mimi ni kafiri.

Waliibua fitina katika njia yetu, na wakala njama kwa kuungana na Wakristo.

Wakasema kuwa mimi ni kafiri, kutokana na ujahili na uadui. Laiti kusingekuwepo na kipofu yeyote kiasi hiki duniani.

Ubahili na ujinga ukazidisha uadui, na chuki ikalipuka na kuyapofusha macho yao yote mawili.

Tu Waislamu kwa fadhili za Mungu, na Muhammad[saw] ndiye Imam na kiongozi wetu.

Sisi tumezaliwa ndani ya dini hii, na tutaondoka dunia tukiwa na dini hii hii.

Kitabu kile cha Mungu kinachoitwa Kurani, mvinyo yetu ya maarifa imetokana na bilauri hii hii.

Mtume yule aitwaye Muhammad[saw], tumeshikamana naye daima dumu dawamu.

Penzi lake liliingia ndani ya mwili wetu pamoja na maziwa ya mama, nalo likawa uhai na litatoka nje likiwa pamoja na uhai tu.

Yeye ndiye mbora wa mitume na mbora wa viumbe, na unabii wa kila aina umekamilika kwake.

Maji yoyote yale tunayanywa kwa kuchukua kutoka kwake, yeyote aliyezima kiu, ameizima kutoka kwake.

Ule wahyi na ufunuo unaotuteremkia, hautokani nasi, bali hutokea huko huko.

Kila mwanga na kila ukamilifu twapata kutoka kwake, haiwezekani kukutana na Mpendwa wa tangu azali bila ya kupitia kwake.

Imo ndani ya asili yetu kufuata kila agizo lake, chochote asemacho twakiamini kikamilifu.

Yale yote aliyosema Mtume huyo wa Mola wa watu kuhusiana na malaika na hali za akhera,

Yametoka kwa Mungu Mmoja, na mwenye kuyakataa anastahili kupata laana.

Miujiza yake yote ni ya kweli na sahihi, mwenye kuikataa ni mwenye kuteremkiwa na laana ya Mungu.

Miujiza ya manabii wote wa hapo kabla ambayo imetajwa kwa uwazi kabisa ndani ya Kurani,

Yote hiyo tunaiaamini kwa moyo wote, na aikataaye ndiye miongoni mwa wenye bahati mbaya.

Kukaa mbali hata hatua moja na kitabu hicho chenye nuru, ni ukafiri kwetu na hasara na ni maangamio.

Lakini, watu dhalili hawana habari ya uhakika wa Kurani Tukufu, kila moyo hauzitambui siri

zake.

Maadamu mtafuta haki hajitakasi batini yake, na maadamu penzi la Yule Mpendwa Asiye na mfano halina harara moyoni mwake,

Anawezaje yeyote kuzifahamu siri za Kurani Tukufu. Kwa kuifahamu nuru, yahitajika kuwa na nuru nyingi ya batini.

Hii si kauli yangu, bali Kurani pia imenena kwamba kuifahamu Kurani kuna sharti ya kujitakasa.

Kama kila mtu angeweza kuifahamu mwenyewe Kurani Tukufu basi kwa nini Mungu Alizidisha sharti ya kujitakasa.

Yule tu anaweza kuitambua nuru ambaye mwenyewe amekuwa nuru na amekuwa mbali na mapazia ya uasi.

Vipofu wote hawa wanaonikufurisha kwa yakini hawana habari na nuru ya Kurani,

Na hawazielewi siri za maneno hayo, ni wapuuzi, wabovu na wasiopevuka.

Mikononi mwao hamna chochote zaidi ya mfupa, na vichwani mwao hamna akili yenye busara.

Wa wafu wenyewe, na fahamu yao pia imekufa, wamenyimwa vyote viwili upendo na mpendwa.

Kwa kifupi Kurani ndio msingi wa dini yetu, hiyo hutuliza mioyo yetu yenye huzuni.

Nuru ya Furkani huvutia kwa Mungu, kwayo twaweza kuona Uso wa Mungu.

Twawezaje kufumba macho yetu tusimtazame yule Mpendwa? U wapi uso mzuri kama Uso wake?

Uso wangu kang'aa kutokana na nuru ya Uso wake, chochote ulichopata moyo wangu kimetokana na neema Zake.

Kadiri utambuavyo macho yangu uzuri wake, hakuna ajuaye. Nafsi yangu imejitoa mhanga kwa Jua hili la sifa kamilifu.

Penzi kama hilo ninalo kwa dhati ya Mustafa[saw]. Kama nyuni moyo wangu unaruka kuelekea kwa Mustafa[saw].

Tangu nilipohabarishwa kuhusu uzuri wake, moyo wangu hauna utulivu kutokana na penzi lake.

Mimi nauona uso wa mpendwa yule. Kama

mtu amtolee moyo wake, mimi kumshinda huyo nimtolee uhai wangu.

Huyo huyo mtunza roho ndiye aninyweshaye ambaye daima hunifurahisha kwa bilauri ya mvinyo.

Uso wangu umetokomea ndani ya uso wake, na toka nyumbani mwangu na mataani mwangu husikika harufu njema ya huyo huyo.

Nimejipoteza ndani ya penzi lake, mimi ni huyo huyo, ni huyo huyo, ni huyo huyo.

Roho yangu inajipatia chakula toka kwenye roho yake, na jua lile lile limechomoza toka kifuani mwangu.

Ahmad amedhihiri ndani ya nafsi ya Ahmad, ndio sababu jina langu likawa jina la mtu huyo asiye na kifani.

Nikawa sihitaji tena jaha wala heshima kutokana na penzi lake, siuwezi moyo, wala Sijijui hali yangu. Sina habari nyingine yoyote.

Ni uzushi dhidi yangu kuwa nageuka nisikikabili kizingati kile; ni uongo mkubwa ulioje huu wa hao mafasiki!

Je mtu kama mimi anaweza kupa kisogo

mpendwa huyu? Laana ya Mungu iwe juu ya wazo hili la adui.

Mimi ndiye yule ambaye utakiona kichwa changu kikiwa kimepakwa damu na mavumbi katika njia ya Mwongozi huyo.

Kama mtaani mwa mpendwa huyu ukipigwa upanga, mimi nitakuwa mtu wa kwanza kujitolea dhabihu ya uhai wake.

Kama hii ndiyo kufuru mbele ya maadui, basi ni mwenye bahati nzuri sana yule aliye kafiri kama mimi.

Watu hawa wameniita kafiri, dajali na mlaaniwa. Mimi sielewi hii ni imani na dini gani.

Tabia zao hizi ni ngumu kama jiwe. Kama vifuani mwao mna moyo, basi onyesheni uko wapi huo?

Shughuli za watu hao, wakati wote, ni kuzusha, na saa zote rafiki yao ni uroho na tamaa.

Mioyo yao imejaa uchafu, na batini zao shari, wako mbali sana na nia njema.

Nia njema inapokuwepo moyoni, huangukia

juu ya ua la ukweli kama kurumbiza,

Na hajiweki tayari kufanya shari, yeye humwogopa Yule Ajuaye siri zilizojificha.

Lakini ujasiri huu na kukosa haya, na uzushi juu ya uzushi,

Hiyo siyo kazi ya waaminio na wacha Mungu, wala sio maadili ya watawa wenye mioyo iliyotakasika.

Yule aliye mtumwa wa tamaa zake saa zote, nawezaje kumfahamu kuwa anamcha Mungu.

Wamejidhania kuwa wema; yasikitisha kwamba watu hao wamejielewa vibaya sana kiasi gani.

Kuzitii nafsi zao na kumkengeuka Mwenyezi Mungu, hiyo ndiyo alama ya wenye bahati mbaya.

Aliye na uchafu kama huo moyoni mwake, kama huyo anayo hata harufu ya imani ndani mwake, hapo mimi ni kafiri.

Mimi nimesoma mbele ya watu hao kile kitabu kisicho na shaka (yaani Kurani),

Pia nimetoa hata Hadithi za yule Mtume ambaye, kwa fadhili za Allah, ni mkweli na

ameepukana na upuuzi.

Lakini dhamira yao haikuwa ya kuukubali ukweli; kwamfaa nini kondoo kulia mbele ya mbwa mwitu.

Waliniita kafiri na kukengeuka na wakawa wana yakini kana kwamba wameona kwa kupasua moyo wangu.

Kuhusiana na hao, yule mfalme wa dini alisema vyema kabisa kwamba watu hao ni makafiri moyoni na ni waaminio kidhahiri.

Mdomoni mwao kuna Kurani, lakini mioyoni mwao mna huba ya dunia, kiburi na uadui.

Madai yao ya kuifahamu dini ni majisifu tu, kwani wakati wa kila vita wakakimbia.

Hao ndio wale majahili wasioifahamu lugha ya Kiarabu, wala Kurani Tukufu na siri zake zilizojificha.

Kiburi chao kilipofika kileleni, hapo ghera ya Mungu ikazichana mapazia yao.

Watu hawa ni maadui wa dini kama yule mwovu Shimar (aliyemwua Imam Husain[ra]), na dini ni mgonjwa na dhaifu kama Zainul 'Abidini.

Mwili wangu unatetemeka na roho na moyo wangu unagwaya nizionapo hiana zao.

Wamefanya hila nyingi, na bado wanaendelea kufanya, ili waivuruge vuruvuru nidhamu ya shughuli zetu.

Lakini jambo litokalo mbinguni lawezaje kafifia kwa husuda za mahasidi.

Ni kitu gani mie? Vita yao ni dhidi ya Mungu ambaye bustani hii na jumba hili vimejengwa kwa mikono Yake miwili.

Yule ajiingizaye kwenye kazi za Mungu, huyo kwa hakika anainuka kupigana vita na Mungu.

Sisi ni watu wenye kufa, na mshale wetu ni mshale wa Mungu, na windo letu, kwa hakika, ni windo la Mungu.

Mkweli huwa katika hifadhi ya Huyo Aliye wa Pekee, na mkono wa Mungu huwa unafichika ndani ya mkono wa vazi lake.

Yule anayepigana na Mungu kwa sababu ya uadui, yeye anaung'oa mzizi wake mwenyewe kama Shetani aliyelaaniwa.

Watu wengi ni kama Bal'am ambaye kazi yake huangamizwa na mikono ya Musa.

Mimi nimekuja katika wakati mwafaka kama mawingu ya majira ya kuchipua, na ninazo ishara mamia za hisani za Mungu.

Mbingu inyeshesha baraka kwa ajili yangu, ardhi nayo saa zote yasema kwamba wakati ndio huu huu.

Hizo mbili zimesimama kutoa ushahidi kunisaidia, hata hivyo majahili hawa wanaendelea kuniandama.

Yasikitisha kwamba watu hao ni vipofu na viziwi wa aina ya ajabu, mamia ya ishara wanaziona, lakini wanaenda zao wakighafilika.

Kwa nini wanaruka juu kiasi hiki kwa kiburi, pengine wanamkana Yule Dhati asiye na mfano.

Mungu Huyo anapomfadhili mtu, Humfanya kuwa wa mbinguni kutoka hali ya kuwa wa ardhini.

Humpa heshima kwa fadhili, hisani na ukarimu Wake. Huvifanya jua na mwezi kumsujudia.

Mimi sikujidaia madai haya, bali nimelifuata agizo la Mungu.

Hii ni kazi ya Mungu na siyo hila ya mwanadamu, adui yake ni adui wa Mungu Mwadilifu.

Yule Mungu Aliyenichagua, rehema zake zimenyesha mtaani kwetu.

Nilipokufa, Mpendwa wangu Akaja baada ya kufa kwangu, nilihiliki, uso Wake ukanidhihirikia.

Wimbi la penzi la Mpendwa lilikuwa na nguvu, hilo likashinda na kufagilia mbali vyote tulivyonavyo.

Mimi sina hazina ya amali, bali penzi likafurika na kazi zote hizi zikafanyika.

Unyenyekevu ukawa Tuur ya Mungu kwangu, ubinafsi ulipotoweka, ikaja nuru ya Mungu.

Mimi nikageukia upande Wake, kwani uso huo ndio unaostahili kutazamwa, na kila moyo uliobarikiwa huelekea Kwake tu.

Upo wapi uso kama wake duniani na Akhera, na u wapi mtaa minghairi ya mtaa wake!

Wale watu wanaoghafilika na mtaa wake ni dhalili kuliko hata mbwa koko.

Mahuluki na dunia imo ndani ya makelele

na zahama, lakini wapenzi wake wamo katika ulimwengu mwingine kabisa.

Yule mtu ambaye ule ulimwengu uliofichikana kwake, huyu mwenye bahati mbaya kaona nini baada ya kuja duniani.

Ni rahisi kwa wakweli kuipata njia ya Mungu. Amtafutaye Mungu, humpata tu Yeye.

Yeyote atakaye kuungana Naye kwa ukweli na nia safi, Mungu wa mbinguni humfungulia njia ya kumwendea.

Jicho la Mpendwa huwatambua wakweli; hila na ujanja havifai kitu hapa.

Kwa kumpata Mpendwa, ukweli wahitajika. Amtafutaye bila ya ukweli ni mpumbavu.

Mwenye kuwa na ukweli mbele ya Mungu, hatimaye humpata kutokana na baraka za uaminifu wake.

Mamia ya milango iliyofungwa hufunguka kwa sababu ya ukweli. Rafiki aliyepotea hurejea kutokana na ukweli.

Alama ya wakweli ndiyo hii kwamba huingia hatarini kwa ajili ya Mpendwa.

Hudumu kuitazama sura ya Mpendwa,

na huwa hawana habari ya kusifiwa wala kulaumiwa na watu.

Kwa ajili ya Akhera huwa matendo yao yote, imeokoka mioyo ile iliyojeruhika na kuvunjika kwa ajili ya Mungu.

Kazi hii huwa haitendeki kwa kusema tu maneno, uaminifu unahitajika kwa kufuzu.

Wataalamu wameifanya elimu yao kuwa sanamu, nao hushughulikia kuiabudu asubuhi na jioni.

Kama dini ingeitegemea elimu ya dhahiri tu, basi kila mtu asiyestahili angekuwa ni mwenye kuzifahamu siri za kidini.

Rafiki yetu Huiangalia batini, usiiringie sifa yako yoyote ile.

Yu Mtukufu na Mwenye shani kubwa, kwa ajili ya kumfikia yafaa kufanya vilio vingi (vya maombi).

Uhai umo ndani ya mauti, unyenyekevu na vilio vya maombi. Aliyeanguka, ndiye hatimaye atakayeinuka (akiwa hai)

Maadamu uchungu haufiki mpaka kwenye kutaa uhai, kilio chake hakifikii mlangoni pa

Mpendwa.

Atenganaye na majisifu ndiye ampataye Mungu. Kumpata ni kitu gani? Ni kujitenga na nafsi yako.

Lakini kuiua nafsi sio kazi rahisi, ni mamoja kufa na kuyaacha majisifu.

Mpaka upepo ule usivume juu ya uhai wetu, ambao upeperushe hata chembe ya dhati yetu,

Wawezaje kuonwa uso ule mzuri kutokana na mavumbi haya yaliyofanywa na watu.

Tusipojitoa kwa Mungu wetu na tusipojitokomeza ndani ya Rafiki yetu,

Tusipojitenga na dhati zetu, na kisipojaa kifua penzi lake,

Tusipofikiwa na malaki ya vifo twawezaje kuupata uhai mpya kutoka kwa Mpenzi huyo?

Asipojinyonyoa manyoya na mbawa zake za zamani, huwa vigumu kuruka kwa ndege wa njia hii.

Ni mwenye bahati mbaya mtu yule ambaye wakati wake umepotea, Rafiki yake Amekasirika na moyo wa maadui ukafurahi.

Sizikatai akili za wenye busara, lakini hiyo sio njia ya kumfikia Mpendwa.

Penzi, huba kali na umajununi visipokuwepo, Mpendwa huyo Asiye na kifani Haonyeshi mng'ao Wake.

Kwa kuwa Mpenzi yule mwenye heshima Amefichika, basi kila mtu anajichagulia njia yoyote ili kukutana Naye.

Lakini njia waliyoitumia wenye (kuitegemea) akili, kwa kujikalifisha wameuficha zaidi Uso wa Mungu,

Wakaweka mapazia juu ya mapazia ya awali, makusudio yalikuwa karibu, lakini wakayapeleka mbali zaidi.

Sisi tuliozing'arisha nyuso zetu kwa kumwona, tumempata kwa njia za upendo na kujipoteza ndani ya huba yake.

Sisi tulipotengana na kiburi chetu kwa ajili ya Mungu Yule, basi natija ya kujipoteza ndani Yake ikawa kuishi milele.

Katika njia hii mtu hastahili kuvumilia shida sana, Yeye Hutaka uhai wako tu, na kuutoa sio vigumu.

Kama Yeye Mwenyewe Asingeniita kwa fadhili na ukarimu wake, hapo hata kama ningejaribu namna gani, juhudi zangu zote zisingefaa kitu.

Kwa mtazamo mmoja tu Akanifanya mimi maskini kuwa mfalme, na akafupisha njia yetu ndefu.

Mpendwa Huyo Mwenyewe Akanifungulia mimi njia Yake, nalifahamu jambo hili jinsi mtunza bustani anavyolifahamu ua.

Anayetengana nami katika zama zangu, huyo mwenyewe anajidhulumu nafsi yake.

Kifua changu kimejaa nuru ya Mpendwa, mkono Wake Yeye ukaking'arisha.

Dhati yangu ikawa Dhati ya Yule Mpendwa wa azali, na kazi yangu ikawa kazi ya Mpendwa Yule wa tangu zamani.

Kwa kuwa roho yangu imefichika ndani ya Mpendwa wangu, kwa hiyo harufu nzuri ya Mpendwa imeanza kusikika kutoka ndani ya bustani yangu.

Ndani mwa shuka yangu mna nuru ya Mungu, Mpendwa huyo amejitokeza kifuani mwangu.

Jina langu ni Ahmad wa zama za mwisho, na bilauri ya mvinyo yangu ndiyo bilauri ya mwisho (kwa ajili ya dunia).

Ni habari njema kwa aitakaye njia ya Mungu kwamba Mungu Amemwonyesha zama za ufaulu.

Yule ambaye hamwoni rafiki yake, basi huyo huulizia habari zake kwa yeyote anayemfahamu.

Na yule amtafutaye mpenzi, anawezaje kutulia mahali pamoja.

Yeye hukimbia huko na huko, kama punguani, asaa akauona uso wa mpenziwe sehemu yoyote.

Yule ambaye moyoni mwake mmepenya penzi la mpendwa wake, basi kwa utengano wa rafiki huyo moyo wake hufadhaika.

Subira na utulivu upo wapi kwa wapendao! na kwawezaje kukengeuka kwa uso wa mpendwa!!

Aupendaye uso wa mpenzi, yeye huufikiria uso wake usiku na mchana.

Kama kwa bahati apate kutengana naye, hapo

hutengana roho yake na mwili wake.

Pasipokuwa na mpenzi, kila sekunde huyafanya maisha yake kuwa machungu.

Kisha anapoona uzuri wake na uso wake, basi humkimbilia kama mwenye wazimu.

Na hushika vazi lake kwa jazba kubwa akilonga, ‘ Ewe mpendwa, moyo wangu umejeruhiwa vibaya kwa kutengana nawe.'

Ikiwa ikhlasi kama hii imo ndani ya moyo wa mtu, basi huyo, kama kurumbiza, hulifanya ua kuwa maskani yake.

Kama uanguke kwa vilio na vite mia mbili, hapo lazima hujitokeza wa kukusaidia.

Kuliepuka jua ling'aalo kwa kufikiria kwamba mimi mwenyewe nitajizalishia mwanga kutoka ndani yangu,

Basi hizi huwa athari za kutofanikiwa. Mzizi wa bahati mbaya ni kiburi na dosari.

Wazo hili limeipofusha dunia na kuitumbukiza kisimani mwa upotevu kichwa chini.

Mwenye kiu hupaswa kuyakimbilia maji. Aliyetafuta kwa moyo wa kweli, hatimaye

akayapata makusudio.

Ni mwenye akili mtu yule autafutae mtaa wa mpendwa na kupoteza heshima yake kwa ajili ya uso wa mpendwa.

Hugeuka kuwa vumbi ili upepo ulipeperushe huko na huko, na ajifie ili yeyote amwonyeshe njia.

Bila ya ukarimu wa Mungu kazi haiwi kamilifu, ni mwenye busara tu ndiye ajuaye jambo hili. Wassalamu.

Hayo yote yaliyodhihirika kwa kalamu yangu ni kwa sababu ya hali halisi sio maneno tu, ni kwa jazba sio kwa juhudi ya kujikalifisha. Sasa afadhali kuomba ruhusa. Yaliyomo mononi mwangu Mungu Akufunulie hayo moyoni mwako pia. Huba huvutia huba. Pokea salamu kutoka kwa mheshimiwa ndugu yangu Maulawii Nurud Din na mheshimiwa Sirajul Haq Jamali. Maulawii Sahib huwa anakutaja kwa maneno mazuri. Ni ajabu kuwa katika maongezi mafupi tu, yeye kwa sababu ya huba na ikhlasi ameeleza kuwa ulimwambia kuwa ukimsalia Mtume kwa maneno fulani na utamwona Mtume Mtukufu[saw], basi usiku huo huo alipata heshima ya kumwona.

Wassalam,

Mwandishi
Ghulam Ahmad kutoka Qadian

**Barua ya tatu ya Bwana Khwaja**

Kwa mheshimiwa Mirza Ghulam Ahmad, mjuzi wa maana za ndani, mwenye maarifa, mwenye kutazama mambo ya kweli, mjuzi wa sheria na mwenye kumwomba Mungu msaada, na kumtegemea tu Mwenyezi Mungu.

Assalamu alaikum wa Rahmatullahi wa Barakaatuh. Jazba yangu ya kukuheshimu haina kikomo kama zilivyo khulka zako bora. U johari ya ardhi na mbingu. Mapenzi yako, unayejitahidi katika njia ya Mwenyezi Mungu, yanazidi kila saa. Mkarimu kama wewe usiye bahili umenijaza mimi kwa furaha na kunifanyia hisani sawa na afya yangu ya dhahiri na batini. U mwenye khulka njema, sifa nzuri, mwenye heshima, umenisaidia kwa kuniandikia. Barua yako imeniwasilia iliyojaa shada la lulu zing'aazo za huba na urafiki na shada la johari ng'aavu za ukweli na umoja, yaani ikhlasi, iliyojaa tele urafiki na upendo, iliyopambwa kwa ukarimu, ambayo imenifurahisha sana sana. Mimi nimepata furaha ya moyo kwa maneno ya huba na maana za kuchangamsha na kwa maarifa za kushangaza za mpiga mbizi wa bahari

za mwongozo. Na ile makala iliyosomwa katika Mkutano wa Dini, uliyoniletea ni maarifa mapya pamoja na kuwa masurufu ya mambo ya kweli. Moyo unayosikiliza yaliyo kama lulu. Daima usaidiwe na kuheshika, katika bidii zako za makusudio ya juu, kwa neema za ghaibu na ukarimu usio na shaka. Umenifikiria kuwa mtu wa kufaa kuambiwa hali zako zenye kufurahisha na pia umenifurahisha kwa kuniletea vijitabu bora na barua zenye thamani.

4 Shawali 1314 Hijriyya

Mwandishi

Ghulam Farid Alchishti, Alnidhami

Sajjada Nashin

Kutoka Chachrhan Sharif

Fakir Ghulam Farid
Mwenye kuwahudumia
mafakir 1301

Muhuri

Mwandishi: Awatakiye heri Wakristo    Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian

**TANGAZO LA ZAWADI**

**YA RUPIA ELFU MOJA**

Mimi hivi sasa kwa ahadi madhubuti natoa tangazo hili kuwa kama mtu yeyote mingoni mwa Wakristo aweze kuthibitisha ishara za Yesu zinazofikiriwa kuwa ndiyo dalili za uungu wake kwamba zinazidi na miujiza yangu katika uhaikisho madhubuti na katika wingi wa idadi, mimi nitampatia zawadi ya Rupia elfu moja.* Mimi nasema kweli kabisa na kwa kuapa kuwa haitafanywa kinyume chake. Mimi naweza kuziwekeza pesa hizi kwa mwuamuzi ambaye watu wa pande zote mbili watamkubali. Waamuzi watafanywa wengine wasiohusikana na makundi haya mawili.

Maombi yanatakiwa yaletwe haraka.

28 Januari 1897

*Tanbih: Kama waletao maombi ni zaidi ya mmoja, hao wanaweza kuzigawanya baina yao — Mwandishi.